# Nipashe

Jumatano Mei 8, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579912

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## UTAIFISHAJI DECI

Mahakama Kuu imeamuru mali zote zinazomilikiwa na Kampuni ya Development Enterpreneuship for Community...

UKURASA 4




## RCO AFA

Ofisa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Kipolisi Ilala, jijini Dar es Salaam, amefariki dunia katika ajali...

UKURASA 4



Spika Marekani amshukia Mwanasheria Mkuu, bado amgwaya Rais Trump

Ukurasa 20

Mvutano ndani ya chama tawala Kenya, Jubilee waongezeka?

Ukurasa 19

siasa

JUMATANO MEI 8, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Korea Kaskazini yatunisha misuli yake, yafyatua makombora masafa mafupi

Ukurasa 18

Dk. Bashiru: Urais umeipasua Zanzibar katika vipande vinne

• Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini na Pemba • Kurejea kufundisha chuo kikuu baada ya ukatibu mkuu

Na Mashaka Mgeta, Dodoma

INAENDELEA UK.16

Rais wa Zanzibar, Ali Mohamed Shein. PICHA: MTANDAO

Demokrasia Venezuela hatarini pande mbili zikiwania jeshi liwaunge mkono

Ukurasa 15

Siku 100 DRC za Rais Tshisekedi madarakani, amefanikisha nini? Ukurasa 19

UKURASA 13

# KWAHERI





REGINA



JACQUELINE



Rais John Magufuli akiongoza maelfu ya Watanzania kuaga mwili wa aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, katika ukumbi wa Karimjee, jijini Dar es Salaam jana. **Picha ndogo:** Mke wa marehemu, Jacqueline na watoto Regina, Abdiel, Ryan na Jayden, wakati wa kuaga mwili wa baba yao. **Picha zaidi Uk.7. PICHA: JOHN BADI /SELEMANI MPOCHI**

**MICHEZO** SIRI YA DK. MENGI STARS AFCON 2019 UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6



HUZUNI 1942 - 2019

# JPM aongoza maelfu ku

Na Romana Mallya

RAIS John Magufuli jana alishindwa kujizuia na kujikuta akijifuta machozi mbele ya jeneza lililokuwa na mwili wa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, ambaye aliagwa jana jijini Dar es Salaam.

Dk. Mengi alifariki dunia usiku wa kuamkia alhamis iliyopita nchini Dubai, Falme za Kiarabu.

Shughuli za kuaga mwili wa marehemu Dk. Mengi ambao ulirejeshwa nchini juzi, zilizofanyika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam, zilihudhuriwa na Rais Magufuli, mawaziri, wabunge, mabalozi wa nchi mbalimbali na viongozi wastaafu akiwamo Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi.

Wamo pia Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Mohamed Gharib Bilali; mawaziri wakuu wastafu John Malecela, Cleopa Msuya na Mizengo Pinda pamoja na Spika mstaafu, Anne Makinda.

Viongozi wengine waliohudhuria ni kutoka taasisi mbalimbali za serikali, sekta binafsi, taasisi za kitaifa na kimataifa.

Shughuli za kuaga mwili huo zilianza saa 5:15 asubuhi ambapo ziliongozwa na Rais Magufuli ambaye mara baada ya kupita kwenye jeneza hilo alionekana akitoa miwani yake na kufuta machozi.

Baada ya Rais Magufuli kuaga alifuata Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan na ndipo viongozi wengine wa serikali na wastaafu nao walipata nafasi hiyo.

Wengine ni wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, Katibu Mkuu Kiongozi John Kijazi, Mkurugenzi Usalama wa Taifa, Katibu Mwenezi CCM, Humprey Polepole, Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita.

Baada ya viongozi wakuu kumaliza kuaga, mwanamuziki wa nyimbo za injili, Joel Lwaga aliimba wimbo sitabaki nilivyo uliowatoa machozi waombolezaji wengi wakiwemo wanafamilia ya marehemu Dk. Mengi.

**SALAMU ZA SERIKALI**

Akitoa salamu za rambirambi za serikali, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema serikali inatoa pole kwa familia, mke wa marehemu, watoto, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na mpendwa wao Dk. Mengi.

"Tunatoa pole kwa wafanyakazi kwa kuondokewa wa kiongozi, sisi tunatambua mchango wake, upendo wa dhati na ukarimu wake aliokuwa nao kwa kipindi chote. Ni dhahiri kifo chake ni pigo kubwa, "alisema.

Alisema serikali, Watanzania na dunia kwa ujumla imepokea kwa simanzi na masikitiko taarifa za kifo cha Dk. Mengi kutokana na ukweli kwamba kifo chake kimekuwa cha ghafla mno.

Prof. Kabudi alisema baada ya serikali kupata taarifa kupitia ubalozi mdogo Dubai kwa kushirikiana na familia ulianza maandalizi ya kuhifadhi na kuusafirisha mwili wa marehemu kuja nchini.

Alisema licha ya muda kuwa mfupi ikizingatiwa siku ya Ijumaa ni ya mapumziko nchini humo, lakini walihakikisha nyaraka za kuusafirisha mwili huo zinapatikana siku hiyo hiyo saa 10 jioni na hatimaye juzi kuuleta Tanzania.

Prof. Kabudi alisema serikali inamshukuru Balozi Nassoro Mbaruku kwa kazi kubwa aliyoifanya kuhakikisha taratibu zinakamilika na mwili huo unarejeshwa nchini mapema.

"Kifo ni fumbo, na fumbo hili alijuaye ni Mungu peke yake, tunamshukuru Mungu kwa kila alichoamua, serikali imeguswa na kifo cha Dk. Mengi ambaye amefanya mengi katika maeneo ya uchumi, gesi, madini, kilimo na afya ametoa ajira, kuboresha mazingira ya biashara, kutoa ajira, amevutia wawekezaji, alichangia kushauri sera za kiuchumi, alikuwa na jawabu ya namna gani ya kuboresha sera zetu," alisema.

Prof Kabudi alisema Dk. Mengi amewezesha Tanzania kuwa nchi ya viwanda na kwamba serikali itaendelea kumuenzi kwa aliyoyaacha.

"Katika kulifanya hili kwa vitendo hivi karibuni alionyesha nia ya kuwekeza kwenye viwanda tofauti, kiwanda cha dawa, uunganishaji magari, simu, nidhahiri mchango wake ni mkubwa, Watanzania tunaweza kuwekeza nchini tukiwa na nia,"alisema

Alisema serikali inatambua mchango wake, moyo wake wa upendo na ukarimu hususani kwa wanyonge, maskini na watu wenye ulemavu.

Prof Kabudi aliongeza: "Hii ni ishara tosha moyo wa upendo, ukarimu na huruma na kuandaa chakula kwa ajili ya watu wenye ulemavu."

Alisema Dk. Mengi amepata tuzo mbalimbali duniani, amekuwa mdau mkubwa wa sekta ya mazingira na amehamasisha upandaji wa miti sehemu mbalimbali nchini ikiwamo kuzunguka Mlima Kilimanjaro.

Alisema kitabu chake cha I Can, I Must, I Will ni hazina kwa sababu kinafundisha mengi na aliwataka Watanzania wahamasike kukinunua ili kiwawezeshe kubadilisha hali ya maisha yao.

**SALAMU ZA TPSF**

Akitoa salamu za sekta binafsi, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Salum Shamte, alisema



Viongozi kadhaa wakiwa wamelibeba jeneza lenye mwili wa Dk. Reginald Mengi kuingia katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya shughuli ya kuuaga. Mbele kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka na kushoto ni Mbunge wa Vunjo, James Mbatia. **PICHA; SELEMAN MPOCHI**

# Jaji Werema, Mpina watoa neno

Na Salome Kitomari

MWANASHERIA Mkuu wa zamani wa Tanzania, Jaji Fredrick Werema, amesema wakati wa masiba ndiyo muafaka kwa familia kushikamana na kutoruhusu lolote kuwatenganisha.

Akizungumza baada ya kuaga mwili wa marehemu Dk. Mengi, Jaji Werema alisema wakati huu ni wa kuishi na kufuata aliyoyaacha na kuhakikisha yanakuwa endelevu, huku akiwataka wanaotumia mitandao ya kijamii kuacha kuiandika familia kwenye mitandao.


Werema alisema Watanzania wanapaswa kujifunza kutoka kwa Marehemu Mengi kwa kutokuwa watu wa ovyo

"Pamoja na kwamba unaweza kuwa huna kitu, lakini lazima utumie akili kufanya kitu cha maana kinachoweza kukuwezesha kwenda mbele badala ya kukaa kwenye vigenge na kupiga umbea," alisema na kuongeza:

"Kutafuta watu waliofanikiwa unaanza kuwarushia mawe na kamwe hiyo haiwezi kusaidia kitu hasa kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amemzugumzia Marehemu Dk. Reginald Mengi kama kiongozi aliyetumia maisha yake kubadilisha mifumo ya sera, sheria hasa kwenye eneo la biashara, uwekezaji na ushiriki wa wazawa katika kujenga uchumi. Waziri Mpina amesema Taifa limempoteza mwalimu wa viongozi. Alisema enzi ya uhai wake marehemu Dk Mengi akiwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) licha ya kuwa hakuwa kiongozi wa Serikali, lakini mawazo yake yaliwezesha kubadilishwa kwa sera nyingi hasa suala la Watanzania kushiriki katika uwekezaji.

Alisema msiba huo ni funzo kubwa kwa taifa hasa katika kipindi hiki ambacho taifa linakwenda kwenye uchumi wa viwanda.



HUZUNI 1942 - 2019

# ...umuaga Dk. Mengi

Mungu amechukua roho yake lakini nyota yake itaendelea kung'aa na kuonyesha njia.

"Tumempoteza mwasisi kiongozi, muongoza njia na mpendwa wetu aliyekuwa na mchango mkubwa kwenye sekta binafsi na uchumi wa nchi," alisema.

Alisema baada ya kupata taarifa za kifo chake, Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, aliwawakilisha kwenda Dubai kushirikiana na serikali na familia kukamilisha taratibu za kuurejesha mwili nyumbani.

Shamte alisema Dk. Mengi alikuwa muumini wa ushirikiano wa sekta binafsi na umma kwa sababu ndiyo nguzo muhimu kuleta maendeleo ya nchi.

Shamte alisema Dk. Mengi alikuwa nguzo muhimu katika sekta binafsi kwani aliiongoza kwa miongo minne na muda wote mchango wake ulikuwa mkubwa na wenye manufaa kwao.

Aliongeza kuwa Dk. Mengi alitamani nchi iwe na mabilionea wengi kumzidi yeye kwa sababu aliamini hilo linawezekana iwapo watu watafanyakazi na kuamini kwamba wanaweza.

"Jukumu la kutengeneza wajasiriamali ni letu sote kwa kuwajenga watoto kuanzia shule na kuweka mazingira bora, aliamini dhana pana ya uongozi wenye maadili na alithubutu kukemea

INAENDELEA UK. 8



## Jumuiya ya Afrika Mashariki yamlilia

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Afrika Mashariki (EAC), imesema wakati wa uhai wake, Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Marehemu Dk. Reginald Mengi, alitoa mchango mkubwa kuiendeleza jumuiya hiyo.

Taarifa ya Katibu Mkuu wa EAC, Balozi Liberat Mfumukeko kwa vyombo vya habari, ilisema Dk. Mengi alikuwa mtu aliyependa kuwapo kwa ushirikiano katika biashara, soko la pamoja kwenye nchi zinazounda jumuiya hiyo.

Alieleza kuwa EAC ilipata mshtuko mkubwa baada ya kupokea taarifa ya kifo chake kwa kuwa alikuwa nguzo muhimu kwa ustawi wa Jumuiya.

Alieleza kuwa Dk. Mengi amechangia kwa kiwango kikubwa kuindeleza EAC kwenye uhusiano wa pamoja kupitia taasisi binafsi, alikuwa mtu muhimu wakati wa mkataba wa ushuru wa pamoja uliosainiwa mwaka 2004.

"Aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bodi ya Taasisi ya Sekta binafsi ya Afrika Mashariki, iliyokuwa na lengo la kuiweka Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye ushirikiano wa pamoja kupitia biashara na uwekezaji," alisema balozi Mfumukeko.

Alisema Dk. Mengi alikuwa ni mtu wa pekee, aliyeona mbali, alijitoa kuweka daraja la wengine kufanikiwa, aligusa maisha ya kila mtu katika EAC.

Alisema EAC inaomboleza kuondoka kwa mtu wa kipekee Tanzania na Afrika Mashariki ambaye ameacha alama ya kudumu kwenye mioyo ya watu.

## MCT: Dk. Mengi alisimamia uhuru wa habari

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limeelezea kusikitishwa kwake na kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, ambaye alisimamia uhuru wa vyombo vya habari na alipenda kuona tasnia ya habari inakua na kujiendesha yenyewe.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Kajubi Mukajanga kwenye salamu zake za rambirambi, alimwelezea Dk. Mengi kuwa ni mtu ambaye aliwaendeleza waandishi wa habari kielimu nje na ndani ya nchi.

"Baraza la Habari Tanzania limepokea kwa mshtuko na majonzi makubwa sana taarifa za kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP kwasababu marehemu amesaidia waandishi wengi kupata elimu na ajira," alisema Kajubi.

Alisema Baraza linatoa pole kwa familia yake, wafanyakazi na tasnia ya habari kwa kumpoteza mtu aliyekuwa nguzo kwa familia ya wanahabari na kiongozi kwa wamiliki wa vyombo vya habari na mfano wa kuigwa.

**WCF YAMKUMBUKA**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Masha Mshomba, amesema mfuko huo utamkumbuka Dk. Mengi, kwa kuwa miongoni mwa wachangiaji wakubwa wa mfuko huo.

Alisema Dk. Mengi kupitia kampuni yake alikuwa akitoa ushirikiano mkubwa sana katika mfuko huo wa fidia kwa wafanyakazi na kuhamasisha kampuni nyingine ambayo alikuwa na urafiki na wamiliki wake kujiunga katika mfuko huo. "Tunasikitika sana kumpoteza Dk. Mengi kwasababu alikuwa ni mdau mkubwa kampuni yake yalikuwa ni wachangiaji wazuri katika mfuko hivyo basi nakuomba mgeni rasmi kabla hatujaanza mafunzo haya naomba tusimame kwa dakika moja ili kumkumbuka ndugu yetu," alisema Mshomba.

## 'Dk. Mengi alitupa mil. 10/- tusiwe ombaomba'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA cha watu wenye ualbino (TAS) na Shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu vilivyopo wilayani Kahama, vimesema Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi aliwapatia Sh. milioni 10 kwa ajili ya kujiinua kiuchumi ili wasiwe tegemezi.

Mwenyekiti wa chama hicho, Ngassa Mrisho, alisema hayo jana kuwa katika kipindi cha 2005 Mengi alifika wilayani Kahama na kuwakabidhi watu wenye ualbino kiasi cha Sh. milioni 10.

Alisema, lengo la kuwapatia kiasi hicho cha fedha ni kuanzisha mitaji midogo na kujinyanyua kiuchumi ili kuondokana na dhana ya kuwa tegemezi kwenye jamii jambo ambalo mpaka sasa asilimia kubwa ya watu wenye ualbino wanajishughulisha.

"Wakati wa uhai wake Dk. Reginald Mengi alikuja Kahama na kuguswa na hali ya watu wenye ualbino kwa kutoa kiasi cha Sh. milioni 10, ndani ya fedha hizo wapo watu wengi wanaendelea kunufaika hadi leo wamenyanyuka kiuchumi kupitia fedha hizo," alisema.

Aidha, alisema wapo matajiri wakubwa hapa nchini zaidi ya Dk. Reginald Mengi kwa kuwa mioyo yao haijafunguka kusaidia wanyonge ndiyo maana Mengi anaendelea kuonekana ni tajiri mkubwa na mwenye moyo wa kusaidia watu.

Naye Mwenyekiti wa shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu katika Halmashauri ya mji wa Kahama, Michael Nkanjiwa, alisema Dk. Mengi aliwaunganisha wenye ulemavu na makundi mengi kwa kuwapatia misaada ambayo imewafanya kutokuwa tegemezi.

Nkanjiwa aliwaomba wafanyabiashara na matajiri kuiga mfano wa Dk. Mengi katika kusaidia jamii hasa watu wenye ulemavu na ualbino ili wasije wakazagaa mitaani kwa kukosa mitaji na kuwa tegemezi kwa jamii.

Alisema kabla ya halmashauri za mji na wilaya kutenga fedha asilimia mbili kwa ajili ya watu wenye ulemavu na fedha alizokuwa anazitoa Mengi, walikuwa wanadharaulika kwenye jamii na kuitwa ombaomba.

# Waziri Lukuvi asimamisha

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dorothy Mwanyika, awasimamishe kazi wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya ya Karagwe na Kibaha kutokana na kulalamikiwa na wananchi kupokea rushwa.

Lukuvi amewataja wenyeviti hao kuwa ni Rugate Assey wa Karagwe na Jerome Njiwa wa Kibaha.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Dodoma, Waziri Lukuvi alisema katika kutatua migogoro ya ardhi, wizara imeunda mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya 97 kwa ajili ya kushughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama na Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura 216.

"Nimekuwa nikipokea tuhuma kuhusu utendaji wa wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya hususani mabaraza ya Wilaya ya Karagwe na Kibaha.

"Kwa mamlaka niliyonayo, namwagiza Katibu Mkuu kuanzia leo (jana), kuwasimamisha kazi hao wenyeviti ili kupisha uchunguzi.

"Waliosimamishwa ni Rugate Assey, Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Karagwe na Jerome Njiwa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Kibaha.

"Tuhuma ni kwamba wamelalamikiwa na watu wengi kwamba wanapokea rushwa," Waziri Lukuvi alisema.

INAENDELEA UK. 8



Wachuuzi wakisubiri wateja wa bidhaa zao katika soko la Ilala, jijini Dar es Salaam jana wakikabiliwa na changamoto ya maji machafu yaliyotuama kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika Jiji hilo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mahakama yaamuru mali zote za DECI kutaifishwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, imeamuru mali zote zinazomilikiwa na Kampuni ya Development Enterpreneuship for Community Initiative (DECI) ikiwamo magari, mali zisizohamishika (nyumba) na Sh. bilioni 14.3 kutaifishwa kuwa mali ya serikali.

Kadhalika imemwagiza Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kubadilisha umiliki wa magari kutoka DECI kwenda kuwa ya serikali, Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), aliwasilisha maombi mahakamani ili madalali wakawahamishe wananchi wanaoishi kwenye nyumba hizo kuwa za serikali.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Stephen Magoiga.

Alisema mali zisizohamishika ikiwamo nyumba zibadilishwe majina ya umiliki kutoka DECI kuwa kwa jina la Msajili Hazina.

Akifafanua hukumu hiyo, jaji alisema akaunti za kampuni hiyo zilizopo benki ya NMB tawi la Msasani, benki ya Community tawi la Uhuru na KCB tawi la Samora, wahamishe Sh. bilioni 14.3 kutoka kwenye matawi yao kwenda serikalini mara watakapopokea amri ya mahakama yake.

"Nimepitia hoja za mlalamikaji (DPP) na walalamikiwa Wakurugenzi wa DECI, Jackson Mtares, Dominick Kigendi, Timotheo Saiguran Ole Loitg'nye na Samwel Mtares, bila kuacha shaka walalamikiwa wameshindwa kuthibitisha kwamba mali na fedha taslimu zimepatikana na chanzo tofauti na kampuni hiyo," alisema na kuongeza:

"DPP katika maombi yake amewasilisha vielelezo kuthibitisha kwamba mali zote zilipatikana kwa fedha za upatu, zilizopatikana kwa njia isiyo halali, lakini walalamikiwa hawajawasilisha majibu yoyote yanayopinga maombi hayo au kufafanua upatikaji wa mali hizo tofauti na vielelezo vya mlalamikaji, mahakama yangu inaamuru mali zote zitaifishwe kuwa mali za serikali," alisema Jaji

INAENDELEA UK. 8




# RCO Dar alivyokufa ajalini

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Upelelezi wa Mkoa wa Kipolisi Ilala jijini Dar es Salaam (RCO), Anael Mbise (50), amefariki kwenye ajali iliyohusisha gari aina ya Prado na basi mali ya Kampuni ya KVC.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Hamis Issa, aliliambia Nipashe jana kuwa ajali hiyo ilitokea jana maeneo ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro.

Kamanda Issa alimtaja matu mwingine aliyefariki kwenye ajali hiyo ni Frank Macha (35) ambaye ni fundi umeme mkazi Dar es Salaam na majeruhi ni kondakta Samson Macha (23) aliyevunjika mguu wa kushoto.

Alimtaja mtu mwingine aliyekuwa kwenye gari hilo la RCO ni Daniel Macha (35) ambaye ni fundi magari mkazi Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam aliyetoka salama.

Kamanda Issa alisema ajali hiyo ilihusisha magari mawili ambayo ni basi aina ya Tata lenye namba T 851 DKG mali ya KVC na gari aina ya Prado T 558 AUV ambayo marehemu na wenzake walikuwamo.

Alisema wakati wa tukio hilo basi la KVC lilikuwa likitokea Moshi Mkoa wa Kilimanjaro kuelekea Wilaya ya Same wakati Prado ilikuwa ikitokea Same kuelekea Moshi.

"Wakati ajali hii inatokea kulikuwa na mvua na kwa mujibu wa mashuhuda Prado lilihama upande wake na kwenda kugongana na Tata upande mwingine, na ndipo wakafa hao watu wawili akiwamo RCO, majeruhi yupo hospitali ya Wilaya ya Same," alisema.

## HABARI KITAIFA



Acky Charles wa Dartcom Miles (wapili kushoto) akiwaelekeza wafanyakazi wa Vodacom Tanzania juu ya matumizi ya vifaa mbali mbali vya usalama, katika hafla ya kuhitimisha wiki ya afya na usalama iliyofanyika makao makuu ya kampuni hiyo Jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi wamkamata mbunge Chadema akiwa bungeni

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Kibamba, John Mnyika (Chadema), amelieleza Bunge kuwa Mbunge wa Mbozi, Pascal Haonga (Chadema), juzi alikamatwa na polisi akiwa getini wakati akitoka bungeni baada ya kusitishwa kwa shughuli za chombo hicho cha kutunga sheria.

Mnyika ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Tanzania Bara, aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana aliposimama na kuomba kutoa hoja ya kujadili jambo la dharura mara tu baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali'.

Mnyika alisema alirejea mwongozo uliotolewa na Spika Job Ndugai wa kuzuia wabunge kukamatwa na polisi wakiwa bungeni isipokuwa kwa kibali chake.

"Mheshimiwa Spika alitoa mwongozo juu ya utaratibu wa Jeshi la Polisi kuwakamata wabunge wakati Bunge linaendelea kwamba ni kinyume cha haki za Bunge, lakini jana (juzi) usiku Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi lilimkamata Mbunge wa Mbozi, Mheshimiwa (Pascal) Haonga alipotoka tu getini hapo na limemlaza ndani.

"Leo (jana) wakati kipindi kikiendelea kipindi cha 'Maswali', limekuja naye hapa bungeni kwa ajili ya kuwachukua wabunge wengine kutoka kwenda naye na 'kum-search' (kumpekua) kwa kuandika ujumbe tu Mei 2018 kwenye kundi la wabunge la mtandao wa WhatsApp.

"Sasa, Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya polisi kuwakamatakamata wabunge wakati Bunge likiendelea vimekuwa vikikithiri.

"Kwa hiyo, naomba kutoa hoja jambo hili lijadiliwe na Bunge ili kukomesha tabia hiyo na Mheshimiwa Haonga aachiwe mara moja ili aendelee na kazi zake na utaratibu ufuatwe kama ambavyo Mheshimiwa Spika aliwahi kutoa mwongozo. Naomba kutoa hoja," Mnyika aliwasilisha.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Bunge, Najma Murtaza Giga, aliyekuwa anaongoza kikao cha chombo hicho, alizuia hoja hiyo kujadiliwa na Bunge, akieleza kuwa katazo la Spika linahusu ukamataji wa wabunge waliomo ndani ya Bunge na si vinginevyo.

"Hoja hiyo haiwezi kukubaliwa kwa sababu mwongozo wa Mheshimiwa Spika ni kwamba mtu yeyote hatatakiwa kukamatwa ndani ya Bunge mpaka kibali cha Spika, lakini nje ya Bunge hana mamlaka hayo," Giga alisema.

# Bunge labaini uhaba mkubwa wa watumishi sekta ya afya

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BUNGE limesema limebaini uhaba wa watumishi wa afya nchini kwa sasa ni takribani asilimia 50.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka ujao wa fedha, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Peter Serukamba, alisema kamati yake imeshuhudia uhaba huo katika taasisi za afya kama vile Hospitali ya Mwananyamala ambayo ina upungufu wa watumishi kwa asilimia 47.

"Kamati inashauri Serikali kuiangalia hospitali hii na hospitali nyingine zenye upungufu na kuzipa umuhimu wa kipekee wa kuzipatia wataalamu wa kutosha," alisema.

Serukamba pia alisema kamati imebaini changamoto ya malipo mbalimbali zikiwamo motisha ya posho ya nyumba, motisha ya saa za ziada kwa watumishi wa afya ni

INAENDELEA UK. 8

# Dk. Shein asifu ushirikiano na Brazil

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuna umuhimu mkubwa wa kuendeleza ushirikiano kati ya Zanzibar na Brazil kwa maslahi ya wananchi wa nchi mbili hizo.

Dk. Shein alisema hayo jana Ikulu mjini hapa, alipokuwa akizungumza na Balozi wa Brazil nchini, Antonio Augusto Cesar, aliyefika kwa ajili ya kujitambulisha.

Dk. Shein alisema Zanzibar na Brazil zina uhusiano wa muda mrefu na zimekuwa zikishirikiana katika masuala mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ya kiuchumi na kijamii

Alisema pamoja na nchi hizo kutofautiana kwa ukubwa wa eneo na kupatikana katika barabara tofauti, zimekuwa zikishirikiana kwa karibu, huku Zanzibar ikiwa na mengi ya kujifunza kutoka nchi hiyo, ikiwamo suala la kuiendeleza sekta ya utalii.

Alisema Zanzibar ambayo kabla ilikuwa ikilitegemea zao la karafuu kuendesha uchumi wake, imebarikiwa kuwa na vivutio na rasilimali kadhaa za utalii hususan kupitia uchumi wa bahari (Blue Economy), eneo ambalo kuna mambo mengi ya kufanya.

Dk. Shein alimweleza Balozi huyo dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuvutia wawekezaji kutoka Brazil katika nyanja mbalimbali, ikiwamo sekta ya utalii, ili kuimarisha uchumi wake.

SALAMU ZA POLE NA RAMBIRAMBI

tnbc



21521690Z

Katibu Mkuu Kiongozi na Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Balozi Mhandisi John W. H. Kijazi, Wajumbe na Watumishi wote wa Baraza la Taifa la Biashara, wanatoa pole nyingi kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki, wafanyakazi wa IPP na wote walioguswa kwa kuondokewa na mpendwa wetu **Dkt. Reginald A. Mengi.**

Pamoja na kutekeleza majukumu mengine mbalimbali ya manufaa kwa Taifa letu, katika uhai wake Dkt. Reginald A. Mengi pia alikuwa mjumbe wa Baraza la Taifa la Biashara ambalo linaongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli, na pia alikuwa Mwenyekiti Mwenza wa Kamati Tendaji ya Baraza hilo kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2018. Daima tutaukumbuka na kuuthamini mchango wake mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu kupitia uwekezaji wake katika sekta mbalimbali pamoja na kuhamasisha ukuaji na maendeleo ya sekta binafsi; kuhamasisha ushiriki wa watanzania katika shughuli za kiuchumi; kutoa nafasi za ajira; na kujitoa kwake katika kusaidia makundi mbalimbali ya wenye uhitaji.

*Pumzika kwa Amani Dkt. Reginald A. Mengi.*

BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA JINA LA BWANA LIBARIKIWE

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Tusikubali imani za kijinga zitukoseshe maendeleo*

**TAARIFA** kwamba zahanati moja wilayani Sumbawanga mkoani Rukwa, imefungwa na serikali kwa zaidi ya mwezi mmoja, kutokana na hofu ya imani za ushirikina ni za kusikitisha sana.

Habari hizo zilichapishwa katika toleo letu la jana, ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, ilitangaza kuwa umeifunga zahanati ya kijiji cha King'ombe kutokana na watendaji wa zahanati hiyo kutishiwa na matukio ya kishirikina wawapo kazini.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Jacob Mtalitinya, alisema halmashauri imeamua kuifunga zahanati hiyo mpaka hapo uongozi wa kijiji utakapokaa na wakazi wa kijiji hicho ili wakubali kuachana na vitendo hivyo.

Alisema zahanati hiyo ilifungwa zaidi ya mwezi mmoja uliopita, kutokana na watumishi wa afya waliokuwa wakifanya kazi katika zahanati hiyo kulalamikia kuwapo vitendo vya kishirikina. Alisema serikali haiamini masuala ya ushirikina, lakini kama vitendo vizuri vipo hata vibaya vipo pia, na kuwa vitendo hivyo vimejenga hofu kwa watumishi.

Mkurugenzi huyo alisema anasubiri taarifa ya kikao hicho na wakishakaa na kuonyana kuhusiana na tabia hizo, wakati wowote zahanati itafunguliwa, lakini ni vigumu kwa sasa watumishi kuendelea na kazi kwa kuwa wameingiwa na hofu.

Imedaiwa na baadhi ya watumishi wa zahanati hiyo kuwa walikuwa wakipigwa makofi na watu wasioonekana, kuanguka kifafa na wakati mwingine walikuwa wakikuta funza wamejaa katika vyumba vya kutolea huduma.

Kutokana na mazingira hayo, walitoa taarifa kwa uongozi wa Manispaa ambao uliamua kuifunga, hatua ambayo imeelezwa na baadhi ya wanakijiji hicho kuwa imewasababishia usumbufu, kutokana na kulazimika kutembea umbali mrefu kwenda maeneo mengine kufuata huduma za afya.

Imani potofu za kishirikina ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya jamii na kama wanajamii husika hawataamua kuachana nazo, wajue kuwa watakosa maendeleo mwa kipindi kirefu, huku wenzao katika maeneo mengine wakiendelea kwa kasi.

Matukio ya kishirikina yamekuwa yakitajwa kuwa chanzo cha baadhi ya maeneo nchini kukumbwa na watumishi kadhaa wa serikali kutokana na kuhofia maisha yao, na wakati mwingine watumishi wapya huamua kukataa kwenda katika maeneo hayo wanapopangiwa kuanza kazi au kuhamishwa.

Hali hiyo pia huchangia watumishi wa umma walioko katika maeneo hayo kukosa morali wa kazi kutokana na kuishi kwa hofu na kutojiamini kutokana na imani hizo potofu.

Kimsingi, imani za kishirikina zinapaswa kupigwa vita kwa nguvu zote na jamii yetu kama tunataka maendeleo, vinginevyo, maeneo yatakayoziendeleza na kuziendekeza zikubali kubakia nyuma kimaendeleo. Tunasema hivyo kutokana na athari watakazozipata zikiwamo kukimbiwa na watumishi wa sekta za afya, elimu, sheria na nyingine ambazo zinagusa maisha yao moja kwa moja.

Hakuna mtumishi wa umma kama mwalimu, daktari, muuguzi na hakimu ambaye atakuwa tayari kupangiwa kufanyakazi katika jamii isiyostaarabika, ambayo inawatishia maisha badala ya kuwapa ushirikiano na kuishi nao vizuri.

Kibaya zaidi ni kuwa wanaoathirika zaidi kutokana na imani hizo ni wananchi wengi, ambao wanakosa huduma za afya, elimu na nyinginezo muhimu.

Kwa kuwa kwa muda mrefu suala la elimu kwa jamii kubadilika na kuachana na imani potofu kama za kishirikina, tunaona kuwa kuna haja ya jamii, wadau na serikali kuchukua hatua nyingine kusudan za kisheria dhidi ya watu wachache ambao watabainika kuhusika. Kamwe tusikubali imani za kijinga zitukoseshe maendeleo kwa sasa na kwa vizazi vijavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## *Kufanya kazi kwa mazoea hakufai zama hizi, tuache*

Na Raphael Kibiriti

**MOJA** ya vikwazo vinavyokwamisha gurudumu la maendeleo ya taifa ni cha watu kufanya kazi kwa mazoea.

Na ndiyo maana kinaendelea kupigwa vita kwa nguvu na serikali ya awamu ya tano, ili kisiwe sehemu ya utamaduni wa Mtanzania.

Kwa miongo sasa, suala la watu kufanya kazi zao kwa mazoea, likijionyesha kwa uwazi upande wa watumishi wa umma, limekuwa ni kama utamaduni wa kawaida.

Wahenga wanasema mazoea hujenga utamaduni na watalaam mbalimbali wanabainisha wazi kuwa mazoea ni adui mkuu wa ufanisi, iwe katika sekta ya umma au binafsi, iwe kwenye biashara mpya au za zamani.

Kwa nini? Kwa sababu katika zama hizi za mabadiliko makubwa ya kimaendeleo, zama za sayansi na teknolojia, zama za utandawazi, kunahitajika nidhamu ya kipekee ya utendaji kazi.

Nidhamu inayoongozwa na sheria, kanuni na taratibu za kitaasisi ili kuweza kufikia maendeleo ya watu na taifa kwa ujumla.

Na kwa kulitambua hilo, baada ya awamu ya tano kuingia madarakani, Rais John Magufuli aliwaonya watumishi wa umma kuachana na utamaduni huo.

Akachukua hatua madhubuti za kuwatambua wale wote ambao hawakuendana na maelekezo yake ili kuonyesha anamaanisha anachokisema.

Dk. Magufuli akawataka wasaidizi wake kwenye wizara, idara, mashirika na taasisi za umma waongozwe na sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma zinazowataka wawatumikie wananchi kwa mujibu wa miongozo ya ofisi zao.

Hata hivyo, Muungwana anaona kwamba suala la kuchukulia vitu kwa mazoea ni kama imekuwa utamaduni si tu kwa watumishi wa umma, bali hata kwa wananchi wa kawaida.

Na matokeo yake, ndiyo hasara tunazoendelea kuzishuhudia kama nchi karibu kila siku.

Hasara za kupotea kwa maisha ya watu, wengine wakiambulia vilema vya maisha, uharibifu wa mali na hatimaye kuathiri uchumi wa nchi.

Kinachomshangaza Muungwana ni kwamba bado baadhi yetu tunaendelea na utamaduni huo wa kufanya kazi kwa mazoea na hatusikii la Mwadhini wala Mnadi swala na hivyo kuishia kusababisha majanga makubwa.

Na hiyo ni pamoja na maelekezo, maonyo na tahadhari zinazotolewa na viongozi wa serikali, wa dini, wa kimila na taasisi mbalimbali, yanayobainisha madhara ya kufanya kazi kwa mazoea.

Kwa mfano tafiti mbalimbali zilizofanywa nchini, zinaonyesha asilimia 75 ya ajali za barabarani zinatokana na makosa ya kibinadamu, huku asilimia 50 ya makosa hayo yakihusiana na mambo ya kibinadamu yanayofanywa na madereva.

Lakini mpaka sasa bado unakuta dereva wa Kitanzania anaendesha gari huku akiongea na simu, 'akichati' au akizungumza na mtu wa pembeni.

Bado unakuta dereva wa Kitanzania akipita kwenye taa ambazo hazimruhusu, hasimami kwenye alama za pundamilia ama akipita gari la mbele bila ya kuchukua tahadhari na matokeo yake ni ajali.

Ukimuuliza ana majibu yasiyo na mashiko, kwamba hajaanza leo kuendesha gari akiongea na simu au akichati.


Tunaambiwa kwa mfano tuachane na mazoea ya kuchoma moto misitu au kukata miti ovyo, kwani yanagharama kwa maisha yetu, hatusikii.

Takwimu za uhifadhi wa mazingira zinaonyesha kuwa Tanzania hupoteza takribani hekta 400,000 za misitu kila mwaka kutokana na miti kukatwa kwa sababu ya mazoea.


Matokeo yake ni mabadiliko ya tabianchi ambayo ndiyo chanzo cha mafuriko na vimbunga kama Idai au Kenneth tulivyovishuhudia nchi jirani za Msumbiji, Malawi na Zimbabwe. Tunaambiwa na wataalamu wa afya tuweke mazingira yetu katika hali ya usafi ili kuepukana na magonjwa kama ya kuharisha na kipindupindu.

Lakini kutokana na mazoea ndio haohao tunaofungulia maji ya chooni na kuyaelekeza kwenye mitaro ya maji na hatimaye magonjwa ya kuambukiza.

Ni wakati sasa kwa Watanzania wa kuachana na utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea, ili kuliepusha taifa na majanga ambayo kimsingi yanaepukika.



# HUZUNI 1942 - 2019





Watoto wa marehemu Dk. Reginald Mengi, Regina na Abdiel, wakiaga mwili wa baba yao, katika Ukumbi wa Karimjee, jijini Dar es Salaam jana.



Mke wa marehemu, Jacqueline, akiaga mwili wa mumewe.



Umati wa waombolezaji wakiwa wamekusanyika nje ya ukumbi wakisubiri kuaga.



Baadhi ya watu wenye ulemavu wakipita kutoa heshima zao za mwisho.



Waombolezaji wakipita mbele ya jeneza lenye mwili wa Dk. Reginald Mengi, kutoa heshima za mwisho. **PICHA ZOTE: JOHN BADI**



Jeneza lenye mwili wa Dk. Reginald Mengi, likiwasili nyumbani kwake, Kinondoni, baada ya shughuli ya kuaga kumalizika katika Ukumbi wa Karimjee.

# JPM aongoza maelfu kumuaga Dk. Mengi

INATOKA UK. 3

rushwa hadharani kwa kutaja majina," alisema Shamte.

Alisema Dk. Mengi alipenda kuwawezesha wananchi kiuchumi ambapo aliamini kwamba kwa utajiri ambao nchi imebarikiwa kuwa nao wananchi wake hawakupaswa kuwa maskini.

Shamte alisema Dk. Mengi aliamini dhana ya uongozi wa kujitolea na alikubali madaraka na kuongoza taasisi nyingine mbali ya kampuni zake.

Alisema Dk. Mengi aliishi maisha yenye unyenyekevu na kujali wasiojiweza na kwamba kitabu alichokiacha ni wosia tosha kwa Watanzania hivyo wanapaswa kukisoma ili kujiongezea maarifa na ujuzi zaidi.

**BALOZI UFARANSA**

Naye Balozi wa Ufaransa nchini, Frederick Clavier, alisema Dk. Mengi alikuwa mshauri mzuri na kwamba tangu aje nchini yapo mengi amejifunza kutoka kwake ikiwemo fursa.

**SHIVYAWATA**

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye ulemavu (Shivyawata), Ummy Hamis, alisema mara nyingi alikuwa akisimama kumshukuru Dk. Mengi kwa namna alivyoshiba maisha yao.

"Tulipokea kwa mshtuko na tumefadhaika na kuumia sana kwa sababu alikuwa akitetea jamii yetu kiuchumi, utu wetu, kisiasa na kijamii kwa kuamini utu na uzalendo," alisema.

Pia alisema: "Hakika kwetu alikuwa baba mshauri na mtetezi wetu, alitumia ushawishi wake kuwaita rafiki zake kuunga mkono masuala ya walemavu, alianzisha 'Dk. Reginald Mengi Foundation for Disability' na mwaka jana alianzisha tuzo za I Can ambazo mwaka huu tulipatiwa zawadi mbalimbali."

**KAULI YA CCM**

Katibu wa Itikadi na Uenezi, Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, alisema zipo aina mbili za matajiri duniani ambapo ya kwanza ni waliobarikiwa utajiri, wazalendo wa taifa ambao hutumia kusaidia watu na ya pili ni wale waliopata kwa ujanja ujanja na kujinufaisha wenyewe.

Polepole alisema Dk. Mengi alibarikiwa neema ya utajiri na alikuwa mshauri wa uchumi na kila kulipokuwa na mkwamo kati ya serikali na sekta binafsi alishauri namna bora ya kutatua matatizo hayo kabla mambo hayajaharibika.

**JAMES MBATIA**

Mbunge wa Vunjo (NCCR Mageuzi), James Mbatia, alisema amemfahamu Dk. Mengi miaka 28 iliyopita na katika kipindi cha mwaka huu alimshirikisha mambo yake mengi.

Alisema Machi 20, mwaka huu kwenye mazungumzo ofisini kwake, Dk. Mengi alizungumzia maridhiano ya vyama ili uchaguzi ujao usimwage damu na kusisitiza kuwa maisha yapo kwenye ndimi, hivyo zikitumika vizuri Tanzania itakuwa salama. "Maisha mema ya Dk. Mengi iwe sauti huru na haki na matendo yetu. Mathayo 5:3 inasema heri yao wapatanishi..Nawashauri familia iendeleze pale alipoacha Dk. Mengi ili kazi zake ziendelee kuishi," alisema.

**UPINZANI**

Akisoma salamu za Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni kwa niaba ya kiongozi wa kambi hiyo, Freeman Mbowe, Mbunge wa Ubungo, Saed Kubenea, alisema hana maneno ya kutosha kufikisha ujumbe wake kwa niaba ya wana Hai, lakini alimshukuru Mungu kwa maisha aliyompatia duniani na kuwa baraka kwa wengi aliowajua na asiowajua.

**RC MAKONDA**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alisema wamempoteza baba, rafiki, mwajiri ambaye alikuwa mkombozi kwa watu wengi na aliwaomba radhi wananchi kwa kufunga barabara juzi ili kutoa heshima kwa Dk. Mengi kwa mema aliyoyafanya nchini.

Alisema anamtambua Dk. Mengi kama mwamba wa kaskazini, sikio kwa waliokata tamaa na ambaye alikuwa tayari kuwa mfano kwa wanyonge na maskini na amepigana vita vizuri.

"Mchaga anakubali kumpa mali mtu hata asiyekuwa na ndoto, matumaini siyo jambo rahisi, kwa hili nazidi kusema siyo tu tumepoteza mchaga bora katika wachaga wote, bali tumepoteza Mtanzania aliyekuwa zaidi ya kabila lake," alisema Makonda. Alisema mwaka jana Dk. Mengi alimwambia aandae tukio kwa ajili ya chakula na viongozi wa dini na kutokana na serikali kutokuwa na bajeti ya tukio hilo ilimbidi akope fedha sehemu mbalimbali ikiwamo Sh. milioni 50 kwa rafiki wa mke wake na baadaye Dk. Mengi alilipa deni lote la Sh. milioni 147.

"Nilipata tabu nikaanza mandalizi na kamati niliyounda ilinihoji fedha tutatoa wapi, lakini nami nikawaambia waendelee na maandalizi na ilinibidi nikope kwa rafiki wa mke wangu Sh. milioni 50 kwa ajili ya malipo ya awali, baada ya shughuli kuisha Dk. Mengi alirejea nchini nikamwambia nina deni akaniambia kwa sababu umesikia sauti ya Mungu fedha zipo, akalipa deni lote Sh. milioni 147," alisema.

**CLOUDS MEDIA GROUP**

Mkurugenzi Mtendaji wa Clouds Media Group (CMG), Joseph Kusaga, alisema licha ya kwamba Dk. Mengi alikuwa anamiliki vyombo vya habari, lakini mara alipokutana naye alikuwa akimshauri namna ya kuviendesha.

Alisema Dk. Mengi amewaongoza katika tasnia ya habari kwa miaka 20 kwa kupigania haki ya uhuru wa vyombo vya habari.

"Binafsi nilimjua Dk. Mengi miaka 26 iliyopita nilikuwa nakwenda nyumbani kwake kupiga disco, akawa anazungumza mambo ya redio, yeye akaanza na mimi nikaendelea kupata mawazo. Mtu anachombo cha habari lakini anakupa mawazo ya kufungua chombo cha habari," alisema.

Kusaga alirudia maneno ya Dk. Mengi ambayo aliyasema wakati wa msiba wa Ruge Mtahaba kuwa, "Ruge hajafa' na kueleza kuwa, "Dk. Mengi hajafa".

**SALAMU ZA CTI**

Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), Subash Patel, alisema wamempoteza mshauri mkubwa ambaye alikuwa mwenyekiti aliyetumikia kwa miaka minne CTI.

"Mchango wa Dk. Mengi kwenye jamii ulikuwa mkubwa, utajiri wake aliishi nao kwa msaada, elimu aliyotupa ya kuishi duniani ni kubwa kuliko fedha alizokuwa nazo, tulikuwa marafiki alikuwa mshauri wangu," alisema.

Patel aliwataka Watanzania wenye utajiri wamuige Dk. Mengi kwa kuwa na moyo wa kutoa na kusaidia wengine.

# Waziri Lukuvi asimamisha

INATOKA UK. 4

Katika hatua nyingine, Lukuvi amewateua wenyeviti 20 wa mabaraza la ardhi na nyumba ya wilaya kwa kipindi cha miaka mitatu.

Lukuvi alisema mamlaka aliyonayo yanampa nafasi ya kuwateua wenyeviti hao pale anapoona inafaa.

"Kwa Mamlaka niliyonayo kwa mujibu wa kifungu cha 25(1)cha Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216, nimewateua wenyeviti 20 wa mabaraza ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi ya wilaya kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Aprili Mosi, mwaka huu," Lukuvi alisema.

Aliwataja wateule hao kuwa ni Rajabu Mnyukwa, Edward Muhina, Nadhiru Ngukulike, Rebeca Mjanja, Hussein Lukeha, Augustine Lugome, Baraka Shuma, Tendai Chinolo, Mangeti Sangiwa, Jackson Kanyerinyeri, Jacob Kabisa, Ntumengwa Moses, Justine Lwezaura, Jesca Mugalu, Regularly Mtei, Jimson Mwankenja, Bahati Ndambo, Richard Mmbando, Felix Rutajangulwa na Ngasa Masunga.

# Bunge labaini uhaba mkubwa

INATOKA UK. 5

kubwa na inaweza kuathiri utendaji kazi wao. "Kamati inashauri Serikali suala hili kipekee na kulitafutia ufumbuzi wa haraka. Kwa Hospitali ya Mwananyamala ambayo haina nyumba hata moja ya watumishi, kamati inashauri serikali iharakishe ujenzi wa nyumba za watumishi," alisema.

Kamati hiyo pia iliishauri serikali kuongeza bajeti ya ununuzi wa dawa na kuhakikisha fedha zinatolewa kwa wakati.

**UPINZANI**

Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko (Chadema), akiwasilisha hotuba kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Afya, mbali na kuzungumzia uhaba wa watumishi, alikemea tabia ya wanasiasa kuwawajibisha madaktari pasipo kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa.

Matiko pia alisema Kambi ya Upinzani inazitaka mamlaka zenye dhamana ya kusimamia ulinzi wa watoto kuwajibika ipasavyo kwa kushindwa kuwalinda watoto chini ya Katiba ya Tanzania kutokana na matukio ya hivi karibuni ya watoto kukutwa wakiwa wameuawa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Upinzani pia uliitaka serikali kuchukua hatua kukabiliana na maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU) hasa kwa vijana, ukieleza kuwa takwimu zinaonyesha maambukizo kwa kundi hilo kwa sasa ni asilimia 46 na wengi wao ni walio katika umri wa kuhitimu shule ya msingi mpaka chuo kikuu.

# Mahakama yaamuru mali kutaifishwa

INATOKA UK. 4

Magoiga.

Alisema DPP aliwasilisha maombi akitaka kutaifisha mali hizo kuwa za serikali baada ya kubainika kuwa zimepatikana isivyo halali na kwamba ni fedha chafu.

Hata hivyo, walalamikiwa hawajawasilisha utetezi kuonyesha kwamba walikuwa na biashara nyingine zaidi ya upatu.

Jaji aliendelea kuichambua hukumu kwamba walalamikaji wameshindwa kujitetea kwamba fedha na mali zote hazihusiani na upatu uliotokana na makusanyo kutoka kwa wananchi bila kuwa na leseni ya kufanya hivyo.

Alisema lengo la DPP si kuitajirisha serikali bali ni kuwataka watu wafuate taratibu na sheria kuendesha shughuli zao.

Maombi hayo namba 42/2019 yalifunguliwa na DPP Biswalo Mganga dhidi ya wakurugenzi wa DECI.

Walalamikiwa waliwakilishwa na Wakili Majura Magafu.

Mapema mahakamani hapo Magafu akijibu hoja za mlalamikaji, alidai kuwa akaunti zilizowasilishwa na DPP, kati ya hizo moja inamilikiwa na kanisa na ya pili inamilikiwa na mlalamikiwa wa kwanza.

Hata hivyo, hati ya kiapo iliyowasilishwa na DPP hakuna mahali inaonyesha ushahidi kwamba mali zote zimetokana na fedha za ujanjaujanja.

Jopo la mlalamikaji liliongozwa na DPP Biswalo Mganga akisaidiana na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, Mawakili wa Serikali Waandamizi, Theophil Mutakyawa na Shadrack Kimaro.

Akijibu hoja za walalamikiwa, DPP alidai kuwa walalamikaji walikuwa wanaendesha mchezo wa upatu kinyume cha sheria na kwamba mali zote ni mali ya DECI zinafaa kutaifishwa.

Alidai kuwa fedha na mali hizo zimethibitika kuwa zilitokana na upatu na ndiyo maana Mahakama ya Rufani katika hukumu yake ilimuelekeza kufungua maombi hayo Mahakama Kuu.

Alidai kwamba, DECI haikuwa na shughuli nyingine yoyote mbali ya kukusanya fedha na kwamba wajibu maombi hawakuleta ushahidi wa kulingana na hilo hivyo biashara haramu ya upatu ndiyo ilikuwa kazi yao.

Kuhusu uhusiano wa mali za kanisa na DECI, DPP Mganga alidai kuwa fedha zilizokuwa katika akaunti ya kanisa zilikuwa za DECI kwasababu wakàti huo hawakuwa na akaunti kwa kuwa walikuwa bado hawajakamilisha usajili.

"Wakili anasema DECI ilikuwa inafanya biashara nyingine, lakini hawakuonyesha biashara hizo zilizowafanya wapate fedha na mali hizo, katika kiapo chao hakuna ushahidi, ushahidi pekee upo katika kiapo chetu," alidai DPP.

Katika maombi ya msingi, DPP Mganga aliwasilisha maombi hayo mahakamani, akiiomba itoe amri ya kutaifishwa kwa mali za kampuni hiyo yakiwamo magari 11, nyumba na viwanja vinane na fedha ziwe mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika maombi hayo, DPP anaiomba mahakama hiyo kutoa amri ya kutaifishwa kwa kuwa mali ya serikali, nyumba namba UKMMD/1237 iliyoko Mwembe Madafu, Ukonga, Dar es Salaam, kiwanja namba 651, kitalu 'M' kilichopo Forest area, Mbeya, nyumba iliyoko kiwanja namba 7, kitalu 'P' ikiwa na hati namba 033004/23 kilichopo mtaa wa Rufiji, Manispaa ya Mwanza.

HABARI KITAIFA

# RC aagiza DED awekwe ndani saa 24

Na Ibrahim Yassin, MBOZI

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali mstaafu Nicodemus Mwangela, ameagiza polisi wamshikilie kwa saa 24, Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo, Seriadi Mbugi, kutokana na kurundika takataka jirani na makazi ya wananchi.

Mrundikano huo wa taka ngumu pamoja na mizoga ya wanyama, vimekuwa vikitupwa kwenye maeneo hayo na kuhatarisha maisha ya watu, wanafunzi pamoja na kuharibu mazingira hatua ambayo imesababisha wananchi watoe kero zao kwa Mkuu wa Mkoa baada ya ngazi ya wilaya kushindwa kusikiliza kero zao.

Brigedia Mwangela alifikia uamuzi huo mapema jana wakati akifanya ukaguzi wa hali ya usafi katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlowo na kukuta takataka zimemwagwa katikati ya makazi ya wananchi ikiwa ni siku saba tangu amwelekeze Kaimu Mkurugenzi huyo kuhakikisha mji huo unakuwa msafi.

"Nilifanya mkutano na wananchi wa mji wa Mlowo na malalamiko yao makubwa yalikuwa mrundikano wa takataka na madampo katikati ya miji yao, nilimwagiza na kumpa siku saba Mkurugenzi kuhakikisha anausafisha mji huu, lakini leo siku saba zimepita ninakagua na kukuta hajatekeleza," alisema.

Alisema mkurugenzi huyo amekiuka agizo lake na hivyo kuhatarisha maisha ya wananchi hao kwa kuwawekea takakata katikati ya makazi yao kinyume na taratibu za kiafya zinavyoelekeza.

"Huu sio utendaji wa serikali kabisa, licha ya Kaimu DED kukaa ndani, namwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kuhakikisha ndani ya saa nne takataka hizo ziwe zimetolewa na dampo hilo lifutwe," alisisitiza.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akisalimiana na Ofisa Mauzo wa Benki ya Biashara ya DCB Tawi la Dodoma, Nuru Ashraf wakati Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Godfrey Ndalahwa (katikati), alipomtembelea Waziri Mkuu, ofisini kwake, bungeni, Dodoma juzi. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU.**

# SIDO yachagiza utekelezaji wa programu bidhaa moja wilaya moja

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), limesema mwitikio wa mikoa katika kutekelezaji Programu ya wilaya moja bidhaa moja (ODOP) utachochea uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na mazao ya kilimo na mifugo hapa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mpango huo jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Prof.Sylvester Mpanduji, alisema utekelezaji wake umeanza kwa mafanikio baadhi ya mikoa.

"Programu hii imechochea mazao ya kilimo na mifugo kuongeaza uzalishaji wa bidhaa kupitia viwanda vilivyopo katika wilaya husika na huchagiza maendeleo katika ngazi ya wilaya na hatimaye taifa kwa ujumla," alisema Prof. Mpanduji. Alisema kuwapo kwa ODOP kumeamsha hali kwa wananchi kujikita katika uzalishaji zaidi hali inayochochea ukuaji wa uchumi na kufanikisha azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025 kwa vitendo.

"ODOP imeweza kutekelezeka katika mikoa mbalimbali ikiwemo Singida, Mbeya, Dodoma, Manyara na Morogoro katika kuzalisha bidhaa zinazotokana na mazao ya kilimo na mifugo kama vile alizeti, mahindi, Mpunga na mazao ya mbogamboga," alisema.

Alisema jukumu la SIDO katika program ya ODOP ni kuhakikisha viwanda vinajengwa katika kila wilaya kwa lengo la kuzalisha bidhaa moja itakayochaguliwa na wilaya husika ambapo uhamasishaji utafanywa katika uzalishaji wa mazao ili yatumike kama malighafi ya kiwanda na kuzalisha bidhaa. "Programu hii itachochea ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo ya haraka katika wilaya husika ka kupitia mapato yatakayopatika kutoka katika viwanda vyao hali itakayochochea miundombinu na mahitaji muhimu kupatikana kwa wakati," alisema Prof. Mpanduji.

Prof.Mpanduji aliwataka Watanzania kutumia programu hii kwa kuwa mafanikio yake ni makubwa katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla kama kutakuwa na utayari katika kufanya kazi kwa pamoja.

"SIDO inaendelea kusimamia programu hii na jukumu lake kubwa ni kuhakikisha viwanda vinaanzishwa na kukua kutoka viwanda vidogo na hatimaye kufikia viwanda vikubwa vinavyoweza kujiendesha na kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi," alisema Prof.Mpanduji. Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Uwekezaji wa

SIDO, Shoma Kibende, alisema ODOP imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na mwitikio wa kila wilaya katika programu hii ambayo imekuwa mkombozi wa mazao ya wakulima.

"Wakulima wamekuwa na uhakika wa soko la mazao yao kutokana na uwapo wa viwanda vinavyochakata mazao katika kila wilaya, wanachagua zaomoja kuwa la biashara na uzalishaji wa uhakika unaanza," alisema Kibende.

# Watoa msaada wa kisheria washauriwa

Restuta Damian, BUKOBA

MASHIRIKA yanayotoa msaada wa kisheria kwa kushirikiana na wasaidizi wa kisheria, Jeshi la Polisi, Magereza na Mahakama yametakiwa kuhakikisha msaada wa kisheria namba 1 ya mwaka 2017 unatekelezwa kwa ufanisi katika jamii.

Hayo yalisemwa na Msajili wa watoa huduma ya msaada wa kisheria nchini, Felisia Joseph, wakati akizungumza na wadau wa kisheria mkoani Kagera waliojumuika na mikoa ya Geita na Tabora kwa lengo la kujadili kuamua namna ya kusaidia mwananchi.

Joseph alisema sheria hiyo imelenga kusaidia jamii kutambua sehemu gani ya kupata msaada wa huduma ya kisheria juu ya changamoto inayohitaji utatuzi wa haki na utetezi.

Aidha alisema kuwapo kwa sheria hiyo mpya, ambapo awali ilikuwa na tarabu ambazo zinafanywa na watoa huduma zenye kumfanya mwananchi kushindwa kujua sehemu sahihi ya kupatia huduma ya kisheria.

"Kwenye Taasisi au watoa huduma ambao hawajasajiliwa na kutambuliwa ilisababisha mwananchi kushindwa kumudu gharama kwa kuwa wengi hawakuwa rasmi na hawakufuata tararibu zenye kuisaidia jami, hivyo kusababisha mtu kukosa haki,"alisema Joseph.

Wakili wa kujitegemea kutoka Taasisi inayotoa msaada wa kisheria (MHOLA), Telesia Bujiku, alisema sheria hiyo imetambuliwa tangu mwaka 2017, na inaendelea kusaidia kuweka miongozo zaidi ya utoaji huduma.

Alisema sheria hiyo imeweza kutofautisha majukumu ya wajumbe wa Baraza la Mahakama, Mahakama na kuondoa migongano iliyokuwapo na kutambuka kazi zao pia.

"Hii sheria imesaidia kuondoa migongano na mivutano kwa watu wa misaada ya kisheria kwenye mabaraza ya mahakama, inasaidia zenyewe na kila sekta kujua kaziyake kwa jamii na kumpa mwanga asiyejiweza kwa gharama kuendesha kesi yake," alisema Bujiku.

Afisa Maendeleo ya Jamii mkoa wa Kagera, Issa Mlimi, alisema katika kesi zinazofika kwenye ofisi ya mkoa kwa mwezi ni zaidi ya 55 ikiwa 10 hadi 15 zinapelekwa mahakamani.

# Watumishi 8,400 waajiriwa s/mitaa

BUNGE limeelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19, serikali imeajiri jumla ya watumishi 8,444 wa kada mbalimbali za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hayo yalielezwa jana Bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Josephat Kandege, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Zubeda Sakuru.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema hospitali na vituo vya afya hutakiwa kukidhi vigezo vya utoaji huduma kwa wagonjwa.

"Lakini hospitali nyingi na vituo vya afya vingi havina viwango vya utoaji huduma. Je, Serikali ina mkakati gani mahusus wa kuhakikisha vituo vya afya na hospitali vina kidhi viwango vya utoaji huduma?" alihoji.

Akijibu, Kandege alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya afya, kuajiri wataalam, kununua dawa, vitendanishi na vifaa tiba ili kuhakikisha vituo vya kutolea huduma vinakidhi viwango vinavyohitajika.

Aidha, alisema ili kuboresha viwango vya utoaji huduma za afya nchini katika mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19 serikali imetoa kiasi cha Sh. bilioni 285.17 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 67 za Halmashauri.

"Pia ujenzi na ukarabati wa Hospitali 9 za wilaya, vituo vya afya 304 na zahanati 39.Vile vile serikali imejenga na kukarabati nyumba 301 za watumishi wa afya nchini," alisema.

Kadhalika, alisema kwa mwaka wa fedha 2019/20 serikali imetenga Sh. bilioni 23.9 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya 27 za wilaya na ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya 52.



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dk. Kebwe Steven Kebwe (aliyesimama), akitoa hotuba yake ya ufunguzi wa mafunzo ya siku tano kwa madaktari na watoa huduma za afya kuhusu namna ya kufanya tathmini ya magonjwa na ajali zitokanazo na kazi. Mafunzo hayo yaliypowaleta pamoja zaidi ya madaktari 100 kutoka mikoa mitano yaliyoanza juzi mjini Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yafafanua watoto magerezani kwenda shule

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema hakuna watoto wanaokwenda shule wakiwa magerezani isipokuwa kuna watoto walio chini ya miaka miwili wanaolazimika kubaki gerezani na mama zao ili kupata haki yao ya kunyonya.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Faustine Ndugulile, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi.

Kisangi alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kusaidia watoto ambao wanaishi gerezani na huenda shule na kurudi gerezani kulala na mama zao.

"Hali hiyo sio nzuri kwa makazi ya mtoto hasa kwa mambo wanayoyaona na kusikia wakiwa gerezani.Je, serikali ina mpango gani wa kusaidia watoto hao waondokane na hali hiyo?" alihoji.

Akijibu, Dk. Ndugulile alisema watoto kuwapo magerezani inatokana na mama zao kuhukumiwa kutumikia adhabu ya kifungo wakiwa katika hali ya ujauzito au kuwa na mtoto aliye chini ya umri wa miaka miwili, ambaye anapaswa kupata haki ya kunyonya maziwa ya mama.

Alifafanua kuwa yapo mazingira yakiwemo kukosekana kwa malezi mbadala kwa watoto zaidi ya miaka miwili na isiyozidi miaka 5 kubaki na mama zao gerezani, hivyo kulazimika kuhudhuria katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana.

"Madhumuni ya kupatiwa huduma ya malezi changamshi ya awali ili kuchochea ukuaji na maendeleo yao kiakili, kimwili, kihisia, kijamii na kimaadili," alisema.

Alibainisha mwaka 2015 kulikuwa na watoto 150, 2016 watoto 85, 2017 watoto 108 na kwamba watoto hao ni kwa mgawanyiko wa wakina mama mahabusu na wafungwa katika magereza.

Kadhalika, alisema serikali kupitia Sheria ya Mtoto namba 21, ya mwaka 2009 kifungu cha 144, Kanuni za Ulinzi na Usalama wa Mtoto za mwaka 2015 na Sera na taratibu za ulinzi wa mtoto katika magereza ya mwaka 2018.


"Imeweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa mtoto anapata malezi yanayohitajika ikiwemo mlo kamili, virutubisho, huduma za afya pamoja na chanjo," alisema.

Aidha, alisema utaratibu wa watoto chini ya miaka 5 kuhudhuria kwenye vituo vya kulelea watoto wadogo mchana unalenga kupunguza muda wa watoto kukaa gerezani na kutumia muda wa zaidi ya saa sita katika vituo hivyo.

"Chini ya Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 serikali imeanzisha programu ya malezi mbadala kama vile walezi wa kuaminika, malezi ya kambo na kuasili," alisema.

Dk. Ndugulile alisema watoto walio na mama zao gerezani ambao wamekosa malezi mbadala wanapata fursa ya kupokelewa katika makao ya watoto kwa muda wakati jitihada nyingine zikiendelea.

"Programu hizo zinahakikisha watoto wa zaidi ya miaka 5 wanaondolewa gerezani na kuunganishwa na watoa huduma za malezi mbadala," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## Sababu vitambi kuongezeka hizi

SERIKALI imesema asilimia 10 ya Watanzania wana lishe iliyopitiliza ambapo kinamama na kinababa wana vitambi.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainab Mwamwindi, ambaye alisema udumavu na utapiamlo mkali ni tatizo kubwa kwa watoto wengi nchini.

"Je, Serikali ina mpango gani unaotekelezeka kwa kukabiliana na hali hiyo ikiwemo kuzijengea uwezo kamati za lishe na kata?" alihoji.

Alisema kuna changamoto ya Watanzania kula bora chakula kuliko chakula bora hali ambayo imesababisha kuwa na lishe iliyopitiliza.

"Serikali tumeliona hilo na ndio maana tulizindua mpango mkakati wa masuala ya lishe na unaratibiwa Ofisi ya Waziri Mkuu, hivyo tunalenga kupunguza udumavu wa watoto na kupambana na lishe iliyopitiliza," alisema.

Pia alisema ipo katika mchakato wa kuajiri kada ya wahudumu wa Afya ngazi ya jamii angalau wawili kwa kila kijiji ambao pamoja na shughuli nyingine watatoa huduma za lishe katika ngazi ya kaya.

Alisema kuwa serikali ilianzisha muundo wa kada ya maafisa lishe chini ya wizara ya Afya mwaka 2012 na jumla ya maafisa lishe 114 wameajiriwa katika mikoa na halmashauri na serikali, lakini kwa sasa Wizara hiyo na Ofisi ya Rais, Tamisemi ipo katika mchakato wa kuajiri kada ya wahudumu wawili kila kijiji.

Alifafanua kuwa serikali imeazimia kutekeleza malengo ya Baraza la Afya Duniani la kutokomeza utapiamlo ifikapo 2025 pamoja na kutekeleza maazimio mbalimbali ya kupunguza utapiamlo kimataifa, kikanda na afrika mashariki.

Alisema kitaifa serikali kupitia sera ya taifa ya afya ya mwaka 2007 ambayo kwa sasa inapitiwa imeelezwa wazi kuwa itaboresha huduma za lishe kwa wananchi wake.

"Kwa miaka ya karibu serikali imeongeza juhudi katika kupambana na tatizo la utapiamlo nchini kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi ambapo juhudi hizo ni pamoja na kuandaa na kutekeleza mpango mkakati jumuishi wa kimataifa wa utekelezaji wa afua za lishe ya mwaka 2016/17 hadi 2021/22 ambao una vipengele vilivyolenga kupunguza utapiamlo ifikapo 2021," alisema.

Alitaja vipengele hivyo kuwa ni pamoja na kupunguza viwango vya udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka asilimia 34 ya mwaka 2015 hadi 28.

"Nyingine ni kudhibiti viwango vya ukondefu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kufanya viendelee kubaki chini ya asilimia 5 iliyopo kwa sasa," alisema.

Kadhalika, alisema kupunguza viwango vya watoto wanaozaliwa na uzito pungufu kutoka asilimia 7 ya mwaka 2015 hadi kufikia chini ya asilimia tano na kupunguza udadi ya wanawake walio katika umri wa uzazi miaka 15 hadi 49 wenye upungufu wa damu kutoka asilimia 44.7 ya mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 33.

Vilevile, alisema kupunguza tatizo la upungufu wa vitamini A kwa watoto wenye umri miezi 6 hadi 59 kutoka asilimia 33 ya mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 26.

# Wachimbaji wa madini wamlilia marehemu Dk. Reginald Mengi

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WACHIMBAJI wa madini ya Tanzanite, Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wameelezea kusikitishwa na kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, marehemu Dk. Reginald Mengi ambaye pia alikuwa mwekezaji katika machimbo ya Tanzanite, kupitia kampuni ya Tanzanite Africa Ltd.

Wachimbaji hao wakizungumza jana na Nipashe wilayani humo, walisema kuwa wanamshukuru Mungu kwa kuwapatia Mzee Mengi, ambaye watamkumbuka kwa mchango wake kwenye sekta ya madini.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema), tawi la Mirerani, Shwaibu Mushi, alitoa pole kwa wadau wote wa madini,kwa kuondokewa na mmoja kati ya wamiliki wa sekta hiyo.

Mushi alisema wachimbaji wa madini wamempoteza mtu muhimu na mlezi wao, kwa kuwa alimchukulia marehemu Mengi kama mzazi wao. Mmoja kati ya wamiliki wa mgodi wa madini ya Tanzanite, Fatuma Kikuyu, alisema marehemu Mengi, atakumbukwa kwa mengi ikiwamo kuwajali wanyonge wakiwamo wenye ulemavu na wenye ualbino. "Apumzike kwa amani Mungu atamlipa kwa mema aliyotenda, ni mfano wa kuigwa kwa wenye uwezo muhimu kufahamu kwao dunia hii ya kupita sio nyumbani," alisema Malhassan. Mmoja kati ya wakazi wa mji mdogo wa Mirerani, Mohamed Issa, alisema mzee Mengi alikuwa anasaidia watu wa makundi mbalimbali bila kubagua madhehebu na alikuwa anatoa msaada pindi akiombwa.

"Hata sisi tulishasaidiwa mambo mbalimbali na marehemu mzee Mengi ambaye alituwezesha kupitia Meneja wa kampuni ya uchimbaji madini ya Tanzanite Africa, Wilfred Mushi, ambaye alimwakilisha," alisema Issa. Mkazi wa Kijiji cha Naisinyai, Simon Laizer, alisema unapomzungumzia marehemu Mengi unakuwa unataja yatima, wenye ulemavu, wajane na watu wenye uhitaji mbalimbali.

"Hapa Naisinyai tuliwahi kumuomba aje kwenye harambee yetu na alifika na kutuchangangia fedha za maendeleo, huku akituahidi kutusaidia siku yoyote ile ambayo tungekuwa tunahitaji na akatimiza hayo," alisema Laizer.



Balozi wa Ujerumani nchini, Dk. Detlef Waechter, akimkabidhi funguo za Hospitali ya Kanda ya Jeshi Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, hospitali iliyojegwa katika eneo la jeshi lililopo wilayani Monduli mkoani Arusha. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Watoto 83,000 wapatiwa kinga ya minyoo, kichocho

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WATOTO 83,000 wenye umri kati ya miaka mitano hadi 14, katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, wamepatiwa dawa ya kuwakinga ugonjwa wa kichocho na minyoo, kwa ajili ya kuwanusuru watoto

na magonjwa ambayo hayapewi kipaumbele.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Mganga Mkuu wa halmashauri hiyo, Dk. Peter Mboya, alisema utoaji na ugawaji dawa wa kinga hiyo umefanyika katika maeneo mbalimbali ya halmashauri hiyo.

Alisema waliweka vituo 139 vya ugawaji wa dawa hizo na wazazi wa watoto kwa kushirikiana na jamii kwa ujumla, walihamasishana hadi ugawaji ulipomalizika.

Aidha, alisema ugawaji huo ni wa kitaifa na serikali inatoa kinga ya tiba hiyo bure kutokana na kuwapo kwa ongezeko la tatizo kubwa kwa magonjwa ya minyoo na kichocho kwa watoto wadogo.

Alisema magonjwa hayo yameleta madhara kwa watoto kupata upungufu wa damu, pamoja na utumbo kutoboka na hatimaye kupoteza maisha.

"Ugonjwa wa kichocho ni tatizo kubwa kwa watoto na usipopatiwa tiba halisi kwa haraka, husababisha madhara na wakati mwingine husababisha kifo hivyo, ni vema wazazi kuchukua tahadhari kwa kuwapa watoto dawa

hizo," alisema Mboya.

Hata hivyo, Mboya, aliwataka walezi na wazazi kuhakikisha watoto wao, wanapatiwa kinga ya tiba hiyo kwa kuwa ni muhimu kwa afya za watoto.

"Wazazi na walezi wa watoto hakikisheni mnawapeleka watoto kupata kinga hii, kwa kuwa ni muhimu kwa afya zao, lakini msipowapeleka madhara

hayawezi kujitokeza mapema," alisema Mboya.

# Ujerumani yajenga hospitali ya kisasa JWTZ Monduli

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SERIKALI ya Ujerumani kupitia Balozi wake nchini Tanzania Dk. Detlef Waechter, imekabidhi funguo za hospitali ya Kanda ya Jeshi iliyopo katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli wilayani humo, iliyogharimu Sh. bilioni 5.6.

Akikabidhi funguo hizo kama ishara ya ufunguzi na makabidhiano, kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Balozi, Dk. Waechter alisema

hospitali hiyo ni moja ya mkataba kati ya Wizara ya Ulinzi nchini Ujerumani na wizara hiyo nchini Tanzania, kupitia sekta ya afya.

"Mradi huu ulianza mwaka 2017 na ulitakiwa kuisha mwaka 2020, lakini tumeongeza muda wa mradi hadi 2024, ili kuendelea kusaidia Serikali ya

Tanzania, kupitia Wizara ya Ulinzi na tunaahidi kuendelea kufadhili miradi ya serikali ya Tanzania," alisema balozi huyo.

Kwa upande wake Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dk. Hussein Mwinyi, aliiomba Serikali ya Ujerumani kuendelea kutoa msaada kwa kuwa hospitali za Kanda, hazihudumii wanajeshi pekee, bali zinasaidia wananchi kwa asilimia 80, huku wanajeshi asilimia 20.

"Wenzetu wa Ujerumani wametusaidia sana, walitusaidia katika ujenzi wa chuo cha wataalam wa tiba, vifaa na maabara na niwashukuru kwa kuongeza

muda wa mradi huu," alisema na kuongeza:

"Lakini Hospitali hii ina vifaa bora na vya kisasa pengine kuliko hata hospitali nyingine na itasaidia kupunguza idadi ya wagonjwa waliokuwa

wakienda nje kutibiwa," alisema Waziri Mwinyi.

Naye Mkuu wa Majeshi nchini, Brigedia Jenerali Venance Mabeyo alisema, hadi kukamilika kwa ujenzi wa hospitali hiyo kumegharimu Sh. Bilioni 5.6, kati ya hizo Sh. bilioni 2.8 zilitumika kwaajili ya vifaa tiba na Sh. bilioni 2.8 kwaajili ya miundombinu kwa ufadhili wa Serikali ya Ujerumani.

"Walijenga Chuo cha Tiba Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na hapa na zote ni za viwango vya juu, tunawashukuru sana wenzetu hawa," alisema

Brigedia Mabeyo.

Kwa upande wake Mkuu wa Tawi la Tiba wa Jeshi la Wananchi Tanzania, Meja Jenerali Denis Janga, alisema matibabu yataanza mapema, kutakuwa na wataalam wa idara zote ikiwamo meno, uzazi na picha (x-ray),

huku ikilaza wagonjwa 50 kwa siku na kuhudumia 300 kwa siku.







Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akipeana mkono na mdau wa maendeleo, Peter Toima (kushoto), aliyenunua matairi manne kwa ajili ya gari la polisi la mkoa huo Mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanachama wamkataa mwenyekiti

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WANACHAMA wa chama cha msingi Muruwia kilichopo kata ya Uru Mashariki, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wamesusia mkutano wa makisio wa mwaka 2018/2019 kwa kile walichodai hawamtaki mwenyekiti aliyepo kwa kuwa walishachagua mwenyekiti mwingine ambaye hawajui alipo.

Wanachama hao waliopiga kelele wakimkataa mwenyekiti wa zamani,

Matius Akaro, waliiambia Nipashe kuwa hawatakubali kufungua kikao hadi wapewe maelezo ya kina kuhusu mwenyekiti waliyemchagua, Philipo Sabas, kuwapo kwenye meza ya uongozi.

Liberatus Temba, alisema hawapo tayari kufanya kikao cha makisio ya mwaka 2018/2019 mpaka watakapoelezwa nini kilitokea, kwa nini mwenyekiti waliyemchagua kwa takribani mwaka mmoja haonekani katika meza ya uongozi.

"Zipo tetesi kuwa bodi ilikaa na kudai kuwa mwenyekiti huyo ni mwizi wa kahawa stoo ya wanachama kilo 24 zenye thamani ya Sh. 84,000 ... na

kumsimamisha bila kutupa taarifa kwa takribani mwaka sasa...sisi ndio waamuzi, kwa nini hawajatuletea taarifa hadi leo...?" Alihoji Alfred Ngowi.

Zakaria Njau, aliiomba serikali kuhakikisha inawatazama wao kama vyama vya ushirika kwa kutoa elimu na kuweka ukomo wa uongozi ili kuepusha

migogoro na uchu wa madaraka.

"Haituingii, akilini kuona kuwa bodi imekaa na kusema kuwa kuna wizi umetokea stoo na kahawa hiyo ikaja kuuzwa hapo na ikawalazimu mwenyekiti (Philipo Sabas) tuliyemchagua kusimamishwa kazi wakati huo huo walinzi wakiwa kazini ikiwa ni wizi

ulitokea ni lazima wote walishiriki," alihoji.

Kwa upande wake mshika funguo wa stoo (Kisusa), Patrick Kasimi, alisema hajaona kasoro yoyote katika stoo yake licha ya kusikia tuhuma hizo

zinazomlenga mwenyekiti aliyechaguliwa.

Alisema binafsi anaona kama ni chuki binafsi zilizopo baina ya pande zote mbili na kuzitaka mamlaka husika kufuatilia kwa ukaribu ili kutoa haki iliyosawa.

Akijibu tuhuma hizo, Akaro alisema kuwa alibaini kuwa

mwenyekiti aliyechaguliwa ni mwizi hivyo hakuona umuhimu wa kumkabidhi madaraka na akachukua jukumu kuita bodi ndipo walipokubaliana kumsimamisha.

Naye mwenyekiti aliyechaguliwa, Sabas, alikiri kusimamishwa uongozi bila sababu ya yoyote huku akituhumiwa kushiriki wizi wa kahawa.

Aidha, Ofisa Ushirika na mlezi wa chama hicho, Godless Barinaba, alilazimika kuahirisha mkutano huo na kuwaahidi wanachama kushughulikia mgogoro huo mapema iwezekanavyo kabla ya kuleta makisio ya mwaka wa bajeti ya 2018/2019.

# Siha waomba mila za ukeketaji kutokomezwa

**Na Mary Mosha,** SIHA

WANANCHI wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wameiomba Serikali ya Awamu ya Tano, kuingalia kati mila na desturi zinazowakandamiza

wanawake na watoto hasa ukeketaji ili kupunguza madhara wakati wa kujifungua.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti baadhi ya kinamama hao walisema, matatizo ya ukeketaji kwa Wilaya ya Siha bado ni kitendawili kisichoteguka kutokana na wanajamii hao kuwakeketa watoto wadogo.

Evaline Moleli, kutoka Kata ya Karansi, alisema wapo baadhi ya wauguzi katika hospitali mkoani Kilimanjaro ambao wamekuwa wakipewa rushwa na kuwakeketa watoto wenye umri chini ya miaka mitatu.

Alisema hali hiyo inasababisha matatizo makubwa hasa wakati wa kijifungua ikiwamo uvujaji wa damu na hatimae wengine kupoteza

maisha.

Safina Mohamed alisema miongoni wa mila na desturi zinazomuathiri mwanamke katika baadhi yamakabila ni ukeketaji ambao umekuwa ukifanyika kwa njia za siri katika vituo vya afya na zahanati.

"Tunaomba serikali ya asasi na kiraia kuungana katika kuelimisha hasa jamii za wafugaji na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kufanya vitendo kama hivyo," alisema Safina.

Msele Emanuel, alisema bado elimu ni ndogo kwa wanajamii kuhusu masuala ya ukeketaji na madhara yake ili kuepukana na matatizo kwa

vizazi vijavyo.

Naye Mratibu wa Nafgem Tanzania, France Selasini, alikiri kuwapo kwa ukeketaji katika Wilaya Siha, hasa katika kata za Naibili, Karansi, Lekrumuni, Orkolili, Ngarinairobi na Donyomoro unaofanywa kwa siri kwa watoto ambao

hawawezi kujieleza.

"Katika Wilaya ya Siha tatizo hili bado ni kubwa ambalo serikali inapaswa kuliangalia kwa umakini katika kuhakikisha wanaweka sheria kali zitakazowabana wahusika watakaobainika kuingia kwenye makosa mbalimbali yakiwamo ya ukatili kwa kinamama na watoto," alisema na kuongeza:Tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha mpango maalumu

wa kuielimisha jamii kuhusu ukeketaji na kuanzisha mpango maalumu wa kutoa elimu kila mara ili kuhakikisha wa-

# Tanroads kufunga kamera vituo vya mizani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKALA wa Barabara nchini (Tanroads), Mkoa wa Kilimanjaro, inakusudia kufunga kamera katika vituo vya kupimia uzito wa magari (mizani) ili kufuatilia shughuli mbalimbali za utendaji kazi na kudhibiti mienendo ya vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya wafanyakazi wasiokuwa waaminifu.

Meneja wa Tanroads mkoani Kilimanjaro, Ntije Nkolate, aliyasema hayo jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kuongeza kuwa, hivi sasa wapo katika hatua za maandalizi ya mwisho kwaajili ya ufungaji wa kamera hizo.

Alisema mkongo wa mawasiliano ya taifa tayari umeshafika karibu na vituo vya kupimia uzito wa magari na kwamba wapo kwenye maandalizi ya kuandaa chumba maalumu kitakachofungwa mitambo hiyo ili kurahisisha shughuli za ufuatiliaji wa kazi mbalimbali katika mizani hizo.

Alisema kufungwa kwa kamera hizo katika vituo vya kupimia uzito wa magari kutawaondolea usumbufu wa kufuatilia utendaji kazi katika mizani hizo kwa kutumia muda mwingi na gharama kubwa, pamoja na kurekodi shughuli zote zinazofanyika.

Hatua ya kufunga kamera na mitambo mingine katika mizani za kupimia uzito wa magari ilitolewa na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi ambaye kwa sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. John Magufuli, ili kuwadhibiti baadhi ya wafanyakazi wasiokuwa waaminifu katika mizani hizo ambao walikuwa wakituhumiwa kuhusika na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa.

"Hii itatuondoa na kutuepusha suala la kwenda kwenye mizani kukagua utendaji kazi wa wa watumishi na masuala mbalimbali kila mara baada ya nusu saa, lakini kwa kiasi kikubwa itatusaidia kurahisisha utendaji kazi wetu kwa kuwa kwa sasa tutaweza kukaa ofisini na kufuatilia mwenendo mzima wa utendaji kazi katika mizani huku tukiendelea na shughuli nyingine," alisema.

Katika Hatua nyingine, Ntije alisema kwa sasa wanatarajia kuanzisha mizani ya kuhamishika (mizani mkeka) ili kudhibiti magari yaliyozidisha uzito wa mizigo na kupita katika barabara ambazo hazina mizani.

Aidha, alisema katika Mkoa wa Kilimanjaro, zipo mizani mbili katika njia panda ya Himo, hivyo mizani ya kuhamishika itatumika katika barabara zisizokuwa nazo ikiwamo barabara ya Bomang'ombe, Sanyajuu hadi Kamwanga ambazo zimekuwa zikipitisha magari mengi ya mizigo ikiwamo mazao.

"Kumekuwapo na magari ambayo yamekuwa yakizidisha uzito kisheria na kupita katika barabara zisizokuwa na mizani, hivyo tunaamini kuanza kwa operesheni kwa kutumia mizani hii inayohamishika, kutasaidia kuzinusuru barabara zetu zisiharibike haraka," alisema.



Ukurasa 19

**Mvutano ndani ya chama tawala Kenya, Jubilee waongezeka?**

Spika Marekani amshukia Mwanasheria Mkuu, bado amgwaya Rais Trump



Ukurasa 20



**Korea Kaskazini yatunisha misuli yake, yafyatua makombora masafa mafupi**


Ukurasa 18


# siasa

JUMATANO MEI 8, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 15

**Demokrasia Venezuela hatarini pande mbili zikiwania jeshi liwaunge mkono**

# Dk. Bashiru: Urais umeipasua Zanzibar katika vipande vinne

• Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini na Pemba • Kurejea kufundisha chuo kikuu baada ya ukatibu mkuu

**Na Mashaka Mgeta,** Dodoma

VUGUVUGU la Uchaguzi Mkuu wa 2020 linaendelea kufukuta kwa wanachama wa vyama tofauti kujipanga ili kuwania na hatimaye kutwaa nafasi za uongozi.

Nafasi zitakazowaniwa katika uchaguzi huo ni zile za ubunge, ujumbe wa baraza la wawakilishi Zanzibar, urais wa Zanzibar na urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, purukushani kubwa zinatarajiwa katika kuwania nafasi ya urais hasa ya Zanzibar ambapo Rais wa sasa, Dk. Ali Mohamed Shein atakuwa anamaliza kipindi cha miaka 10 ya utawala wake.

Ingawa ni hivyo, kwa upande wa urais wa Jamhuri ya Mungano hakuna matumaini ya kujitokeza mgombea atakayeshindana na Rais John Magufuli ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, anaiangazia hali ilivyo ndani ya chama hicho kuelekea Uchaguzi Mkuu huo na ule wa serikali za mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu.

Anasema wapo wanachama wa CCM walioanza harakati za kusaka urais, wengine wakitumia fedha na kuunda mitandao yao.

Hata hivyo, anabainisha kwamba watu wenye hulka hiyo hawawezi kuteuliwa, kwani watachujwa.

"Lakini hata watakaoshinda katika kura za maoni, hawatapaswa kushangilia, kwa maana kushinda kura za maoni si kigezo pekee cha

INAENDELEA UK.16



Rais wa Zanzibar, Ali Mohamed Shein. **PICHA: MTANDAO**

**Siku 100 DRC za Rais Tshisekedi madarakani, amefanikisha nini?** Ukurasa 19

# Wapigakura msiiangushe NEC, jitokezeni wengi kujiandikisha



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), imewahi kukaririwa na vyombo vya habari ikisema imejifunza mengi kutoka katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, ambapo asilimia 32 ya Watanzania waliojiandikisha kupiga kura na kuwa na sifa ya kupigakura hawakufanya hivyo.

Kutokana na hali hiyo, ikaamua kuanza utaratibu wa kuzunguka katika taasisi mbalimbali, zikiwamo shule, taasisi za dini na pia kwenye shughuli zinazokutanisha watu wengi kama Mbio za Mwenge wa Uhuru.

Maeneo mengine ni katika vyombo vya habari lengo likiwa ni kuhakikisha inatoa elimu ya mpigakura kuhusiana na umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi, pamoja na kutambua majukumu ya tume hiyo.

Aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi wa tume hiyo Kailima Ramadhan ndiye aliyekaririwa na vyombo vya habari akisema hayo wakati akizungumzia kufanya maboresho ya daftari la wapigakura kwa awamu mbili kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Kwamba katika awamu ya kwanza daftari hilo lingeboreshwa katika mwaka wa fedha 2017/18, na kwa mara ya pili zoezi hilo litafanyika katika mwaka wa fedha 2019/20.

"Asilimia 32 ya wananchi waliokuwa na sifa za kupiga kura hawakufanya hivyo, ndiyo maana Tume ya Uchaguzi imeamua kuanza zoezi la kuelimisha wananchi katika maeneo mbalimbali kuhusu umuhimu wa kushiriki zoezi hilo." Kailima alikaririwa akisema.

> Nec imeanza uandikishaji kwa ajili ya kuvifanyia majaribio vifaa na mfumo wa uandikishaji wapigakura ili kubaini changamoto kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi hilo.

**UBORESHAJI WA DAFTARI**

Hapa kuna mambo mawili muhimu ambayo ninaamini yanaweza kusaidia wapigakura waliopo na wapya kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Jambo la kwanza ni kuharakisha uandikishaji wa wapigakura wapya na kuukamilisha kabla ya Oktoba mwaka huu, huku elimu ya mpigakura ikiendelea kutolewa ili wahusika watambue haki ya kushiriki katika uchaguzi.

Nec kusema kwamba asilimia 32 ya Watanzania waliojiandikisha kupigakura na kuwa na sifa hawakufanya hivyo katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ni dalili tosha kuwa kuna tatizo la ukosefu wa elimu ya mpigakura.

Nec imeshafanya majaribio za mashine (BVR) kwa kuandikisha wapigakura katika Kata ya Kibuta, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Pwani na Kihonda, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, mkoani Morogoro.

Kwa mujibu wa Nec, uandikishaji ulianza mwishoni mwa Machi mwaka huu na ulitarajiwa kumalizika Aprili 4, 2019 ukiwa umefanyika katika vituo 20 vya kuandikisha wapigakura ikiwa ni vituo 10 katika kila kata.

Hiyo ndio ratiba iliyotolewa na Mwenyekiti wa Tume, Jaji Semistocles Kaijage, Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa Machi mwaka huu, huku akifafanua kuwa uandikishaji huo ni kwa ajili ya kuvifanyia majaribio vifaa na mfumo wa Uandikishaji wapigakura ili kubaini changamoto kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi hilo.

Lakini ninadhani kwa ratiba hiyo na muda uliobaki kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa itawezekana kuandikisha Watanzania wote wenye sifa katika daftari hilo ili watumie haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi, cha msingi ni wao kujitokeza kama wanavyohamasishwa.

Ninasema hivyo kwasababu Nec imeanza uandikishaji kwa ajili ya kuvifanyia majaribio vifaa na mfumo wa uandikishaji wapigakura ili kubaini changamoto kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi hilo.

Katika mazingira hayo ni wazi kwamba inawezekana baadhi ya wale ambao wamefikisha umri wa kupigakura wasishiriki uchaguzi wa serikali, kama hawatachangamkia haki hii katika muda waliopewa.

Uchaguzi wa serikali za mitaa umepangwa kufanyika Oktoba mwaka huu, halafu ikumbukwe kwamba nchi hii ina wilaya zaidi ya 150, na sijui kama miezi sita iliosalia inaweza kutosha kuzifikia wilaya zote.

Kwa waliofuatilia uandikishaji wa wapigakura kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, watakumbuka changamoto zilizokuwa zikijitokeza zikiwamo za mashine za BVR kuharibika na kusababisha usumbufu.

Wakati mwingine waandikishaji walikuwa wakitumia muda mrefu tofauti na ilivyotarajiwa na hivyo kujikuta wakishindwa kufuata ratiba iliyokuwa imepangwa, kutokana na sababu ambazo ziko juu ya uwezo wao.

Kulikuwa na vituo ambavyo wakati mwingine uandikishaji ulikuwa unasimama kwa muda kufuatia mashine kukosa muendeshaji wa kuziendesha kwa ufasaha.

Changamoto hiyo ya uhaba wa wataalamu wa kuziendesha mashine hizo ulisababisha kazi ya kuandikisha wapigakura kwenda taratibu tofauti na ilivyotarajiwa.

Wapo wapigakura wengine ambao ilidaiwa kuwa tatizo la vidole sugu ambavyo vilishindwa kusomwa na mashine hizo za BVR za kuandikisha wapigakura, lakini baadaye tatizo likapatiwa ufumbuzi na wataalamu.

Sasa ni zaidi ya miaka miwili tangu kutokea hayo, inawezekana matatizo katika mashine hizo yakawa yameisha, lakini siyo vibaya kukumbusha kile kilichotokea na kusababisha usumbufu.

Lengo la kukumbusha changamoto hiyo ni kutaka kuwaandaa wataalamu vizuri ili kuhakikisha wenye sifa wote wanaandikishwa kwa wakati ili hatimaye waweze kushiriki katika uchaguzi.

Inawezekana Nec imeshajipanga vizuri katika hilo ili kuhakikisha wapigakura wapya wote wanaandikishwa kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa na ule mkuu wa mwaka 2020, kama ndivyo, basi itapendeza zaidi.

Nilijaribu kuonyesha wasiwasi kwamba huenda muda wa miezi saba uliobaki kabla ya uchaguzi wa serikali usitoshe kuwaandikisha wenye sifa wote kutokana na changamoto zilizojitokeza katika uandikishaji wa mwaka 2015.

**IDADI YA WAPIGAKURA WAPYA**

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, Antony Mavunde, serikali inakisia kuandikisha wapigakura wapya milioni nne kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Mavunde aliwahi kusema hayo Januari mwaka huu bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali na mbunge wa Viti Maalum Cecilia Pareso (Chadema), aliyetaka kujua ni lini Daftari la Kudumu la Wapigakura litaanza kuboreshwa.

Inafafanua kuwa katika zoezi la uandikishaji wa wapigakura kabla ya uchaguzi wa mwaka 2015, Nec iliandikisha Watanzania 22, 751, 292 wakati ile ya Zanzibar (Zec) 503, 193.

Hivyo ndivyo naibu waziri huyo alivyojibu, kwani Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara 5 (1) imeweka wazi kuwa raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 ana haki ya kupiga kura katika uchaguzi wa kupata kiongozi anayemtaka.

# Venezuela hatarini pande mbili zikiwania jeshi liwaunge mkono

Na Nimi Mweta

RAIS Nicholas Maduro ameshinda raundi nyingine ya mpambano endelevu na kiongozi wa upinzani Juan Guaido ambaye ni Spika wa Bunge asiyetambuliwa na Mahakama Kuu ya Venezuela.

Hiyo ni baada ya miito ya kiongozi huyo wa upinzani kwa jeshi kuunga mkono waandamanaji kugonga mwamba.

Amekuwa akitoa miito hiyo kwa takriban mwezi mmoja sasa, na hivi majuzi aliripotiwa kufika katika kituo cha jeshi la anga kurudia mwito huo, ambako sehemu ya wapiganaji ilimsikiliza.

Ulitokea uasi katika jeshi na hasa wasomi wa Jeshi la Anga (kama ilivyo kawaida katika nchi nyingi) lakini ulizimika baada ya muda mfupi uliposhindwa kupanuka.

Rais Maduro alitembelea kambi kubwa ya jeshi la nchi hiyo na kupokewa kwa shangwe na wanajeshi hao baada ya uasi huo kuzimika, wakati Guaido alijifariji kwa kukwama kwa jaribio la kulivuta jeshi kwenda upande wa upinzani.

Alitoa mwito wa maandamano ya amani katika kambi za jeshi, yaani kwa nia siyo ya kushinikiza Rais Maduro ajiuzulu kama ilivyo kwa maandamano ya kawaida, ila kulishinikiza jeshi liunge mkono waandamanaji, wakati siyo jeshi lililoko madarakani, ni chama na mgombea aliyepigiwa kura.

Ni hali tete kwa demokrasia kwani Guaido anatoa visingizio maridhawa kwa jeshi kuingilia kati, kuwa hiyo ndiyo demokrasia.

Ingekuwa ni katika miongo iliyopita, miito ya jeshi kuingilia kati ingeelekea moja kwa moja katika mapinduzi ya kijeshi ya kihafidhina, kulinda mali binafsi dhidi ya chokochoko za kimapinduzi, na kuweka mazingira muafaka kwa kampuni za nje kuwekeza katika madini, au hata viwanda na kilimo.

Nchini Venezuela, ni huyu Guaido ambaye kwa kiasi fulani anawakilisha mwelekeo kama huo, ila kwake inakuwa ni harakati ya kidemokrasia kwani kuna chama cha kimapinduzi kiko madarakani.

Kimsingi anachokifanya Guaido ni kulihamasisha jeshi liachane na hulka ya kimapinduzi lirudie utetezi wa mali binafsi na soko huria, kuondoa mapinduzi Venezuela.

Kinachompa nguvu Guaido ni idadi isiyo ndogo ya waandamanaji ambao wamechoshwa na kuzorota kwa uchumi wa Venezuela, huku wakiungwa mkono na sehemu kubwa ya Bunge la nchi hiyo, na nchi za Magharibi.

Kwa upande mwingine, washikadau wa Rais Maduro ni pamoja na wafanyakazi katika sekta ya umma nchini humo ambayo kimsingi imeshika hatamu za uchumi, na kwa sababu ya utegemezi kwa mauzo ya mafuta, kiwango cha kujishikiza na dola ni kikubwa, na wakati huo huo dola haina mbinu ya kufufua au kuchangamsha uchumi kwani unategemea zaidi mafuta. Hakuna sera mpya kuhusu mafuta anayoweza kubuni Rais Maduro.

Mkasa unaoendelea nchini Venezuela una vianzio vya kiitikadi vilivyorindima karne iliyopita na hatua kwa hatua hali hiyo inabadilika kote Amerika ya Kusini.



Rais wa Venezuela, Nicholas Maduro. **PICHA: MTANDAO**

> Ni hivyo uzalendo mpya ulijengeka, siyo wa kupinga uvamizi ila kupinga ubepari hodhi unaomiliki rasilimali kila mahali.

Ni mvutano kati ya itikadi ya ukombozi kutoka kwa wamiliki hodhi wa ardhi, majumba, kampuni hasa za madini, ambao pia kwa sehemu kubwa wanamiliki utii wa jeshi kwani linatokana zaidi na wenye fedha na wenye mamlaka ya serikali kuu na majimbo.

Ndio ambao vijana wao wanapatiwa kwa urahisi nafasi za kuingia jeshini na kusomea uofisa wa jeshi, hupendelewa zaidi katika kupewa vyeo au usimamizi wa taasisi ndani ya ulinzi na usalama kwa jumla kwa sababu ya unasaba unaoaminika kisiasa.

Ipo pia itikadi ya ukombozi ambayo chanzo chake halisi ni harakati ya kuzuia ardhi ya Amerika ya Kusini isichukuliwe na wahamiaji kutoka Ulaya, hasa Hispania kwa bara hilo, ila kwa eneo pana la Brazil ambayo ilimilikishwa Ureno (wakati huo ni Papa wa Roma ndiye anachukua maamuzi kuhusu nchi zinazogombana).

Harakati hiyo ilififia lakini wazawa wa nchi hizo wakawa wameingizwa katika dini mpya, kuhamia mijini na kushiriki kazi za viwandani ambako wana uhusiano wa kiharakati na wafanyakazi wa mashambani.

Ni hivyo uzalendo mpya ulijengeka, siyo wa kupinga uvamizi ila kupinga ubepari hodhi unaomiliki rasilimali kila mahali.

Ndiyo 'kigoda' cha kimapinduzi kilichoingiza madarakani chama cha ki-Bolivar (mpambanaji dhidi ya ukoloni mamboleo mwanzoni mwa karne iliyopita na baba wa mapinduzi Amerika ya Kusini) kikiongozwa na hayati Hugo Chavez.

Licha ya kuwa Venezuela ilikuwa na uchumi unaong'ara na demokrasia ya mfano katika bara hilo, mwaka 1999 wapiga kura wakamchagua Chavez ambaye unaweza kumfananisha na aliyekuwa kiongozi wa vijana wa ANC nchini Afrika Kusini, Julius Malema.

Tangu 1999 chama hicho kimejikusanyia wafuasi lukuki wa mfumo wa uchumi wa umma wasiotaka ufilisiwe, wapewe mabepari wa ndani na nje, hivyo wanavumilia taabu.

Unaweza kusema mvutano wa Venezuela ni kama ilivyokuwa hapa nchini wakati wa miaka ya mwisho ya Ujamaa, upande mmoja ukisema Rais Nyerere 'haambiliki,' abadili mbinu za uchumi ili uchanganye na mambo yaende sawa, wakiwa na maana ni pamoja na mashirika ya umma kumilikishwa wageni.

Upande wa pili, wale waliokuwa wanaona kuna taabu lakini hawako tayari kuachia kila kitu, ndio walihangaika hadi kupata muafaka wa viwango vya mageuzi, yakaanza kwa nguvu awamu ya pili na kupooza awamu ya tatu.

Hisia yao alijumuisha Mwalimu akiongea kuhusu yeye mwenyewe kuwa hayuko tayari 'kugeuka jiwe,' yaani kurudi tulikotoka, ukoloni.

Ambacho bado kinabishaniwa katika vyombo vya habari hasa vya Magharibi ni nafasi ya washirika wa Rais Maduro, hasa Russia na China, katika jitihada yake ya kuendelea kubaki madarakani, licha ya uhalisia kuwa alishindwa idadi ya wabunge na kuchaguliwa kwake upya 2013 kulikuwa na utata.

Maandamano yalianza mapema 2016 kutokana na kuvurugika hali ya uchumi baada ya kasi ya kukua uchumi wa China kutuama, na bei ya petroli kutokuwa na nguvu ya kupanda wakati sarafu ya Venezuela inashuka thamani kutokana na bei ya mafuta kushuka na kwa njia hiyo fedha za kigeni na mapato ya serikali.

Halafu mfumo wa Ujamaa na wa kiusalama una gharama kubwa, kwani taasisi za dola haziendeshwi kwa tija ila kuweka makada wamefurahi.

Russia na China zinasemekana kuwekeza katika uchumi wa Venezuela hasa kwa mitambo ya kusafisha mafuta na ujenzi wa miundombinu, na baadhi ya wadadisi wa nchi za Magharibi wanasema hii ndiyo sababu nchi hizo zinamzuia Maduro kuachia madaraka.

Haijapita hata wiki mbili Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo akatoa taarifa kuwa Russia imemzuia Maduro kutafuta hifadhi ya kisiasa huko Cuba, dai lililokuwa la kushangaza kwani vyombo vya dola likiwamo jeshi na Mahakama Kuu vinamtii Rais Maduro, sasa ahangaike kujisalimisha dhidi ya mkono upi wa dola mpya nchini humo?

Ina maana kuwa kuna propaganda zinapigwa ili wafuasi wa Maduro wafadhaike wakubali kufanyika uchaguzi haraka, huku upinzani ukionyesha unafaa zaidi.

# Dk. Bashiru: Urais umeipasua Zanzibar katika vipande vinne

- Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini na Pemba
- Kurejea kufundisha chuo kikuu baada ya ukatibu mkuu

INATOKA UK.13

kuteuliwa,"anasema.

Dk. Bashiru anasema CCM inaendeleza mpango wake wa kukusanya ushahidi wa wanachama 'wanaojipitisha' kutafuta kuungwa mkono ili kufikia nia zao za kuongoza.

**MPASUKO ZANZIBAR**

Dk. Bashiru anasema harakati za kuutaka urais zipo pia upande wa Zanzibar ambako kuna wanachama wanaotaka kuteuliwa baada ya Rais Shein kumaliza muda wake.

"Ugonjwa wa urais umeipasua Zanzibar kwa upande wa Kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini na Pemba...kisha kuna 'Zanzibara'," anasema akimaanisha wafuasi waliopo upande wa Bara.

Anasema maeneo hayo yana wanasiasa wanaotaka kila eneo kumtoa Rais wa Zanzibar `atakayemrithi' Dk. Shein.

"Sipo CCM kutafuta umaarufu wa kisiasa...sikubebwa kuwa hapa na wala sitombeba mtu... ni kama alivyo Rais (John Magufuli), Mzee (Philip) Mangula (Makamu Mwenyekiti wa CCM-Bara, na Dk. Shein (Rais wa Zanzibar) hawana haja ya kumbeba mtu," anasema.

**ONYO KWA WANUNUZI WA KURA CCM**

Katibu Mkuu huyo wa CCM anasema wakati ambapo Taifa linaelekea katika uchaguzi wa serikali za mitaa baadaye mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa 2020, wanachama wa chama hicho wenye hulka na mipango ya kununua kura wanapaswa kutambua kwamba wapo katika 'vita vikali' vyenye hatima ya kukatwa kuwania uteuzi.

Anasema viongozi wa ngazi za juu katika CCM wakati huu, Mwenyekiti, Rais Magufuli, Makamu Mwenyekiti - Zanzibar, Rais Dk. Shein, Makamu Mwenyekiti - Bara, Mzee Mangula na Katibu Mkuu (Bashiru) hawahongeki na kwamba `hawakubebwa' katika uchaguzi, hivyo `hawatambeba' mgombea yeyote.

Anabainisha rushwa inaposhamiri ndani ya chama tawala, inaenezwa hadi serikalini kwa vile miongoni mwao wanateuliwa kushika nafasi tofauti katika utawala wa nchi.

Ni kwa mtazamo huo, Dk. Bashiru anaviasa vyombo na asasi za habari kushughulikia kero zinazohusiana na rushwa ili kuwa sehemu ya kufanikisha mapambano dhidi ya uovu huo.

**MAGUFULI KUONGEZA MUDA WA UTAWALA**

Kuhusu hili, Dk. Bashiru anasema hakuna sababu kwa Watanzania kuzungumzia suala la Rais Magufuli kuwapo madarakani zaidi ya miaka 10, kwa vile licha ya kukanusha kwake mara kadhaa, lakini bado yupo katika awamu ya kwanza ya miaka mitano ya utawala wake.

"Hata atakaporejea tena katika awamu ya pili ya utawala wake, ataomba kuteuliwa na CCM, huo ndio utaratibu wetu," anasema.

Anasema zipo porojo zinazoenezwa kuhusu kuwapo uwezekano wa Rais Magufuli kutawala zaidi ya miaka 10, lakini zinapaswa kupuuzwa kwa vile hivi sasa kiongozi huyo amejikita kutekeleza majukumu yake ya utumishi wa umma.



Mwenyekiti wa CCM, Dk. John Magufuli. **PICHA: MTANDAO**

> Lakini hata watakaoshinda katika kura za maoni, hawatapaswa kushangilia, kwa maana kushinda kura za maoni si kigezo pekee cha kuteuliwa.

**ANAVYOCHUKIA KUITWA MHESHIMIWA, MKUU**

Anasema miongoni mwa mambo anayoyachukia, ingawa amelazimika kuyakubali kutokana na mfumo uliopo ni kuitwa Mheshimiwa ama Mkuu.

Kwa mujibu wa Dk. Bashiru, kutokana na mfumo alioukuta katika utekelezaji wa majukumu yake mapya baada ya kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, analazimika kuyakubali majina hayo ingawa dhamira yake kamwe haiyapendi.

Anasema msingi wa kutoyapenda majina hayo ni ukweli kwamba kila binadamu anastahili heshima dhidi ya mwenzake, hivyo kumtambua mmoja miongoni mwa watu kuwa ni mheshimiwa ni ishara ya kuiondoa haki hiyo kwa wengine.

"Tangu nilipopata nafasi hii ya u-Katibu Mkuu wa CCM, hizi sifa za Mhesimiwa, Mkuu...zipo nyingi sana hasa kwa watendaji wangu... nikiwaelekeza utasikia wanajibu nitatekeleza Mkuu ama nitatekeleza Mheshimiwa...lakini hawatekelezi," anasema na kusababisha vicheko kwa wahariri.

**UHURU NA USAWA**

Dk. Bashiru anasema Tanzania iliasisiwa kwa misingi mikuu ya uhuru wa Taifa na watu wake pamoja na usawa kwa watu wote.

Anasema hata kauli mbiu ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari inayosema 'Vyombo vya habari na demokrasia: uandishi wa habari na uchaguzi nyakati za upotoshaji wa taarifa,' inajijenga katika dhana mbili hizo.

Anabainisha kuwa jamii inapaswa kujengwa na watu wenye uwezo mpana wa kukosoa, kudadisi, kuchambua, kupima, kushawishi, kuongoza mwelekeo, fikra na mawazo. Ni kutokana na mtazamo huo, anasema kila mtu anapaswa kuzungumza akiwa huru pasipo kusimamiwa, ili mradi afuate kanuni za weledi na maadili.

"Hata ninyi (waandishi wa habari) mkitaka kufanikiwa kwa kiwango cha kuridhisha, ipo sababu ya kuzungumza bila woga," anasema.

**UGENI KATIKA SIASA**

Dk. Bashiru anathibitisha kuwa ni mgeni katika siasa, lakini anachokizungumza na kutenda ni kwa lengo la kuisaidia CCM kujisahihisha na kuwa karibu na wananchi hasa kwa kupitia vyombo vya habari.

**KUZITETEA NA KUZIENEZA FIKRA ZA MWALIMU NYERERE**

Dk. Bashiru anasema Oktoba 14, mwaka huu, Tanzania itaadhimisha miaka 20 tangu kifo cha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, hivyo asasi mbalimbali vikiwamo vyombo vya habari vinapaswa kutangaza, kuchambua na kuzieneza kazi, fikra na vitendo vya Mwalimu Nyerere.



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally. **PICHA: MTANDAO**

Anasema tangu kifo cha Mwalimu Nyerere kilichotokea kwenye Hospitali ya Mtakatifu Thomas jijini London, nchini Uingereza Oktoba 14, 1999, kuna vijana wengi waliozaliwa wakati huo ambao hawayaelewi maono na misimamo yake (Nyerere).

Katibu huyo wa CCM anasisitiza umuhimu wa kuandika na kumtangaza Mwalimu Nyerere pasipo kutumia hulka za kasuku, bali kwa kutambua alikuwa binadamu wa kawaida na kwamba jambo la msingi ni kwa maandishi hayo kuwa yenye heshima na adabu.

**'KUPOTEA' KWA WAPIGANIA UHURU WA AFRIKA**

Mbali na Mwalimu Nyerere, Dk. Basshiru anasema vijana wengi wakiwamo baadhi ya wasomi wa sayansi ya siasa katika vyuo vikuu hawawajui waliokuwa wapigania uhuru hasa Kusini mwa Afrika.

Anatoa mfano kuwa mwaka 2006, alipokuwa akiwafundisha wanafunzi wa mwaka pili wa shahada ya sayansi ya siasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliwauliza wanafunzi 32 waliokuwa darasani jinsi wanavyomfahamu Samora Machel lakini hakuna hata mmoja aliyemfahamu.

Machel alikuwa Rais wa kwanza wa Msumbiji aliyeshiriki katika harakati za kudai uhuru kwa mataifa ya Afrika, hususani katika nchi zilizokuwa mstari wa mbele ikiwamo Tanzania.

Oktoba 20, 1986, Machel na maofisa wengine 33 wa iliyokuwa serikali walikufa kwenye ajali ya ndege aina ya Tupolev iliyoanguka Afrika Kusini wakati ikitokea Zambia kurudi Msumbiji.

Utawala wa Afrika Kusini wa wakati huo wa Wazungu wachache na washirika wao wa Magharibi, ulidai kuwa ajali hiyo ilitokana na uzembe wa wafanyakazi wa ndege hiyo.

Dk. Bashiru anasema kutokana na kukosekana kwa ufahamu huo, mwaka 2008 kilipoanzishwa Kigoda cha Mwalimu Nyerere kupitia muasisi wake, Profesa Issa Shivji, lilianzishwa somo la Pan African Thoughts and Practices kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza ya sayansi ya siasa, likiwa ni somo la hiari.

"Kwa hali hiyo utaona kwamba nchi isiyokuwa na historia, na watu wasiokuwa na historia ni mfu," anasema.

**UMAHIRI WA MWALIMU NYERERE**

Kiongozi huyo wa chama tawala anasema hakuna jambo katika jamii ambalo Mwalimu Nyerere hakulijadili wakati wa uhai wake, hivyo kutaka jamii ishiriki katika kuyaendeleza.

"Mwalimu Nyerere aliyajadili mambo yote, iwe ni maisha, demokrasia, vyombo vya habari, mshikamano, uongozi wa kisiasa, uchumi, kilimo, viwanda kwa nchi masikini, ulinzi na usalama na haki za binadamu," anasema.

Anabainisha kwa upande wa haki za binadamu, Mwalimu Nyerere alitetea hadi wakati wa kifo chake, haki ya kila raia kuchagua ama kuchaguliwa pasipo kujali chama chake cha siasa.

**UHURU NA DEMOKRASIA**

Dk. Bashiru anasema madai ya haki za uhuru na demokrasia nchini hayapaswi kuelekezwa kwenye taasisi zinazolenga kutafuta utawala wa nchi pekee, bali na kwa asasi nyingine za kijamii zikiwamo za wanataaluma.

**KUTUMBUA**

Dk. Bashiru anasema baada ya uteuzi wake kushika nafasi hiyo, hakutarajia kuwekeza katika utumbuaji (adhabu) kwa wanachama, bali kutoa huduma zenye kukijenga chama hicho na kuusaidia umma wa Watanzania.

Anasema kwa hali hiyo, hayupo tayari kutumikia wadhifa wowote wa kuteuliwa kisiasa baada ya kuwa Katibu Mkuu wa CCM, badala yake atarejea kufundisha Chuo Kikuu.

**UVCCM KUPOTEZA MWELEKEO**

Katika hili anasema kuwa umadhubuti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) umepungua, hali inayoibua hitaji la kuimarisha mafunzo kwa kada hiyo.

Anasema CCM imedhamiria kuimarisha mafunzo ya 'kijana na uongozi' kupitia vyuo vyake vilivyopo maeneo tofauti ikiwamo Ihemi mkoani Iringa na Kibaha (Pwani).

"Hata kama watakaopitia kwenye vyuo hivyo hawatabaki CCM, lakini lengo kuu ni kuwa na viongozi bora wa baadaye," anasema.

**MAISHA MAGUMU**

Akizungumzia kuwapo kwa dhana ya maisha magumu kwa raia anasema inafikirika, kutokana na uwapo wa viongozi wasiowajali watu wengi wanaoishi katika hali hiyo.

Anasema uboreshaji wa sekta ya kilimo ni miongoni mwa hatua muhimu zitakazowezesha nchi kukabiliana na umaskini na kuwaondoa watu katika maisha magumu.

Anabainisha, takwimu zinaonyesha kuwa ingawa takribani asilimia 90 ya Watanzania ni wakulima, lakini mchango wa sekta hiyo kwa uchumi wa taifa umebaki kuwa chini ya asilimia 30.

> Ndiyo maana wakulima wameendelea kuishi maisha magumu huku wakiwezesha shibe kwa kikundi cha watu wachache.

"Ndiyo maana wakulima wameendelea kuishi maisha magumu huku wakiwezesha shibe kwa kikundi cha watu wachache," anasema na kuongeza:

"Na miongoni mwa watu wanaosababisha maisha magumu kwa wakulima ni 'madalali wa kati' wakiwamo viongozi wa kisiasa na serikali katika ngazi za msingi, wanaotumia kigezo cha kulifikia soko kwa urahisi."

Anasema ndiyo maana serikali inajitahidi kukata mirija ya unyonyaji wa wakulima wakiamini kwamba hapatakuwa na viwanda endelevu pasipo kuiimarisha sekta ya kilimo.

**KUSUSIWA UCHAGUZI**

Dk. Bashiru anairejea sifa ya Mwalimu Nyerere kuhusu haki ya kuchagua na kuchaguliwa na kusema si jambo jema kwa vyama vya upinzani kususia uchaguzi.

Anasema vyama vinapaswa kujiimarisha kwa sera, dira na mwelekeo madhubuti ili kuomba ridhaa ya uongozi kwa wananchi.

"Lakini kama (wapinzani) wakisusia uchaguzi, mnategemea sisi (CCM) tufanyeje?" anahoji.

***Mwandishi wa makala haya anapatikana kupitia simu namba 0754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.***




Mfuasi wa Kiongozi wa chama cha EFF, Julius Malema, akionyesha picha yake. **PICHA: MTANDAO**

## Malema na ushawishi Afrika Kusini kuelekea uchaguzi Mkuu

HUENDA Julius Malema asiweze kuondosha sifa ya 'hamasa kubwa' anayotazamwa kuwa nayo, lakini kiongozi huyo wa chama cha pili kwa ukubwa cha upinzani Afrika Kusini mwenye umri wa miaka 38, hatazamwi tu kama mwanasiasa mwenye ghadhabu.

'Mwana wa kiasili,' kama anavyotambulika na wafuasi wa chama chake cha Economic Freedom Fighters (EFF), amekigeuza chama chake kwa muda wa miaka sita iliyopita, kuwa kikosi chenye nidhamu kilichoweka ajenda katika maeneo kadhaa ya sera.

Alitimuliwa kutoka chama tawala cha African National Congress (ANC) mnamo mwaka 2012.

Malema, au 'Juju' kama anavyoitwa wakati mwingine ameiweka EFF katika nafasi ya kuwa mrithi wa ajenda kali ya ANC na amefichua mapengo ya chama hicho tawala.

Lengo la kiongozi huyo mkuu wa EFF kuhusu ukosefu wa usawa nchini Afrika Kusini na kushindwa kwa ANC kuirudisha ardhi kutoka kwa jamii ndogo ya watu weupe kwenda kwa idadi kubwa ya watu weusi nchini, kumekigharimu uungwaji mkono chama chake cha zamani ambacho kiliongoza vita dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Chama cha EFF kilijinyakulia asilimia 6 tu ya kura zilizopigwa mnamo mwaka 2014 katika awamu ya kwanza ya uchaguzi mkuu, lakini ushawishi wake unaonekana kuzidi nguvu takwimu hizo.

Wabunge 25 wanaoonekana kuvaa nguo nyekundu na kofia bungeni na mbinu ya kutimuka bungeni, na Malema kutoa mistari ya nukuu, inamaanisha yeye na chama chake amefanikiwa kuwavutia watu kwa wanayoyafanya. **BBC**

MAKALA

# Korea Kaskazini yatunisha misuli, yafyatua makombora



Kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong-Un (aliyekaa), akiwa na majenerali wa Jeshi la Korea wakati wa jaribio la makombora ya masafa mafupi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Michael Eneza**

KOREA ya Kaskazini imerusha makombora kadhaa ya masafa mafupi, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Korea Kusini, na kushangaza dunia kuwa jitihada ya kufikia uelewano na Marekani iko mashakani.

Hata hivyo, Rais Donald Trump wa Marekani amepuuzia tukio hilo akisema kuwa kiongozi wa Korea ya Kaskazini, Kim Jong-un ametoa ahadi kwake ambazo Trump anatazamia kuwa ataziheshimu, na kuwa Kim ana kila sababu ya kuhakikisha kuwa anaendelea kujenga uhusiano bora na Marekani.

Inaelekea Korea Kaskazini yenyewe haikutangaza kuwa imefanya majaribio hayo ya makombora, hali inayoonyesha kuchelea kuvuruga majadiliano.

Taarifa ya majaribio hayo iliyotolewa na makao makuu ya jeshi la Korea Kusini ilisema makombora hayo yalirushwa kutoka kisiwa-nusu cha Hodo Mashariki ya nchi hiyo, wakati wachambuzi wa habari wanasema 'ikithibitishwa' itakuwa ni mara ya kwanza Korea Kaskazini kufanya majaribio ya makombora tangu irushe kombora la masafa marefu mwezi Novemba 2017.

Taarifa nyingine zilikumbushia kuwa mwezi uliopita Korea Kaskazini ilisema imefanya jaribio la silaha mpya ya kuelekezwa katika uwanja wa vita.

Kinachotiliwa maanani zaidi katika hisia kuhusu tukio hilo ni kuwa ni jaribio la kwanza la silaha tangu mkutano wa Kim na Trump uvunjike bila maafikiano yoyote, na bila

"Ni kama vile vile kulikuwa na haja ya Korea Kaskazini kutingisha anga za kimataifa kuwa bado ipo, ina uwezo wa kutengeneza silaha, kuwa haijafifia bado.

kuwapo taarifa ya pamoja kuhusu kilichojiri katika mazungumzo hayo.

Akitoka katika mazungumzo hayo, Rais Trump alisema kuwa kiongozi wa Korea Kaskazini alikuwa ameleta pendekezo 'dili' bovu ambalo Marekani isingeweza kukubali, katika mazungumzo hayo huko Hanoi, Vietnam.

Jumamosi, baada ya jaribio hilo la makombora mafupi kutangazwa, Rais Trump akasema katika ujumbe wa mtandaoni kuwa anaamini kiongozi huyo wa Korea Kaskazini hatafanya lolote linaloweza kuhatarisha jitihada za nchi yake kuboresha uhusiano (na Marekani) na kufikia hali ya kawaida ya kiuchumi, yaani kuondolewa hatimaye kwa vikwazo kwa nchi hiyo. Ni suala ambalo Kim alitaka limalizwe haraka katika mkutano wa Hanoi.

Katika nyongeza ambayo baadhi ya wachunguzi wa habari walijitafuta inaashiria nini, Trump alisema kuwa kiongozi wa Korea Kaskazini "pia anajua kuwa niko pamoja naye na hataki kuvunja ahadi yake kwangu."

Baadhi ya wachunguzi wa habari walieleza kuwa kufyatua makombora ya masafa mafupi siyo tatizo kwa Trump kwa sababu yanaweza kuwa tishio tu kwa majirani zake na siyo hatarishi kwa usalama wa Marekani.

Ina maana kuwa kufyatua mabomu ya masafa mafupi ni tatizo la kidiplomasia linalohitaji kujadiliwa na majirani zake, hasa Korea Kusini na kwa maana hiyo Trump hakuwa na haja ya kuingilia suala hilo kama ni la Marekani.

Ina maana kuwa tukio hilo halikuwa na maana kwa Trump licha ya kuwa Korea Kaskazini muda wote inataka iongee na Marekani kuhusu silaha zake za maangamizi, ikafikia mahali inarusha makombora ya masafa marefu yanayoweza kufika Marekani.

Alichokuwa anasema Rais Trump ni kuwa hafadhaishwi na jaribio hilo kwani halina madhara yoyote kwa Marekani, na limefanywa kwa njia ya kuhakikisha kuwa halikuwa na dhamira ya kuhujumu majadiliano kuhusu utengenezaji na majaribio ya makombora ya masafa marefu au silaha za nyuklia ambazo ni za hali ya juu (mabomu mazito ya uteketezaji wa kina). Ni silaha ya kawaida medani ya vita.

Hata hivyo, kuna tatizo katika mtazamo huo wa Korea Kaskazini, kwamba licha ya kuwa silaha iliyojaribu siyo tishio kwa Marekani, lengo ni kugusa hisia za Marekani ili ianze kutambua umuhimu wa kusikiliza madai au matakwa ya Korea Kaskazini.

Hadi sasa Rais Trump amekataa mapendekezo ya Korea Kaskazini ambayo kimsingi yanataka kuondolewa vikwazo vya kiuchumi Marekani ilivyoweka kwa nchi hiyo, na vingi zaidi ni vya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, vilivyokubaliwa na majirani zake na maswahiba kiitikadi kwa kiasi fulani, yaani China na Russia.

Ilifika mahali majirani zake walichoka Korea Kaskazini, wakaiachia iadhibiwe.

Bado hakuna maelezo yoyote ya kina kuhusu mustakabali wa kimkakati kwa upande wa Korea Kaskazini, kwani Rais Trump alikataa kabisa kuondoa vikwazo kwa nchi hiyo mradi haijaingia katika mpango rasmi wa kufuta utengenezaji na uhifadhi wa silaha za nyuklia na majaribio ya makombora, hasa yanayoilenga Marekani.

Hata hivyo, kuna wakati Korea Kaskazini ilionyesha dhamira ya kubadili uelekeo na kuacha kutumainia kuwa silaha za nyuklia na kulundika makombora ndiyo kutaihakikishia usalama wake, na badala yake ilenge katika kuinua uelewano na nchi nyingine, kuanzia majirani zake Korea Kusini na Japan, halafu Marekani. Tatizo ni kuwa uelekeo kama huo unabidi uendane na mabadiliko kiasi fulani ya kisiasa Korea Kaskazini, uhuru uongezeke.

Kwa historia ya nchi zinazotawaliwa kiimla au za kimapinduzi, hatari ya kila kitu kuharibika haipo katika kudumu utawala huo bali ikianza jitihada ya marekebisho, kuwa watu wakishaanza kupewa sauti za kuzungumza bila woga hadharani, utawala uliopo hauwezi kujua hali hiyo itaisha vipi, au itaisha wapi.

Ni uoga wa mageuzi ndiyo unaofanya Korea Kaskazini isite kuleta mabadiliko halisi, na inachotaka ni kuwa ionyeshe dhamira ya kuacha kutengeneza na kurusha makombora ya masafa marefu ambayo kimsingi yanailenga Marekani.

Kwa hatua hiyo Marekani iondoe vikwazo vya uchumi dhidi yake, siyo kwa kuondoa silaha zote, kutojaribu makombora.

Ndiyo maana hatua hii ya kujaribisha masafa mafupi ni ngumu kuelezea ina dhamira gani, kwani kundi pekee linaloweza kufarijika na majaribio hayo ni utawala wa jeshi la Korea Kaskazini, wajihisi bado wanahitajiwa na siyo kuwa Mwenyekiti Kim anangonjea mazungumzo mengine na Marekani kuchukua hatua yoyote kuhusu ulinzi na usalama.

Ni majaribio ya silaha yenye lengo ya kufikia tu malengo ya kiutawala Korea Kaskazini, kama vile ni kukamilisha ratiba, na ndiyo maana kulikuwa na usiri fulani katika vyombo vya habari vya nchi hiyo, kwani mara nyingi wakijaribu silaha wanatangaza. Ni pale wanapolenga hisia za nchi za nje, hasa Marekani.

Ina maana pia kuwa Rais Trump amesoma vizuri somo alilolilandaa Mwenyekiti Kim, kuwa asihangaishwe na zoezi hilo la kufyatua makombora kwani bado hakuna hitaji la Korea Kaskazini kutokuwa na silaha kabisa, na silaha hizo ni za kawaida hata kama zinaweza kufika Korea Kusini.

Labda zinaweza zisifike Japan kwani ni za kilomita 60 hadi kilomita 200, hivyo ni kama silaha za Korea Kaskazini kujilinda endapo kuna uvamizi wa aina yoyote, na siyo silaha za kushambulia nchi nyingine kutoka mbali.

Ni kama vile vile kulikuwa na haja ya Korea Kaskazini kutingisha anga za kimataifa kuwa bado ipo, ina uwezo wa kutengeneza silaha, kuwa haijafifia bado.

MAKALA

# Siku 100 DRC za Rais Tshisekedi madarakani, amefanikisha nini?

RAIS Felix Tshisekedi ametimiza siku 100 tangu kuapishwa kwake, lakini hadi leo bado wananchi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wanasubiri kuona mageuzi aliyoahidi, yakiwamo ya kuboresha hali ya maisha ya wafanyakazi wa serikali.

Hadi sasa, bado mkuu huyo wa nchi hajamteua waziri mkuu wala kuunda serikali mpya, ikiwa ni miezi minne tangu kufanyika uchaguzi mkuu wa nchi hiyo.

Kwenye hotuba aliyoitoa mwanzoni mwa mwezi Machi alipozindua mpango wa haraka wa 100, Rais Tshisekedi alisema:

"Ndani ya siku 100 za utawala wangu, nitakuwa nimeshakamilisha baadhi ya miradi kwenye sekta ya usalama, siasa, jamii, uchumi, miundombinu na huduma kwa vijana."

Ahadi hizo za Rais Tshisekedi zilitarajiwa kutekelezwa na serikali mpya, lakini hadi sasa bado hajateua waziri mkuu ambaye ndiye anapaswa kuunda baraza hilo la mawaziri la serikali mpya.

Jijini Kinshasa, kwa mfano, kunashuhudiwa miradi kadhaa ya utengenezaji wa barabara.

Shirika la ujenzi wa barabara lilisema kwamba katika kipindi cha siku 100 za utawala wa Tshisekedi, lingetengeneza kilomita 40, lakini hadi sasa ni chini ya kilomita 20 zilizotengenezwa.

Upinzani katika DRC unaukosoa utawala wa Rais Tshisekedi katika kipindi cha siku 100 tu za utawala wake.

Kiongozi wa vuguvugu la Lamuka, Martin Fayulu, amesema kwamba anachofanya Tshisekedi katika kipindi hiki ni kuponda fedha za umma kwa safari za kila siku.




Rais Felix Tshisekedi wa DRC. **PICHA: MTANDAO**

Kwa upande wake, Valentin Mubake, mshirika wa zamani wa Etienne Tshisekedi, anasema kutokuwepo kwa serikali mpya kunaonyesha wazi udhaifu wa uongozi wa Tshisekedi:

"Walitafuta madaraka kwa ajili ya madaraka tu... ni miezi minne sasa hakuna waziri mkuu, hakuna serikali, na hakuna chochote wanachokifanya ama watakachokifanya," anasema.

Hata hivyo, Rais Tshisekedi anasifiwa na mashirika ya kutetea haki za binadamu kwa hatua za mwanzo alizochukua, hasa kwa kuwaachia huru wafungwa 700 wakiwamo wale wa kisiasa.

Na vilevile kumruhusu Moise Katumbi kurejea nchini humo.

Tshisekedi aliahidi pia kurejesha usalama huko Mashariki mwa nchi, na vile vile kupambana na rushwa katika kipindi cha siku 100.

Rais Tshisekedi aliahidi atahakikisha vyombo vya kisheria vinasimamiwa na watu wenye maadili

"Kwenye sekta nyingine muhimu ikiwemo ile ya kisheria, nitahakikisha kwamba vyombo vya kisheria vinamilikiwa na watu wenye maadili bora na wasio na utovu wa nidhamu, ambao watapambana na rushwa iliyokithiri nchini," alisema.

Lakini, wakati DRC imeshuhudia kujisalimisha kwa baadhi ya wapiganaji huko Kivu na Kassai, bado kumekuwa na mashambulizi kadhaa dhidi ya jeshi kwenye majimbo ya Kivu ya Kaskazini na Ituri.

Jijini Kinshasa, watu wana maoni tofauti kuhusu utekelezwaji wa ahadi za Rais Tshisekedi.

Wengi wanahisi kwamba hakujakuwako na mabadiliko makubwa, mfano wa Muyaya Luaba, mkazi wa Mkoa wa Lemba, Mashariki mwa jiji la Kinshasa:

"Hakuna mabadiliko hata, hali ni ileile, wewe ni mwandishi habari na unafahamu vyema kwamba hali bado ni mbovu."

Utafiti ulioendeshwa na shirika la maoni la TARGET SARL mwezi Machi ulielezea kwamba asilimia 53 ya raia wa DRC waliridhika na siku 30 ya utawala wa Felix Tshisekedi. DW

## Mvutano ndani ya chama tawala Kenya, Jubilee waongezeka?

NAIBU wa Rais wa Kenya, William Ruto, amekitetea chama tawala Jubilee kuwa kiko imara licha ya kuibuka makundi mawili yanayokinzana, Kieleweke na Tangatanga.

Ruto amewakosoa baadhi ya viongozi wa chama tawala cha Jubilee kwa madai ya kujiunga na upinzani ili kuvurugu azma yake ya kuwania kiti cha urais kwenye uchaguzi mkuu ujao.

Hata hivyo, anasema kuwa Jubilee iko imara licha ya kuibuka makundi hayo mawili yanayokinzana.

Salamu za heri kati ya Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani, Raila Odinga, zinazidi kuzua mtafaruku katika chama cha Jubilee.

Sasa pameibuka makundi mawili ndani ya chama hicho tawala, kundi la Tangatanga linalomuunga mkono na lile la Kieleweke linalompinga.

Licha ya hali hiyo, bado Ruto anashikilia msimamo kuwa hakuna mpasuko ndani ya chama hicho.

"Na hiki chama sio lazima mtu fulani akiongoze kama kutakuwa na mtu bora kuzidi Ruto... sio lazima niongoze... huyo tutamuunga mkono, lakini sote tutakuwa ndani ya Jubilee...kile ambacho hatutakubali ni kuletewa fitina za vyama vingine," anasema.

### UKIMYA WA RAIS KENYATTA CHANZO CHA MPASUKO?

Kumekuwa na mvutano ndani ya chama tawala Jubilee kinachoongozwa na Rais Uhuru Kenyatta.

Wachambuzi wanasema kuwa mpasuko unaoonekana katika chama tawala, umesababishwa na ukimya wa Rais Kenyatta kuhusu mrithi wake na badala yake amekuwa akishirikiana na kiongozi wa upinzani, Raila Odinga.

Wafuasi wa makundi haya mawili ya Tangatanga na Kieleweke wanasema makundi hayo yanalenga kupanua demokrasia ndani ya chama.

Joshua Kutuny aliyekuwa rafiki wa karibu wa Ruto na mbunge wa Jubilee sasa amebadilika na kuwa mkosoaji wake mkubwa.



Naibu Rais wa Kenya, William Ruto. **PICHA: MTANDAO**

"Imani imetuleta sisi watu wa Kieleweke pamoja, tulianza wachache watu wanne, sasa tuko zaidi ya wabunge 60 ndani ya huu msafara...hakuna siku rais ameniambia kuwa haungi mkono...wale wengine walianza wakiwa 100 sasa naona wako saba," anasema.

### JOTO LINAZIDI KUFUKUTA KUELEKEA UCHAGUZI MKUU

Ruto ameyataka makundi hayo mawili kukoma kupiga siasa hadi wakati mwafaka utakapojiri.

Ameukosoa upinzani kwa kusema kuwa hauna msingi wowote wa kukishauri chama chake kuhusu masuala ya maendeleo.

Gathoni Muchomba ni mbunge maalum wa upande wa Tangatanga, na anadhani Jubilee kinapaswa kuwa mwakilishi wa taifa zima la Kenya. "Tumesikia wengine wameanza vyama vyao vya ukabila...ili Jubilee ije pamoja, vyama 14 vilivunjwa ili kiwe chama cha kitaifa,"anasema.

Licha ya kwamba bado miaka mitatu kwa Wakenya kushiriki kwenye uchaguzi mwingine, tayari joto la siasa linazidi kufukuta pembe zote za taifa, hali inayoibua suala la viongozi kutimiza ahadi zao kabla ya uchaguzi huo.

Wanasiasa wanazunguka kote, kutafuta miungano na kura. Katika taifa ambalo vyama hutumika tu kama viunzi vya kumpitisha mtu kuwa kiongozi na baadaye vikazikwa, je chama tawala cha Jubilee kitayashinda mawimbi haya na kuibuka kidedea kwenye uchaguzi mkuu ujao ama kitakufa tu kama vinavyokufa vyama vyingine na kusahaulika nchini Kenya? **DW**

# Spika nchini Marekani amshukia Mwanasheria Mkuu wa Trump



Rais wa Marekani, Donald Trump. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

WACHUNGUZI wa habari nchini Marekani, wameshangazwa na nguvu inayotumiwa na viongozi wa Baraza la Wawakilishi ambako chama cha upinzani cha Democratic kina wingi wa viti, kumshughulikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, William Barr.

Wanamshutumu kujitahidi kiasi alichoweza kumkingia kifua Rais Donald Trump na hivyo kutoa muhtasari na uelekeo usio sahihi kuhusu kilichomo katika ripoti ya uchunguzi wa Russia kuingilia uchaguzi mkuu wa Marekani mwaka 2016.

Ikafikia hatua ambako mwanasheria maalum Robert Mueller aliyeendesha uchunguzi akamwandikia barua ya wazi Mwanasheria Mkuu kumsuta kwa hilo.

Imefikia mahali wadadisi wanauliza kama Spika wa Baraza hilo, Nancy Pelosi, anasuka mpango wa kufikia mashtaka ya Mwanasheria Mkuu kwa kile alichokiita 'jinai' ya kulidanganya Bunge.

Pia kulikuwa na hoja kadhaa imekuwaje Mwanasheria Mkuu akakosa kufika katika mahojiano maalum kutoa ushuhuda mbele ya kamati ya Wawakilishi, lakini akatokea katika mahojiano na Kamati ya Senate ambako chama cha Republican kilichoko madarakani kina wingi wa wajumbe.

Wengi kati yao wanaelewa anachofanya Rais Trump hivi sasa na hata walivyomhoji Mwanasheria Mkuu uelewano na kukutanisha mitazamo kulikuwa kunaonekana kiasi fulani.

> Moja ukiwa ni juu ya uwasilianaji wa timu ya Trump ya kampeni na waingiliaji wa Russia wakati kampeni inaendelea.

Mwanasheria Mkuu alitoa taarifa ya kurasa nne kuhusu tume ya uchunguzi ilichogundua na kuainisha katika ripoti yake, muhtasari ambao kwa jumla umepingwa na wabunge (wajumbe wa Baraza la Wawakilishi).

Wakati mmoja Spika Pelosi alimtangazia Mwanasheria Mkuu kuwa hawana haja na muhtasari wake, wala ushauri wake kuhusu nini kifanyike kuhusu ripoti hiyo, ila aichapishe kama ilivyo na kuiwasilisha bungeni, ili wao waangalie cha kufanya.

Alichokifanya Mwanasheria Mkuu ni kufuta maeneo au aya ambazo zinawahusu watu walioshika nyadhifa muhimu serikalini au wanaoweza kuingiliwa katika faragha, ikawa pia ni tatizo la kisheria.

Baada ya Spika Pelosi kusisitiza kuwa hakuwa anataka chama cha Democratic kuanza mkakati wa kutaka kushtakiwa Rais Trump kwa kujaribu kuzuia ukweli usipatikane kuhusu kuingilia kwa Russia katika uchaguzi mkuu huo, ndipo akatoa tamshi kuwa Mwanasheria Mkuu alitenda kosa la jinai la kulidanganya Bunge.

Ni hapo wakinzani wake wakaanza kuvumisha kuwa Pelosi anajipanga kuanza mkakati wa mashtaka ambao chama cha Democratic kinaona wanauweza, yaani wa kumshtaki Mwanasheria Mkuu na siyo Trump.

Imekuwa ni kama mzaha katika tasnia ya habari, kuwa Democratic hawamwezi Trump sasa wanatafuta pa kutolea hasira.

Katika tukio linaloendana na msimamo wa Spika Pelosi kuhusu muhtasari alioutoa Barr na kutotaka kuhojiwa na kamati ya Baraza la Wawakilishi, tofauti na Senate, mwanasheria maalum (zamani akiwa mkurugenzi wa Shirika la Upelelezi la Marekani, FBI) Robert Mueller alipeleka barua kwa Mwanasheria Mkuu halafu akainakili bungeni na vyombo vya habari.

Alimshambulia Mwanasheria Mkuu kwa kukosa uadilifu katika muhtasari aliotayarisha, kuwa haukuwa wenye sura sahihi ya kilichoko kwenye ripoti hiyo.

Kwa mfano alishangaa ni kwa njia gani William Barr alifikia tamati kuwa kamati haikuona baya lolote alilotenda Trump.

Wachunguzi wa habari nchini Marekani walionyesha mshangao kwa mchunguzi maalum huyo kutoka hadharani na kuonyesha anachohisi kuhusu ripoti yake ilivyojumuishwa na wasaidizi wa karibu wa Rais Trump na kwa maana hiyo muhtasari aliotoa Barr.

Ni muhtasari huo ambao Trump aliutumia kusema kuwa ripoti ya uchunguzi imemuondolea tuhuma zote na kumsafisha kabisa, wakati ambapo ukweli ni kuwa ripoti ilisema tu kuwa hakuna ushahidi wa kutosha kuleta mashtaka ya ushirikiano kati ya timu ya Russia iliyoingilia kampeni, na timu ya kampeni ya Trump.

Ilisema hata hivyo Bunge ndilo lingeamua kama yawapo mashtaka ya kujaribu kuzuia ukweli kufahamika wakati uchunguzi wa uingiliaji huo unaendelea, hasa kwa kufukuza maofisa kadhaa.

Baadhi ya wadadisi wanasema kuwa hatua hiyo (ya kuandika barua kwa Mwanasheria Mkuu na kuitoa hadharani) inashangaza kwani Bob Mueller ni mtu wa kufuata kanuni kwa uadilifu sana.

Kwa maana hiyo alimshangaa Bill (William) Barr kwa kutokufanya hivyo, kutoa muhtasari jadidi na usiotafuta kuweka mambo sawa kwa aliyemteua katika nafasi hiyo, yaani Rais Trump.

Mueller anasema muhtasari alioutoa Barr siyo kamilifu haukuingiza yaliyohitajiwa kwa uadilifu, barua hiyo ikatolewa wakati Barr anajiandaa kufika mbele ya Kamati ya Sheria ya Senate, raia wa kawaida wakapata picha sahihi Mueller anafikiri nini kuhusu ripoti hiyo.

Wapo pia maofisa wa Idara ya Sheria walioshiriki katika uchunguzi uliosimamiwa na Mueller ambao pia wameeleza kutoridhika kwao na muhtasari wa Mwanasheria Mkuu, ambao Mueller anasema haukuwa sahihi kutoa picha ya mazingira, undani na uhalisia wa kilichokuwapo katika ripoti.

Mueller alionyesha kukerwa na mkanganyiko ambao umejitokeza kuhusu kilichopo katika ripoti hiyo, na kwa sehemu kubwa hali hiyo inatokana na muhtasari ambao ulifanywa na Barr, hivyo kulazimisha watu, au wachunguzi, kuitafuta ripoti yenyewe kuona ni kiwango gani ilimtilia shaka Trump na watu wake. Kusema amesafishwa kabisa ilikuwa ni kuongeza chumvi na kuwakasirisha watumishi wa Idara ya Sheria, wakishangaa ni ripoti ipi inayozungumziwa.

Mueller alisema kuwa utata mkubwa katika hisia za watu kuhusu kilichogunduliwa katika uchunguzi huo ni hujuma kwa dhamira nzima ya kufanya uchunguzi, kwani Idara ya Sheria (Wizara ya Sheria) ilimteua mchunguzi (mwendesha mashtaka) maalum kuweka wazi matokeo halisi ya uchunguzi wa tukio hilo.

Kwa mwanasheria huyo wa siku nyingi aliyewahi kuwa mkurugenzi mtendaji wa FBI, ilikuwa ni suala la uadilifu na kiapo kuonyesha ukweli wa kilichogunduliwa au kudhihirishwa katika ripoti hiyo, na siyo kujaribu, kwa kadri ilivyoyezekana, kutoa muhtasari ambao unachanganya mambo kwa Trump. Alisafishwa na muhtasari, si ripoti.

Taarifa nyingine zilisema kuwa kuanzia mwezi Machi, mchunguzi Mueller na Barr walikuwa wakiwasiliana na inaelekea walifikia makubaliano ya kutolewa bila kupoteza muda kwa matokeo ya uchunguzi huo.

Kulikuwa na haja ya kuhakikisha kuwa uwasilishaji huo wa matokeo ya uchunguzi hautaleta madhara kwa faragha za kiserikali kama za jopo la uchunguzi, taarifa za kujasusi na mbinu zinazohusiana na uchunguzi wowote ule unaougusa jinai unaoendelea kwa sasa.

Mueller alisema alitayarisha mihtasari miwili ya kina kuhusu kilichopo katika majuzuu mawili ya ripoti hiyo.

Moja ukiwa ni juu ya uwasilianaji wa timu ya Trump ya kampeni na waingiliaji wa Russia wakati kampeni inaendelea.

Na muhtasari mwingine kuhusu uwezekano wa kutaka kuzuia ukweli usifahamike wakati uchunguzi unafanyika, akitaka muhtasari alioutayarisha utolewe kwa watu, si wa Barr utolewe peke yake wakati ni hafifu kuhusu undani wa kilichopo katika taarifa na mapendekezo ya kinachofuata.



# Machifu wamshukuru, wamzawadia Magufuli

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WIKI moja baada ya Rais John Magufuli kumaliza ziara ya siku tisa mkoani Mbeya, viongozi wa kimila wamemshukuru kwa kazi kubwa aliyoifanya mkoani humo na kutoa zawadi mbalimbali kwa ajili yake.

Viongozi hao walimkabidhi zawadi hizo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakimuomba azifikishe kwa Rais, huku wakiomba Serikali kuendelea kushirikiana nao katika masuala mbalimbali ikiwamo ulinzi wa mazingira na amani ya taifa.

Mwenyekiti wa viongozi hao, Chifu Rocket Mwashinga, alisema wao kama viongozi wa mila wanamshukuru Rais Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya katika ziara yake mkoani hapa, akisema kuwa ilionyesha dhahiri kuwa anawapenda wananchi wa Tanzania hasa wanyonge.

Alisema tangu alipochaguliwa mwaka 2015, hakuwahi kufanya ziara mkoani hapa, lakini wananchi wa Mkoa huo walikuwa wanafarijika na kazi alizokuwa anazifanya katika mikoa mingine.

Alisema furaha waliyokuwa nayo kutokana na ujio wake mkoani, ndio maana waliamua kumwandalia zawadi ili ajue kuwa wananchi wa walifurahi na walimpokea kwa mikono miwili.

"Amefanya mambo mengi mazuri katika Mkoa wetu, alisikiliza kero zetu, alitoa zawadi mbalimbali kwa wananchi wake na sisi kama machifu tulifurahi sana, na ndio maana tumeona tumpatie zawadi hizi, tunakuomba Mkuu wetu wa Mkoa utufikishie zawadi hizi," alisema Mwashinga.

Alisema zawadi walizomwandalia Rais Magufuli ni mbuzi, kiti cha kichifu (kigoda), mkuki, shuka jeupe, ungo na debe la viazi, na kwamba wataendelea kufanya kazi zingine kwa ushirikiano na Serikali.Akizipokea kwa niaba ya rais Magufuli, Chalamila aliwashukuru machifu hao kwa kutambua umuhimu wa viongozi wa Serikali, na kwamba hata yeye amekuwa akishirikiana nao kwa muda mrefu.

Chalamila alisema atawasilisha zawadi hizo kwa Rais kwa utaratibu utakaopangwa, huku akiwashukuru kwa zawadi hizo ambazo alisema baadhi wanaweza wakatafsiri kuwa ni ndogo.

"Rais ametusaidia kushughulikia changamoto mbalimbali za wananchi, ikiwamo kutoa fedha kwa ajili ya vituo vya afya, elimu na hata kuleta matumaini ya wananchi kupata huduma mhimu kama za maji, umeme na hata barabara, heshima hii mliyoitoa itakuwa ni sifa kwa mkoa pia," alisema Chalamila.

Alisema pamoja na mambo hayo, pia rais alitoa maelekezo mbalimbali kwa viongozi wa mkoa ambayo alisema wataendelea kuyatekeleza kadri ya maelekezo.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi akiwaonyesha wakazi wa Kata ya Kikuyu, jijini Dodoma orodha ya majina waliyohakikiwa kwa ajili ya kupatiwa viwanja vyao kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watumishi wakumbushwa maadili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi Umma na Utawala Bora), Mary Mwanjelwa, amewataka watumishi wa umma kuzingatia sheria na maadili ya kazi zao wanapowahudumia wananchi ili kuepuka migogoro.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa anazungumza na watumishi wa Kituo cha Afya cha Iyunga jijini hapa, alipokuwa anatoa msaada wa vifaa vya ujenzi pamoja na vituo vingine vya afya na baadhi ya shule za msingi.

Mwanjelwa ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, aliwataka wahudumu wa afya kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali kuwahudumia wagonjwa kwa upendo ili kuokoa maisha yao kwa kuwa kazi hiyo ni ya wito.

"Niwaombe wafanyakazi sekta ya afya kuweni na moyo wa huruma kwa wagonjwa wetu... Serikali inatambua changamoto mbalimbali mnazokumbana nazo mnapotoa huduma, lakini jitahidini kuvumilia na kutoa huduma kwa moyo kuokoa maisha ya watu," alisema Mwanjelwa.

Pia alitoa msaada wa vifaa katika Kituo cha Afya cha Nzovwe na baadhi ya shule za sekondari na msingi za Jiji la Mbeya ili kupunguza changamoto zinazoyakabili maeneo hayo.

Alitoa boksi 1,140 za Marumaru na mifuko 492 ya saruji, akisema saruji itatumika kwenye vituo vya afya Iyunga na Nzovwe na kila kituo kitapata mifuko 158 na mingine itagawiwa kwenye shule tano za pembezoni mwa mji na kila shule ikipata mifuko 25.

Akipokea msaada huo, Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, alimshukuru Naibu Waziri, akisema msaada huo utatumika kama ilivyokusudiwa kuboresha miundombinu ya afya na elimu.

Alisema Jiji la Mbeya bado linahitaji wadau kuendelea kujitoa kuhakikisha vituo vya afya, hospitali na zahanati zinapata vifaa kwa ajili ya kuwezesha miundombinu kuwa bora kwenye maeneo hayo.

"Misaada hii itatumika kama ilivyokusudiwa kwenye maeneo yote mawili ya afya na elimu, ila tunawaomba wadau wengine kuendelea kujitoa kwani bado kuna uhitaji mkubwa wa vifaa tiba na miundombinu ya baadhi ya shule zetu sio mizuri," alisema Kasusura.

Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwashilindi, alimuomba Mwanjelwa asichoke kuendelea kuchangia kwa kuwa uhitaji wa vifaa vya afya na elimu bado ni mkubwa.

Alisema wadau wengine wanatakiwa kujitokea kuchangia ili kuhakikisha changamoto za matundu ya vyoo kwa shule za msingi na sekondari inatatuliwa pamoja na ukosefu wa vifaa katika sekta ya afya.

## Wazazi, walezi wakumbushwa VVU, Ukimwi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imewataka wazazi na walezi wa watoto walio kwenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24, kuhakikisha wanazungumza nao juu ya masuala ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na magonjwa ya ngono.

Lengo la kufanya hivyo ni kusaidia kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya ugonjwa huo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati akizindua kipindi cha redio cha 'Ongea' ambacho kitakuwa kikirushwa kupitia redio za kijamii za mikoa minne ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe.


Alisema programu hiyo ambayo imeanzishwa na Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids) kwa kushirikana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), itasaidia kupunguza ongezeko la maambukizi kwa kundi rika hilo.

Alisema wakati mamlaka na taasisi hizo za serikali zikipambana, ni vema wazazi na walezi wakatambua umuhimu wa kuwalinda watoto kwa kuzungumza nao kwa kuwapa elimu ya VVU na magonjwa ya afya ya uzazi.

"Programu hii imekuja wakati mwafaka, hapa tumeelezwa kwamba kasi ya maambukizi mapya ni kubwa kutoka kati ya watu 72,000 walio na maambukizi mapya, asilimia 80 ni wasichana wenye umri wa miaka 15-24, ongezeko hili ni kubwa na Serikali pekee haiwezi," alisema.

Aidha, Chalamila aliyaomba mashirika hayo kuhakikisha yanaingiza programu zitakazowashirikisha watu wazima kwa kuwa wao wameonekana kuwa chanzo kikubwa cha maambukizi kwa watoto hao.

Ofisa Programu wa Unicef Kitengo cha Ukimwi na Mtoto, Alice Ijumba, alisema kipindi hicho kitakuwa kinarushwa kwa wiki mara moja kupitia kwenye redio zilizoainishwa.





# Bunge lajitosa bima ya afya kwa wote

Na Paul Mabeja, DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema serikali inatarajia katika bunge la mwaka ujao kupitisha sheria itakayosimamia utaratibu wa huduma ya bima ya afya kwa watu wote ili kuwezesha Watanzania kumudu gharama za matibabu.

Ndugai aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua maadhimisho ya Wiki ya Wanasayansi wa Maabara za Afya nchini (MeLSAT), yanayofanyika jijini hapa katika viwanja Nyerere Squre.

Alisema kupitia Bunge lake, baadhi ya wabunge wameshapelekwa katika nchi mbalimbali, zenye utaratibu wa huduma ya bima ya afya kwa wote ili kuweza kujifunza.

"Baadhi ya wabunge nilishawatuma wakaenda nchi mbalimbali kujifunza namna ya kuendesha utaratibu huu wengine walienda kujifunza nchini Uganda, wengine pia walienda Ghana... hii yote tu ni kujifunza ambavyo wenzetu wamefanikiwa katika hili," alisema Ndugai.

Alisema kutokana na umuhimu wa afya ni lazima wanachi wote wajiunge katika utararibu huo wa bima, ili kuwa na uhakika wa kupata matibabu kila wanapo kuwa wanasumbuliwa na magonjwa.

"Bima ya afya itakuwa mkombozi kwa wananchi wetu wote kuwa na uhakika wa matibabu wakati wote kama manavyofahamu kuwa magonjwa wakati mwingine yanakuja hata fedha mtu anakuwa hana ndani, lakini kupitia bima ya afya mtu atapata matibabu bila shida," alisema.

Alisema bima ya afya ndiyo mkombozi wa maskini na Watanzania wanyonge ambao utawawezesha kupata tiba kwani watakuwa na uwezo wa kumudu gharama za matibabu.

Awali, Rais wa Chama cha Wataalamu wa Maabara nchini, Yahya Mnung'a, alisema sekta ya maabara ndiyo eneo muhimu katika kuhakikisha upatikaji wa tiba unakuwa wa uhakika.

Alisema kama serikali haitawekeza katika usimamizi wa maabara ambazo zimekuwa zikitoa huduma za vipimo chini ya kiwango basi suala la matibau ya uhakika litakuwa kitendawili.

"Serikali ifanye uchunguzi wa mara kwa mara katika maabara zilizopo kwa kuwa wakati zinaanzishwa nyingi zilikuwa na vigezo lakini kadri muda unavyokwenda nyingi zinapoteza sifa," alisema Mnung'a.

Aidha, alisema lengo la maadhimisho ya wiki hiyo ni pamoja na kujenga uelewa kwa jamii juu ya huduma zitolewazo na wataalamu wa maabara nchini, kuhamasisha vijana kujiunga na fani hiyo kwani wengi wao wamekuwa wakiwaza zaidi kusomea udaktari pekee.



Msimamizi wa shamba la Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, Mariamu Fissoo, akiwapa maelezo kuhusu ufugaji wa samaki kinamama wajasiriamali kutoka Mkoa wa Mara, walipotembelea jana eneo la Zuzu, jijini Dodoma kujifunza elimu ya shamba darasa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yafunguka malengo endelevu

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Aldof Nduguru, amesema Serikali imefanikiwa kufikia baadhi ya malengo endelevu ya Dunia yaliyokusudiwa.

Kauli hiyo aliitoa jana kwenye mkutano wa wadau mbalimbali wa kutathmini malengo ya maendeleo endelevu ya millenium.

Nduguru alisema katika moja ya malengo ya maendeleo endelevu yaliyokusudiwa na Dunia, Serikali ya Tanzania imefankiwa kufikia baadhi yake.

Alitaja baadhi ya malengo ambayo Serikali imeweza kupiga hatua ni upande wa elimu kwa kuwa imeweza kuwafikia watoto wengi kwa sera yake ya elimu bure, ambayo imewezesha haki ya kupata elimu inafanikiwa.

Aliyataja mafanikio mengine ni eneo la afya serikali, ambapo imejitahidi kufikisha huduma za afya maeneo mbalimbali na huduma za vifaa tiba vinapatikana kwenye maeneo hayo.

Katika eneo hilo alisema serikali imejenga hospitali kubwa za wilaya na mikoa pamoja na kuajiri madaktari bingwa na wahudumu wengine wa afya.

Aliongeza mafanikio mengine ni kuzuia mfumuko wa bei pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara na majengo.

Aidha, alisema pamoja na mafanikio yaliyopatikana alitaja baadhi ya changamoto zilizojitokeza kuwa ni upungufu wa rasilimali fedha na watu.

Alisema lengo la mkutano huo ni kujadiliana kwa pamoja jinsi walivyotekeleza na kuwaonyesha wafadhili wa mapango huo jinsi ya mafanikio yaliyopatikana.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Asasi za Kiraia, Prisca Kowa, alishauri ukusanyaji wa taarifa za takwimu ndani ya Serikali kutoa taarifa hizo kwa wakati ili kuepuka upotoshaji wa baadhi wa watu.

Kowa alisema wizara zinazohusika na ukusaji takwimu hizo kushirikiana ili kufanikiwa zaidi.

Hata hivyo, alitaja baadhi ya changamoto wanazokumbana nazo ni upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati pamoja na ugumu wa kuzipata taarifa hizo wao wakiwa kama asasi za kiraia.

## Serikali yabeba wavuvi

Na Renatha Msungu, DODOMA

SERIKALI imekataa ombi la kufungia wavuvi katika ziwa Tanganyika ili kuacha samaki wakue, kutokana na kuwa wanategemea uvuvi zaidi kujiingizia kipato.

Ombi hilo limetolewa na mwakilishi kutoka Kigoma aliyetaka wavuvi watengewe mfuko wa kujikimu wakati wakisubiri samaki wakue ndani ya miezi mitatu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema kufunga shughuli ya uvuvi ni vigumu kwa sababu suala hilo inabidi wakae pamoja.

"Hatutaweza kulifunga Ziwa Tanganyika kwa sababu ni tegemezi kwa wakazi wa eneo hilo," alisema Ulega.

Alisema kinachofanyika hivi sasa ni kusimamia sheria ili wavuvi wavue kihalali na si kiharamu kutokana na kwamba wanafanya usimamizi wa hali ya huu.

Naibu Waziri alisema lengo lao ni kuona wanafanikiwa katika lile walilokusudia.

Akizungumzia suala la utafiti uliofanywa kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (Danida), alisema utafiti huo umeonyesha matunda mazuri.

Alifafanua zaidi kuwa, awali walikuwa wakivua bila kujua kama samaki wako wengine au la kutokana na kwamba bwawa hilo alijafanyiwa utafiti muda mrefu.

Naye Msimamizi wa Mradi huo, Dk. Ishmael Kimirei, alisema wameamua kudhamini utafiti huo kwa sababu lengo ni kujua kilichopo ndani ya ziwa.

Alisema wanashukuru utafiti huo umefanyika salama na kuleta matokeo mazuri ambayo yatawapa manufaa zaidi katika kuendelea kufanya utafiti mbalimbali.


Alisema mradi huo ulianza 2015 na utaishia mwaka huu na kuongeza kuwa umeleta matokeo mazuri.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Uvuvi Dk. Rashid Tamatama, alisema utafiti wa mwisho Ziwa Tanganyika ulifanyika 1995, hivyo wameona ni bora waufanye katika ziwa hilo.

Alifafanua zaidi kuwa, wamekuwa wakifanya utafiti Ziwa Victoria ambapo wafadhili wengi wamekuwa wakijitolea katika kufanya utafiti kwenye ziwa hilo.

Dk. Tamatama alisema wakitoka Ziwa Tanganyika wanatarajia kufanya utafiti Ziwa Nyasa ili kujua idadi ya samaki na kuona mabadiliko yakoje kulingana na tabianchi.

# HABARI ZANZIBAR





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Balozi wa Shirikisho la Jamhuri ya Brazil nchini Tanzania, Antonio Augusto Cesar, alipofika Ikulu Zanzibar kwa mazungumzo na kujitambulisha jana. **PICHA: IKULU**

## ZSTC yatakiwa kuimarisha kilimo cha karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Kusini Unguja, Hassan Khatib, amewashauri maofisa wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), kuwa karibu na wakulima wa karafuu ili kuwasaidia na kuliimarisha zaidi zao hilo.

Alisema utaratibu wa sasa wa kuendelea kujifungia ofisini kusubiri msimu wa kununua karafuu kutoka kwa wakulima uanze bila ya kuchukua juhudi ya kuwasaidia katika kulikuza zao hilo sio jambo zuri.

Alitoa ushauri huo katika mkutano wa wakulima wa zao la karafuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, ulioandaliwa na ZSTC kwa lengo la kuangalia maendeleo ya zao hilo kwa mwaka 2018/2019 katika Ukumbi wa Kituo cha Walimu Dunga.

Alisema uamuzi wa Shirika hilo kukutana na wakulima mara moja kwa mwaka, baada ya kumalizika msimu wa karafuu, haumsaidii sana mkulima katika kuimarisha na kuliendeleza zao hilo.

Aliwataka wakulima wa karafuu kwa upande wao kuthamini juhudi zinazochukuliwa na Wizara ya Kilimo za kupewa miche ya mikarafuu bila malipo kwa kuitunza na kuhakikisha wanafuatilia ukuaji wake ili lengo la kupewa miche hiyo liweze kufikiwa.

Aidha, aliwataka wananchi wa Mkoa Kusini kuangalia kilimo kingine cha biashara hasa pilipili hoho huku wakijua kwamba eneo kubwa la mkoa huo lina mawe na zao hilo linastawi katika maeneo hayo. Akitoa tathmini ya zao la karafuu kwa mwaka 2018/2019, Mkurugenzi wa Masoko wa ZSTC, Salum Abdalla, alisema msimu huo mavuno hayakuwa makubwa, lakini aliwataka wakulima wasivunjike moyo na matokeo hayo bali waendelee kuitunza mikarafuu na kufanya juhudi ya kupanda mipya.

Aliwaeleza wakulima wa zao hilo wa Mkoa Kusini Unguja kuwa ZSTC iliweka makisio ya kununua karafuu tani 3,000, lakini walinunua tani 195.16 na Pemba zilinunuliwa tani 161 na Unguja tani 34.

Alitoa wito kwa wakulima wa karafuu wanaochukua mikopo kwa ajili ya maandalizi ya kuchuma zao hilo wakati wa kuanza msimu kila mwaka kurejesha mikopo hiyo ili kujenga imani kwa shirika na waweze kukopeshwa katika msimu unaofuata.

Kwa upande wao, wakulima wa karafuu wa Mkoa Kusini Unguja, wamelishauri Shirika la ZSTC kusimamia ugawaji wa miche ya mikarafuu kwa wakulima na kwa wakati bila ya kufanya upendeleo ili kila anayestahiki kupata aweze kuipata.

Katika Mkutano huo Mkuu wa Mkoa alitoa kadi za usajili kwa wakulima wapya wa karafuu wa mkoa huo na kuwataka wakulima ambao bado hawajapata usajili kufanya utaratibu wa kupata ili maslahi yanayopatikana kwa wakulima waliopata usajili waweze kuyapata.

## Wafanyabiashara wapewa angalizo uingizaji bidhaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Hassan Khamis Hafidh, amesema kuwa changamoto zilizopo katika taasisi za viwango isiwe fursa kwa wafanyabiashara kuleta bidhaa zisizokuwa na viwango.

Hafidh aliyaeleza hayo katika kongamano la wafanyabiashara lililoandaliwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), lililofanyika Mazizini nje kidogo ya Mjini wa Zanzibar.

Alisema serikali inatambua kuwa ndani ya taasisi hiyo kuna changamoto mbalimbali ambazo kama serikali imekuwa ikizishughulikia kila hali inaporuhusu.

Alieleza kuwa kumekuwa na baadhi ya wafanyabiashara wanaonunua bidhaa zisizokuwa na viwango ambazo zinauzwa kwa bei rahisi na kuziingiza nchini kwa lengo la kutengeneza faida kubwa. "Hakuna nchi inayokosa changamoto na sisi tunajua kwamba katika taasisi hii kuna changamoto mbalimbali, lakini isitoe fursa kwa wafanyabiashara kuingiza bidhaa zisizokuwa na viwango,",alisema.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuhakikisha wanaingiza bidhaa zilizo bora na kushirikiana na taasisi hiyo ili kuona wanajenga Zanzibar yao.

Aidha, alisema kuwa wizara yake ipo macho katika kuhakikisha wafanyabiashara wenye tabia za kuingiza bidhaa mbovu na watakapomgundua mbali ya kulipia gharama ya kuziangamiza bali watamfutia kibali cha kufanyia biashara.

Alisema kuwa hatua hizo zimekuwa zikifanywa ili kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini zinakuwa na viwango. "Wafanyabiashara tunaowapenda ni wale rafiki kwa wananchi na wanaotambua kwamba biashara si kuwakomoa wananchi," alifahamisha. Aliwataka wafanyabiashara hao kutambua kwamba Zanzibar na Tanzania wanampango wa kuanzisha viwanda hivyo wanahitaji kuzalisha bidhaa zenye viwango.

Naye Mkurugenzi wa ZBS Khatib Mwadini, alisema mkutano huo unalenga kutambua changamoto zilizopo kwa wafanyabiashara ili kuzifanyia kazi.

Alieleza kuwa ni imani yake kwamba mambo yote yaliyojadiliwa kupitia kongamano hilo, ZBS kwa kushirikiana na serikali wataweza kuyafanyia kazi.

Kwa upande wao, wafanyabiashara walioshiriki katika kongamano hilo, waliiomba serikali kuwa na mpango mkakati wa kuendeleza kilimo hai Zanzibar.

## SMZ yamlilia Dk. Mengi kwa kuacha pengo sekta ya habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi imeelezea masikitiko yake makubwa kufuatia kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi na kusema ameacha pengo kubwa katika tasnia ya vyombo vya habari.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhunga, alisema Dk. Mengi atakumbukwa kwa mambo mengi mema ikiwa ni miongoni mwa wawekezaji wa mwanzo kuitumia fursa ya kuanzisha vyombo vya habari nchini.

Alisema hatua hiyo kwa kiasi kikubwa imesaidia uwekezaji katika sekta hiyo ikiwamo kuzalisha ajira kwa waandishi wa habari wanaomaliza elimu katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

"Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar natoa salamu zangu za masikitiko kufuatia kifo cha mfanyabiashara maarufu na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, ambaye ametumia muda wake mwingi katika kuwekeza sekta ya habari na kuzalisha ajira nchini," alisema.

Aliwataka waandishi wa habari na wawekezaji wengine kuiga mfano wa Mengi ambaye ametumia utajiri wake kwa ajili ya uwekezaji na kutoa ajira kwa watu wengine.

"Watu wengine ikiwamo matajiri waige mfano wa Mengi katika kutumia utajiri wake kwaajili ya kuwanufaisha watu wengine katika kuzalisha ajira," alisema. Naye Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Hassan Mitawi, alisema Baraza litamkumbuka Mengi kwa ushirikiano wake mkubwa kwa vyombo vyake vya habari ambavyo vimetoa mchango mkubwa katika uhuru wa vyombo vya habari.

Alisema ni wakati waandishi wa habari kukumbuka mchango wa Mwenyekiti huyo wa IPP ambaye alisaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha taaluma ya uandishi wa habari nchini.

Alivitaja baadhi ya vyombo vya habari vilivyoanzishwa na kiongozi huyo mapema ni Televisheni ya ITV, Redio One pamoja na magazeti ya Nipashe na yale ya Kiingereza ya Guardian.

"Dk. Mengi tutamkumbuka kutokana na mchango wake mkubwa katika kuimarisha taaluma ya uandishi wa habari nchini sambamba na kuanzisha vyombo vya habari ambayo vilisaidia kutoa ajira kwa wananchi wetu wengi nchini." alisema.

Mkurugenzi wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema taaluma ya uandishi wa habari imepata pigo kubwa kufuatia kifo cha marehemu Mengi ambaye ni mwasisi wa vyombo vya habari nchini.

Hata hivyo, alisema njia pekee ya kumkumbuka Mengi ni kwa waandishi wa habari kuendelea kutekeleza majukumu ya taaluma hiyo pamoja na kufauata maadili yanayoongoza fani hiyo.

"Njia pekee ya kumkumbuka na kuenzi kazi nzuri iliyofanywa na Mengi ni kutekeleza na kuwajibika kwa waandishi wa habari na kufuata maadili yanayoongoza fani hiyo,' 'alisema.

# Hivi ndivyo ufisadi miradi ya maji unavyofanyika

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

WIZARA ya Maji imefichua jinsi makandarasi wanavyotafuna mabilioni ya shilingi yanayotolewa na Serikali kutekeleza miradi ya maji wakishirikiana na baadhi ya watendaji wa wizara.

Akijibu hoja mbalimbali wabunge wakati wa kuhitimisha mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Naibu Waziri wa Maji, Juma Aweso, alisema upigaji wa mabilioni ya miradi ya maji umekuwa ukifanyika kwa ushirikiano baina ya baadhi ya watendaji wa wizara na wanaopewa zabuni za kutekeleza miradi hiyo.

Alisema alifanya ziara Mbeya Vijijini na kupewa taarifa na mhandisi wa maji, lakini naye alikuwa na taarifa yake aliyoiandaa.

Alisema baada ya kulipa taarifa hiyo ya mhandisi, alimtaka ampeleke mradi wa Galijembe ingawa katika taarifa yake haukuwapo.

"Mhandisi ananiambia kuwa kule ambapo unataka nikupeleke, kuna miinuko mikubwa utachoka. Nikamwambia 'hapana, sisi tumekuja kufanya kazi, tupeleke mradi wa Garijembe'," Awesso alisema.

Aliongeza kuwa kulikuwa na mvutano mkubwa kabla ya kwenda kwenye mradi huo na kwamba baada ya

kwenda walikuta mradi wa zaidi ya Sh. milioni 290, mkandarasi alikuwa ameshapewa Sh. milioni 260 na hayupo eneo la mradi kwa miaka mitatu.

Alisema alipoulizwa mhandisi alipo, mkandarasi alijibu kuwa ni msumbufu na hata alipoandikiwa barua, hafiki kwenye mradi.

Hata hivyo, alisema alipotoa agizo, afike siku iliyofuatao, mkandarasi alifika kwenye mradi huo.

"Alipoulizwa unawezaje kulipwa fedha za maji ilhali hujatekeleza? Mkandarasi alinijibu 'Mheshimiwa Waziri, tusipoteze muda, nataka kikao chako kiwe kifupi. Mimi fedha tumelipwa lakini tumegawana na mhandisi wako wa maji," alisema.

"Kama ninalipwa 'certificate' ya Sh. milioni 20, Sh. milioni 10 yake na Sh. milioni 10 yangu," alisema.

Alitolea mfano wa mradi mwingine wa Shinyanga Vijijini katika mradi wa Mwakitolio wa zaidi ya Sh. bilioni 1.4 na kwamba fedha zote zimelipwa, lakini maji hayajapanda hata kwenye tanki.

Awesso alisema baada ya kuulizwa, mhandisi alijibu kuwa hajawahi kuona wanakijiji wachawi kama wa kijiji hicho na kwamba wametandika mabomba lakini usiku yanapaa kama Bombardier.

Alisema hawako tayari kuwaona wahandisi kama hao katika wizara hiyo na kwamba waliwabeba na hadi sasa wanaendelea na kesi mahakamani.

Alisema baada ya kuona changamoto hiyo, Wizara ya Maji iliunda kamati ya watu 10 ikiongozwa na Prof. Tolly Mbwete kukagua miradi yote ya maji.

Alisema baada ya kukagua, kamati hiyo ilikuja na changamoto 17 na kutoa mapendezo 50 kutatua matatizo hayo ili kuhakikisha maji yanapatikana nchini.

Alisema moja ya mapendekezo ya kamati hiyo ni kuanzishwa kwa wakala wa maji.

"Wahandisi wa maji 'we will meet again' (tutakutana tena). Nawaambia sisi tutakutana na wahandisi.

Kwa kuwa mmetupa rungu, tunawaambia tutawashughulikia katika kuhakikisha tunaleta nidhamu katika wizara yetu ya maji ili tulete matokeo chanya," alisema.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati), akiwaonyesha waandishi wa habari kitambulisho chake cha Taifa wakati akizungumza nao baada ya kusajili laini yake ya simu kwa alama za vidole jana katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma. **PICHA:OFISI ZA BUNGE**

## Stendi ya mabasi yajengwa kuongeza mapato h/mashauri

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, imezindua ujenzi wa stendi mpya ya kisasa katika eneo la Katumba ambayo itasaidia kuongeza mapato katika halmashauri hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, alisema kuwa ujenzi huo wa stendi ni fursa kubwa kwani unatarajia utakuwa ukiingiza Sh.bilioni 1.2 kwa mwaka kutokana na tozo zitakazopatikana baada ya mabasi kutozwa, watu kulipa kiingilio pamoja na vyumba vya biashara vitakavyokuwapo.

Wangabo alisema ujenzi huo umezinduliwa jana na utachukua miezi saba na kampuni ya ujenzi ya Sumry Enteprisess itafanya kazi hiyo kwa gharama ya Sh. tano.

Alisema kuwa fedha hizo zitatokana na makusanyo ya ndani ya halmashauri hiyo pamoja na serikali kuu ambapo ujenzi ukikamilika unatarajia kuongeza pato la halmashauri hiyo na serikali kwa ujumla.

Mkuu huyo wa mkoa alisema kuwa kuna mipango kabambe ya kuufanya mji wa Sumbawanga kuwa wa kisasa, ndiyo maana inajengwa miradi ya maendeleo ya kisasa itakayo leta hadhi katika Manispaa ya Sumbawanga na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla.

Awali akizungumza katika sherehe hizo za uzinduzi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Jacob Mtalitinya, alisema kuwa kujengwa kwa mradi huo utakuwa ni fursa kwa vijana wa mji wa Sumbawanga na mkoa wa Rukwa kwa ujumla kwani watapata ajira.

Alisema hizo ni jitihada za serikali kupitia agizo la rais John Magufuli katika kuhakikisha kuwa inaongeza mapato na ajira kwa vijana kinachotakiwa ni kuiunga mkono katika kutekeleza miradi hiyo ambayo italeta tija kwa wakazi wa Manispaa hiyo na mkoa wa Rukwa.

## Pinda mgeni rasmi kongamano biashara

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kongamano la kukuza ushirikiano wa kibiashara na utamaduni kati ya Tanzania na China.

Kongamano hilo ambalo pia linakusudia kukuza uchumi kati ya nchi hizo mbili, ambalo litafanyika kesho jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali ya Tanzania, wanadiplomasia, wafanyabiashara kutoka China na ujumbe wa kampuni ya China Kweichow Moutai Distlley ukiongozwa na mkurugenzi wa kampuni hiyo, Wang Yan.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na mwakilishi wa matukio wa kampuni ya China Moutai Group, Charles Wang, alipokuwa akizungumza na waandishi kutoka vyombo mbalimbali vya habari.

"Tumemwalika Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda katika kongamano hilo la kukuza ushirikiano na kukuza masoko ya bidhaa za kampuni yetu ambazo tunataka kuzifanya nchini," alisema Wang.

Alisema kupitia kinywaji chao kiitwacho Kweichow Moutai, wana uhakika watafanikiwa kukuza ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi hizo mbili na mataifa mengine kupitia mkakati uitwao 'Belt and Road Initiative'.

Wang alifafanua kuwa kupitia kongamano hilo, mkakati huo pia utagusa kuimarisha mambo yanayohusu utalii kati ya China na Tanzania.

China Moutai Group ni moja ya kampuni kubwa nchini ambayo imekuwa ikitengeneza bidhaa bora ambazo zinatamba katika masoko mbalimbali ya kimataifa duniani kikiwamo kinywaji cha Kweichow Moutai," alisema.

Alisema kimeanza kuingia katika masoko ya Afrika kupitia mkakati wa 'Belt and Road Initiative' wenye lengo la kukuza uchumi na kuunganisha wananchi kutoka Bara la Afrika na Asia.

## Marekani, China kujadiliana kuhusu ushuru

**WASHINGTON,** Marekani

CHINA inaeleza kwamba wapatanishi wake wanajiandaa kusafiri kuelekea Marekani kwa duru nyingine ya mazungumzo ya biashara.

Hatua hiyo imefikia baada ya Rais wa Marekani, Donald Trump kutishia kuongeza ushuru kwa bidhaa za China zenye thamani ya mabilioni ya dola, baada ya kulalamikia kuwa utaratibu wa majadiliano unachukua muda mrefu.

Matamshi ya Rais Trump kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter kuhusu kuweka ushuru mpya kwa China yalisababisha masoko ya Asia na Marekani kuwa na wakati mgumu Jumatatu na iliongeza hofu juu ya idadi ya mashauriano ya biashara kati ya nchi hizo mbili.

Licha ya soko kushuka vyombo rasmi vya habari China vilikuwa kimya juu ya matamshi ya Trump.

Hata hivyo, saa kadhaa baadae Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje China, Geng Shuang, aliwaambia waandishi wa habari kuwa China inajaribu kupata taarifa zaidi kuhusu matamshi ya RaisTrump kuhusiana na ushuru mpya, lakini alieleza kwamba timu ya mashauriano ya Beijing bado inajiandaa kusafiri kwenda nchini Marekani kwa mazungumzo hayo wiki hii. **DW**

## Ndugu wa Bouteflika, maafisa wawili waswekwa jela

**ALGERS,** Algeria

NDUGU wa aliyekuwa Rais wa Algeria, Abdelaziz Bouteflika, maafisa wake wa karibu wa zamani wanaendelea kusakamwa na vyombo vya dola nchini humo.

Said Bouteflika, mdogo wa Bouteflika, amewekwa kizuizini na Jaji wa mahakama ya kijeshi siku ya Jumapili (Mei 5). Wakuu wawili wa zamani wa idara ya upelelezi waliokamatwa Jumamosi pia wamewekwa jela.

Picha za watu hao zilioneshwa kwenye televisheni ya serikali Jumapili mchana. Saïd Bouteflika, ndugu wa Bouteflika, Mohamed Médiene, mkuu wa zamani wa idara ya upelelezi, na Athmane Tartag, ambaye alichukuwa nafasi yake hadi Abdelaziz Bouteflika alipotimuliwa madarakani, wote wanazuliwa na utawala mpya nchini Algeria.

Jaji wa mahakama ya kijeshi aliamuru watu hao wawekwe rumande.

Watu hao wanashutumiwa kula njama za kuipindua serikali na kuhatarisha usalama wa uongozi wa jeshi, Mashtaka yanayofanana na yale yaliyotolewa na Mkuu wa jeshi, Ahmed Gaid Salah wakati wa hotuba zake alizozitoa hivi karibuni. **RFI**

# Palestina, Israel hatimaye wakubaliana kusitisha vita

**JERUSALEM,** Israel

MAAFISA katika Ukanda wa Gaza, wamesema viongozi wa Palestina wamekubaliana kusitishwa kwa mapigano na Israel siku ya Jumatatu.

Hata hivyo, Msemaji wa Israel amekataa kutoa kauli yoyote kuhusu makubaliano hayo, lakini hakujakuwa na mashambulizi yoyote ya roketi.

Maafisa kutoka kundi la Hamas na Islamic Jihad ambao hawakutaka kutambulishwa walisema Misri ndiyo iliyosimamia makubaliano hayo ya kusitishwa mapigano.

Afisa mmoja wa Misri amethibitisha hilo ingawa yeye naye hakutaka kutambulishwa.

Makubaliano hayo yamefikiwa baada ya kutokea kwa mapigano makali kati ya wanamgambo wa Israel na Palestina tangu vita vya mwaka 2014.

**Mashambulizi yalianza Jumamosi kutoka Gaza na Israel ikarusha makombora ya kujibu, mashambulizi hayo yakaendelea hadi juzi.**

Jeshi la Israel mapema Jumatatu limeondoa vizuwizi vyote vilivyokuwa vimewekwa karibu na eneo la Gaza wakati wa machafuko hayo.

Uongozi wa jeshi hilo umewashauri raia kuendelea na shughuli zao kama kawaida. Shule katika eneo hilo zimekubaliwa kuendelea na masomo ingawa baadhi zimefungwa kutokana na roketi 700 zilizoishambulia Israel.

Mashambulizi yalianza Jumamosi kutoka Gaza na Israel ikarusha makombora ya kujibu, mashambulizi hayo yakaendelea hadi juzi.

Wapalestina 23 wakiwamo wanamgambo tisa waliuawa, upande wa Israel watu wanne waliuawa huku watatu kati yao wakiwa raia wa Israel.

Rais wa Marekani, Donald Trump jana aliihakikishia Israel kwamba nchi yake inaiunga mkono katika mashambulizi wanayoyafanya dhidi ya Palestina.

Machafuko yalianza baada ya waandamanaji wa Palestina kuuawa Ijumaa. Mashambulizi hayo yalifanyika wakati Israel ikiwa inajiandaa kuadhimisha siku ya uhuru wiki hii huku upande wa Gaza Waislamu wakiwa wameanza kufunga katika mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Maafisa wa Palestina katika ukanda wa Gaza wameituhumu Israel kwa kutochukua hatua za kutopunguza vizingiti vya kupita kwa bidhaa zake kama ilivyoahidiwa katika mikataba iliyopita.

Israel na wanamgambo wa Palestina katika ukanda wa Gaza wamepigana vita tangu mwaka 2008. **DW**



Wanachama wa Chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) Afrika Kusini, kinachoongozwa na Julius Malema, wakiwa kwenye kampeni katika uwanja wa Orlando mjini Soweto, nchi hiyo leo inapiga kura kumchagua Rais mpya. **PICHA: AFP**

# Julius Malema atumia hoja ya umaskini kuvutia wapigakura

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

WAKATI Afrika Kusini ikielekea kwenye uchaguzi mkuu, kiongozi wa chama cha upinzani cha Economic Freedom Fighters (EFF), Julius Malema, ametumia hoja ya udhaifu wa chama tawala cha ANC kuvutia wapigakura kuchagua chama chake.

Kampeni za lala salama zinaendelea nchini humo kuelekea uchaguzi unaotarajiwa kufanyika leo.

Katika kampeni za uchaguzi huo, Malema, kiongozi wa EFF amekuwa akiwashawishi wananchi kukichagua chama chake akitumia hoja ya udhaifu wa ANC kinachoongozwa na Rais Cyril Ramaphosa kushindwa kuondoa umasikini na kuwakumbatia wazungu.

Kwa muda wa saa mbili wafuasi wake walikuwa wamebeba mabango yenye kauli mbiu zenye ujumbe wa kimageuzi, muziki mkubwa na hotuba za maandalizi katika uwanja wa michezo katika kitongoji cha Alexandra mjini Johannesburg.

Muda mfupi baadaye Malema anatokea akiwa na gari la kijerumani na kupita jukwaani akipokea heshima.

Umati wa watu unasikika ukisema "Songa mbele kuelekea ushindi 2019-mbele", ikiwa ni siku kadhaa kabla ya uchaguzi kufanyika.

Malema ambaye amejitengenezea utambulisho wake kama Amiri Jeshi Mkuu wa wapigania uhuru wa uchumi katika chama chake cha EFF alikuwa amevalia sare ya chama hicho na kofia nyekundu huku akiwa amezungukwa na kundi la walinzi wake wanaojulikana kama watetezi wa mapinduzi.

Katika mkutano wake huko Alexandra, Malema aliwaambia wafuasi wake ni lazima waichukue ardhi kutoka mikononi mwa wazungu na kuwapa watu wa eneo hilo ili wagawane utajiri wa nchi hiyo.

"Kuna fedha nyingi hapa Afrika kusini ambazo zinapotezwa na wanasiasa. Hebu tuokoe pesa. Mnataka kuzifanyia nini? Ninataka kuwapa akina bibi, nataka kuwapa watoto fedha kutoka katika mifuko ya wanasiasa," alisema Malema. **DW**

# Kusajili zaidi ya laini moja kwa masharti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA Job Ndugai, jana amezindua usajili wa laini za simu kwa alama za vidole, huku Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ikisema mtu yeyote atakayetaka kusajili laini zaidi ya moja kwa mtoa huduma mmoja, ni lazima aeleze sababu.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, alisema pamoja na kuwa hawajazuia mtu mmoja kusajili laini zaidi ya moja kwa mtoa huduma mmoja, lakini ni lazima mtu huyo aeleze sababu mahsusi za kuwa na laini zaidi ya moja.

Alisema kila Mtanzania anatakiwa kusajili kwa alama za vidole laini moja ya simu kwa mtoa huduma mmoja.

"Lakini kama mtu anataka kuwa na laini zaidi ya moja kwenye kampuni ya simu moja, huzuiliwi ni lazima useme laini hiyo ni ya nini," alibainisha.

Kadhalika, alisema hivi karibuni wamemkamata mtu mmoja ana laini za simu 600.

"Kwa akili ya kawaida unaweza kujiuliza anataka kufanyia nini. Tunasema kuna watu milioni 40 wanalaini za simu, huku mmoja ana laini 600 kwa takwimu kama hizi hatuwezi kupanga mipango ya maendeleo," alisema.

Akizindua usajili huo, Ndugai aliwataka Watanzania kujitokeza kusajili laini za simu kwa alama za vidole kwa ajili ya usalama na matumizi bora ya simu.

"Ili kuwa na usalama na matumizi bora ya matumizi ya simu, ni vyema Watanzania wakasajili laini zao na pia wakajitokeza kujiandikisha kwenye uraia,"alisema.

Aidha, kutokana na hoja iliyoibuliwa kuwa Wabunge wa Zanzibar wanashindwa kusajili laini za simu kwa alama za vidole kwa kuwa na kitambulisho cha Mkazi Zanzibar, Spika huyo alisema hakuna mbunge yeyote ambaye atashindwa kusajiliwa laini zake.

Awali, akizungumza katika uzinduzi huo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, alisema lengo la usajili huo ni kujiepusha na uhalifu unaofanywa kupitia simu za mkononi.

Alisema kumekuwa na mwitikio mzuri wa Watanzania wa kusajili laini zao za simu kwa alama za vidole ambao ulianza kabla ya Mei Mosi mwaka huu na kwamba Septemba 30 mwaka huu, serikali itafanya tathmini ya usajili huo.

Hata hivyo, kuhusu wanafunzi chini ya miaka 18 kusajili laini zao, Nditiye alisema majukumu ya wanafunzi ni kusoma na kama watakuwa wanatumia simu basi uwe ni kwa udhamini wa mzazi.

"Kijana kuanzia miaka 18 ndiye anayestahili kupata kitambulisho cha uraia na ndiye anayeweza kumiliki na kutumia simu, chini ya hapo iwe kwa udhamini wa mzazi," alisema.



Wasamaria wema wakisaidia kulisukuma gari lililokwama katika eneo la Goba Tegeta A, kutokana na mvua iliyonyesha jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Muswada sheria bima ya afya Kwa wote waja

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote unatarajiwa kuwasilishwa bungeni Septemba mwaka huu.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alitangaza neema hiyo jana bungeni alipowasilisha hotuba kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema serikali inaendelea na maandalizi ya kukamilisha muswada huo, akibainisha kuwa mkutano wa kuelimisha wabunge kuhusu mkakati wa ugharamiaji wa huduma za afya pamoja na mkakati wa kuboresha mfumo wa Bima ya Afya ya Taifa ulifanyika Januari mwaka huu.

"Wizara ilifanikisha ziara ya wabunge 19 nchini Rwanda na Ghana Desemba 2018, lengo likiwa ni kupata uzoefu wa namna nchi mbalimbali zilivyoweza kutekeleza mfumo wa bima Moja kwa watu wote.

"Katika ziara hiyo, wabunge walijifunza juu ya umuhimu wa kuwa na mfumo imara wa bima ya afya ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kugharamia huduma za afya," alisema.

Alisema kufuatia ziara hiyo, wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu wa Bunge iliandaa taarifa yenye mambo muhimu waliyojifunza nchini Rwanda na Ghana.

Alisema taarifa hiyo imetumika katika maandalizi ya waraka wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Bima ya Afya unaojadiliwa serikalini.

**AJIRA 2,700**

Katika hatua nyingine, Mwalimu alisema katika mwaka huu wa fedha, wizara yake imewasilisha maombi ya ajira mpya 12,775 na inatarajia kibali hicho kitatolewa kabla ya mwaka wa fedha kuisha.

Hata hiyo, mwaka wa fedha 2018/19 umebakisha siku 53 kufika ukomo.

Waziri huyo pia alisema katika mwaka huu wa fedha, nyumba 318 zimejengwa kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa sekta ya afya.

# Vipaumbele 15 Wizara ya Afya kwa 2019/20

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imebainisha vipaumbele 15 vya bajeti yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Ummy Mwalimu, alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo ili kuwakinga watoto chini ya mwaka mmoja dhidi ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Vingine ni kuimarisha hali ya lishe na usafi wa mazingira, upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kuboresha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto chini ya miaka mitano na kuendelea kupunguza pengo kati ya mahitaji halisi ya watumishi wa afya na idadi ya watumishi waliopo vituoni.

Mwalimu alisema vipaumbele vingine ni kuboresha miundombinu na utoaji huduma katika hospitali za rufaa za mikoa, kuimarisha huduma za kibingwa katika hospitali za taifa, maalum pamoja na kuendelea na utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuimarisha na kupunguza maambukizo ya Ukimwi, kifua kikuu na malaria.

Vingine alisema ni kuendelea kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwamo saratani, kisukari, shinikizo la damu na magonjwa ya moyo, kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa katika hospitali za rufaa za mikoa na kukamilisha mchakato wa maandalizi ya kutunga Sheria ya Bima ya Afya itakayomtaka kila mwananchi kuwa na Bima ya Afya ikiwa ni mkakati mahusisi wa kufikia lengo la taifa la afya kwa wote ifikapo mwaka 2030.

Vingine ni kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa wazee na watoto walio katika mazingira hatarishi, kuimarisha usimamizi na uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali, uratibu wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto 2017/18-2021/22 na kutoa huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa katika familia.

Ili kutekeleza majukumu hayo, Mwalimu aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 990.689 kwa ajili ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Kati yake, Sh. bilioni 443.792 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 546.892 ni za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA PASSPORT



**YOHANA SHIJA MASALU**

Mtajwa hapo juu anatangaza kupotelewa na passport (Hati ya kusafiria) Yenye namba **AB557801** iliyotolewa na Jamhuri ya muungano wa Tanzania Kupitia idara ya uhamiaji PCO Dar es Salaam ,imetolewa Tarehe 10 Januari 2013 na inaisha muda Wake Tarehe 10 januari 2023 Kwa atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kwa kumb - **MZN/RB/3592/2019.**

215216402

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SALEH HUSSEIN SALEH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER** yenye namba za usajili **T 905 ASD,** Chassis namba **LJ71007822,** Engine namba **0189476.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/5574/2019.**

215245802

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ahmed Mohamed Khalid** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T423 DFR** aina ya **PREMIO,** yenye chasis namba **ZZT2450006215** na engine namba **1ZZFE5632149.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**KJN/RB/156/2019**

115215702

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA RUVUMA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 21/2019**

**GEOFREY SAMWEL MILINGA .................. MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **WILNERLY DAUD KAPINGA**
2. **EDGAR JOSEPHAT MHAGAMA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu Maombi wa kwanza hapo juu unataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako. Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe 9/5/2019 saa 2:30 asubuhi. Kumbuka pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili bila kujali uwepo wako..

Imetolewa leo nami na muhuri wa baraza hili leo tarehe 6/5/2019

215216802

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.30 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late RAHEL K. MUTOKA**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by JEREMIA A MSAUKA**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections (if any) to the grant should be filed on or before 8th /05/2019.

Dated at Dodoma this ….15th /04/2019

Resident Magistrate
DODOMA

215216502

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Elias Joram Kitundu** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye usajili wa namba **T 295 DRN** aina ya **SANLG.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**KAH/RB/02/2019**

115215602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILAINO.**

Simu: +255 262324455.
Fax: +255 26232233.
Barua Pepe ps@mo.go.tz.
Tovuti: www:mwtc.go.tz.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
07/05/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATATU tarehe 13/05/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka ARUSHA kuelekea MOSHI gari hilo lenye namba za usajili: **T188APK,T741 CPB,T985 ABJ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 17**
   **Upana** – **mita 3**
   **Kimo** – **mita 3.2**
3. Njia itakayotumika **ARUSHA hadi MOSHI kupitia MOSHI ARUSHA** ROAD gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215216302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MIKESE**

**Usimamizi wa mirathi No; 03/2019**

**Ombi la MORISI EMANUEL IBRAHIM**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi**
**marehemu ANTON EMANUEL IBRAHIM**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 30/04/2019.

2152162O2


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# POGBA SASA KULAZIMISHA UHAMISHO MAN UNITED

**MANCHSTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, anataka kuondoka pale Old Trafford kipindi cha majira ya joto na atalazimisha uhamisho hata kama klabu hiyo itakataa kumuuza, kwa mujibu wa ESPN FC.

Pogba, ambaye alijiunga na Man United akitokea Juventus kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 100 miaka mitatu iliyopita, mkataba wake wa sasa unamalizika Juni 2021, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi.

Hata hivyo, chanzo kimoja kimeliambia ESPN FC kwamba, kwa kuwa United imeshindwa kufuzu kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, Pogba anataka kulazimisha kuondoka.

Wakala wa mchezaji huyo, Mino Raiola, amenukuliwa na Gazeti la Daily Mail akisema kwamba, kwa Pogba chochote kinaweza kutokea wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Hata hivyo, Man United yenyewe imenukuliwa mara kadhaa kwamba mchezaji huyo hatauzwa licha ya kutakiwa kwa nguvu zote na Klabu ya Real Madrid ya Hispania.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, Machi mwaka huu alinukuliwa akisema kwamba, kucheza katika Klabu ya Real Madrid ni moja ya ndoto zake.

Barcelona walijaribu kutaka kumsajili Pogba kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini ofisa mtendaji wa Man United alitibua mpango huo dakika za mwisho.

# Manchester City yanusa ubingwa EPL

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City wanajua kwamba watatwaa taji la Ligi Kuu ya England iwapo watashinda mechi ya siku ya mwisho kufuatia Vincent Kompany kupiga mkwaju kutoka mbali ambao kipa wa Leicester City hakuuona na kuipa ushindi wa bao 1-0.

Huku zikiwa zimesalia dakika 20, timu zote zilikuwa hazijaona lango la mwingine katika Uwanja wa Etihad huku mabingwa hao watetezi wakihitaji msukumo katika mechi ambayo ushindi pekee ungewahakikishia kupanda juu ya Liverpool katika kilele cha jedwali la ligi.

Hata hivyo, walipata bao lao la pekee kutoka kwa mtu ambaye hawakumtarajia ambaye alipiga mkwaju kutoka maguu 25- na kipa wa Leicester City hakuutarajia.

Ushindi huu wa City unamaanisha kwamba wanapanda hadi juu ya jedwali na kuipiku Liverpool kwa uongozi wa pointi moja huku wakijiandaa kucheza mechi yao ya mwisho siku ya Jumapili, wakati Pep Guardiola ataelekea Brighton huku Liverpool ikicheza dhidi ya Wolveharmpton.

Baada ya kujikwamua kupata ushindi mwembamba nyumbani, si rahisi kwamba City watalegeza kamba huku shindano hilo la kutafuta mshindi wa ligi likifikia kilele chake.

Lakini kwa kipindi cha muda mrefu ilionekana wazi kwamba Liverpool itasalia katika kilele hadi wikiendi.

Ikifundishwa na aliyekuwa kocha wa Liverpool, Brendan Rodgers, ambaye alikaribia kushinda taji hilo katika Uwanja wa Anfield 2014, safu ya ulinzi ya Leicester ilikuwa ngumu kupitika huku wakitisha katika safu ya ushambuliaji.





# Godin atangaza kuondoka Atletico

**MADRID,** Hispania

DIEGO Godin ametangaza kuwa ataondoka Atletico Madrid wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu, na tetesi za kujiunga na Inter zikizidi kuvuma.

Nahodha huyo wa klabu hiyo, Godin, alijiunga na Atletico akitokea Villarreal mwaka 2010 na alikuwa mchezaji muhimu wakati wakitwaa ubingwa wa La Liga msimu wa 2013-14, lakini amethibitisha kwa hisia taarifa hizo katika mkutano na waandishi wa habari Jumanne kwamba muda wake hapo sasa unaelekea mwishoni.

Beki huyo wa kati mwenye umri wa miaka 33, aliichezea Atletico kwenye mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakifungwa na Real Madrid mwaka 2014 na 2016, ingawa alifanya hivyo pia wakishinda ubingwa wa Europa League mara mbili.

"Ninaondoka Atletico Madrid. Hizi ni siku zangu za mwisho hapa," alisema Godin, ambaye anatarajiwa kusaini mkataba na miamba ya Serie A, Inter.

"Atleti imekuwa familia yangu, klabu yangu na nyumbani kwangu, na ni vigumu kusema kwa heri.

"Hii imekuwa miaka ya kushangaza, nimefurahia sana na kukua kama mchezaji, lakini juu ya yote kama mtu.

"Ningependa kucheza hapa hadi nitakapofikisha miaka 40, lakini hilo ni haliwezekani. Hatukufikia makubaliano, hivyo nimeamua kuondoka, hakuna kingine zaidi."

## HABARI MICHEZO

# Emery: Akili yangu sasa ni Europa Ligi



**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, amesema kwa sasa hesabu zao zinahamia kwenye Ligi ya Europa baada ya kupoteza matumaini ya kumaliza Ligi Kuu England wakiwa kwenye nne bora baada ya sare ya jana dhidi ya Brighton.

'Washika Bunduki' hao wameachwa kwa jumla ya pointi tatu na kikosi cha Tottenham ambacho kipo nafasi ya nne kikiwa na mchezo mmoja wa kucheza ila watatakiwa washinde zaidi ya mabao nane kwenye mchezo huo huku wakiombea Tottenham wapoteze ili kuweza kuwashusha.

"Tunajua hali inazidi kuwa ngumu kwetu kutokana na mambo yalivyo ila hesabu zetu ni kuona tunashinda Ligi ya Europa.

"Tuna nafasi huku kwenye Ligi ya Europa kufanya jambo zuri na la muhimu kwa ajili ya timu, hivyo lazima tupambane kupata matokeo," alisema kocha huyo ambaye ameshinda taji la Ligi ya Europa mara tatu akiwa na Sevilla.

"Kwa uhakika ni kwamba, tunatakiwa kupigana haswa ili kutwaa taji la Ligi ya Europa, na naamini kwa kikosi changu kinaweza kufanya hivyo."

# DE LIGT HANA MPANGO WA KUTUA MAN UNITED



**AMSTERDAM,** Uholanzi

WAKATI Manchester United inampango wa kutaka kumsajili nahodha wa Ajax, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 19, yeye mwenyewe hana mpango wa kutua hapo kwenye Uwanja wa Old Trafford.

De Ligt, ambaye alicheza dhidi ya united wakati akiwa na umri wa miaka 17 kwenye Kombe la Ligi ya Europa mwaka 2017, amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa za Ulaya msimu huu.

De Ligt amekuwa na kiwango kizuri zaidi msimu huu huku akiiongoza Ajax kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na leo Jumatano watacheza dhidi ya Tottenham Hotspurs kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali.

Kinda huyo amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Barcelona, Juventus, Bayern Munich na Liverpool katika miezi ya hivi karibuni. Lakini Man United imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo ili kuimarisha kikosi chake kwenye kipindi cha majira ya joto.

Lakini kwa mujibu wa Gazeti la Daily Star, De Ligt amebainisha kwamba hana mpango wa kujiunga na Manchester.

Gazeti hilo limebainisha kwamba uamuzi wa 'dogo' huyo kutokuwa na nia ya kutua Man United aliufanya kabla hata 'Mashetani Wekundu' hao hawajashindwa rasmi kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.



# Guardiola kocha bora wa Aprili

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ametajwa kuwa kocha bora wa Aprili kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kuiongoza timu yake kushinda mechi tano mfululizo.

Guardiola pia aliiongaza timu yake kuruhusu bao mara moja tu na kuifanya timu hiyo kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England msimu huu. Ni mara ya pili kwa Guardiola kutwaa tuzo hiyo katika kazi yake ya ukocha msimu huu baada ya kuitwaa pia Februari.

Na hii ni mara yake ya tano kushinda tuzo hiyo, na sasa amemkaribia Mhispania mwenzake, Rafa Benitez ambaye ametwaa tuzo hiyo mara sita.

City tayari imeshashinda mara saba mfululizo mechi za Ligi Kuu ya England wakati ikielekea Aprili na ilianza na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Cardiff.

Na ilifuatiwa na ushindi dhidi ya Crystal Palace na Tottenham, wakati katikati ya wiki ilishinda dhidi ya majirani zao wa jiji moja, Manchester.

# DONDOO Z... SOKA MAGAZETI ...AYA




# KOMPANY: NIMEIFUNGIA CITY BAO LA MAZOEZINI

## ●●● Badala ya ubora, fanya kuwa bora, hilo ni bora kwangu...

**MANCHESTER,** England

VINCENT Kompany amefunguka kuwa, kwenye mazoezi hufunga mabao kwa mkwaju wa mbali kama ambalo amefunga wakati Manchester City ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Leicester City.

**Bao hilo la kwanza la msimu kwa Kompany kwenye Ligi Kuu England, limeiwezesha City kurejea kileleni mwa msimamo wa EPL, huku ikiiacha Liverpool kwa pointi moja na hivyo kufanya bingwa sasa kuamuliwa katika mechi za mwisho Jumapili.**

Katika dakika ya 70 kwenye Uwanja wa Etihad juzi Jumatatu, Kompany aliachia mkwaju mkali wa mbali uliomshinda kipa Kasper Schmeichel na kuingilia kona ya kushoto ya lango ya Leicester City.

Kwa maana hiyo, City sasa itatetea ubingwa wake kama itafanikiwa kuvuna pointi zote tatu dhidi ya Brighton and Hove Albion Jumapili.

Kompany, ambaye alikuwa mwenye hisia baada ya kipenga cha mwisho, alikuwa shujaa kwa upande wa Pep Guardiola, lakini lengo la nahodha huyo ni kuona klabu hiyo inatwaa taji la nne katika kipindi chake cha miaka 11 katika klabu hiyo.

"Sijafunga msimu huu, lakini kwangu mimi katika kipindi muhimu kama hiki, ninakwenda kufanya kitu fulani, mara zote ninajisikia kwa njia hiyo," Kompany aliiambia Sky Sports.

"Kulikuwa na kuchanganyikiwa kidogo [kwangu] leo kwa sababu kila mmoja alisema usipige. Ilinitia hasira, sikuwa mbali kwa wachezaji wengine kuniambia usipige. Kwa hiyo nilichukua hatua ya kupiga.

"Nilishafunga mabao kama hayo wakati wa mazoezi. Ni hadithi ya kushangaza kwa sababu ni miaka 15 katika kiwango cha juu cha kuwa na viungo kuniambia usipige. Kwa miaka 15 nilisema usihofu, siku moja nitapiga na kufunga bao kali.

"Tunahitaji kitu fulani kutoka katikati ndani yetu kushinda. Tulihitaji zaidi kuliko ubora na ambacho kawaida tulikihitaji msimu huu. Kwa ukweli ilikuwa kiwango kizuri kwa timu na ukweli ni mwenye furaha na kila mmoja.

"Mambo wakati mwingine yanatakiwa kutokea. Yametokea tu kufunga katika wakati muafaka. Badala ya ubora, fanya kuwa bora, hilo ni bora kwangu."

Mustakabali wa baadaye wa Kompany hapo City unabaki kutofahamika, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, kunza mechi tatu mfululizo za EPL, na kukisaidia kikosi hicho cha Guardiola kuweza kumaliza bila kuruhusu bao ['clean sheets'].

"Kwa muda nimecheza kila mchezo kama ni mwisho wa kazi yangu, inakuwa kazi ngumu sana," Kompany, ambaye mkataba wake umalizika mwishoni mwa msimu, aliongeza.

"Kila mechi ni uwezekano wa mwisho. Sijui kwa pointi hii (endapo nitasaini mkataba mpya)."

## ZISIKUPITE

### FERNANDES AKARIBIA CITY

MANCHESTER City inakaribia kukamilisha dili la kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon, Bruno Fernandes, na klabu hiyo imekuwa ikijadili dili hilo kuwa kati ya pauni milioni 50 na pauni milioni 60 ili kumpata nyota huyo wa kimataifa wa Ureno. ***(Sky Sports)***

### DE LIGT AICHOMOLEA NJE CITY

BEKI wa kati wa Ajax, Matthijs de Ligt, 19, amekataa kujiunga na Man United kwa pauni milioni 60. ***(Star)***

### UTD KUAMUA POGBA REAL

KIUNGO Mfaransa Paul Pogba, 26, yupo tayari kujiunga na Real Madrid majira ya joto- lakini dili hilo linaonekana kutegemea uwezekano wa Manchester United kupunguza thamani yake ya pauni milioni 160. ***(Telegraph)***

### KLOPP ATAFUTA MABAO AJAX

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amejiunga katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Ajax, Mbrazil David Neres, 22, kwa pauni milioni 35. ***(Sun)***

### DYBALA AMULIKWA UNITED

MANCHESTER United ipo tayari kuanza kukisuka kikosi chake majira ya joto na inataka kuanza na mshambuliaji wa Juventus, Muargentina Paulo Dybala, 25, anayethaminishwa na pauni milioni 85. ***(Calciomercato, via Mail)***

### AIKATAA TENA FULHAM

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, 69, kwa mara ya pili tena amekataa ofa ya kuinoa Fulham, mara ya kwanza aliikataa kuwanoa 'Cottagers' hao Novemba mwaka jana kabla ya kuteuliwa kwa Claudio Ranieri. ***(Mail)***

### CONTE KUREJEA SERIE A

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte amesema kwa asilimia 60 kuna uwezekano wa yeye kurudi kufanya kazi ya ukocha Serie A msimu ujao. ***(Le Iene - in Italian)***

### FRASER AZIITA SPURS, ARSENAL

WINGA wa Bournemouth na Scotland, Ryan Fraser, 25, amezifungulia mlango klabu zinazomhitaji, Arsenal, Tottenham, Chelsea na Newcastle. ***(Mail)***

### CAHILL AFUNGUKA HAJAISHA

BEKI wa zamani wa kimataifa wa England, Gary Cahill, 33, ambaye anaondoka Chelsea majira haya ya joto, amesema bado hajamaliza soka lake la kiwango cha juu na akasisitiza anaweza kuendelea kucheza. ***(Talksport)***

### ZIDANE AMPA ZA USO BALE

MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale, 29, ameambiwa hahitajiki tena Real Madrid wakati walipokutana uso kwa uso na kocha Zinedine Zidane, lakini bado ameshikilia msimamo wake kuwa anataka kubaki katika klabu hiyo. ***(Mail)***

### ANCELOTTI AMTAKA LOZANO

KOCHA wa zamani wa Chelsea, kwa sasa Napoli, Carlo Ancelotti, amefunguka kutaka kumfuata winga wa kimataifa wa Mexico, Hirving Lozano, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United. ***(Calciomercato)***

## HABARI MICHEZO

# Matola afunguka alipoishikia Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA wa Lipuli FC, Selemani Matola, amesema haikuwa kazi rahisi kuifunga Yanga na kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake anapata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Lipuli FC imetinga fainali za Kombe la FA baada ya kuifunga Yanga mabao 2-0, katika mchezo uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM, Samora mjini Iringa. Akizungumza na gazeti hili jana, Matola, alisema kilichowafanya wapate matokeo mazuri katika mchezo huo ni kujipanga imara kuzuia mbinu zote za Yanga ambayo inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Matola alisema wachezaji wake walifanikiwa kufuata vema maelekezo yake hasa katika kipindi cha kwanza na kufanikiwa kupata mabao yaliyowapa ushindi katika mchezo huo.

"Mechi ilikuwa ngumu sana na tulijiandaa kukutana na hali hiyo, haikuwa rahisi kumaliza mchezo ndani ya dakika 45, ila kilichotusaidia ni kuzibaini mbinu za kocha wa Yanga (Mwinyi Zahera) na kuzidhibiti, tunamshukuru Mungu tumemaliza na ushindi," alisema Matola.

Kiungo na nahodha huyo wa zamani wa Simba, aliongeza kuwa sasa hawatabweteka na wataendelea kujiimarisha ili waweze kufanya vema katika mchezo wa fainali ambao utakuwa dhidi ya Azam FC ya jijini Dar es Salaam.

"Timu ya Yanga ni wazuri hasa katika kutumia mipira iliyokufa, pamoja na mashambulizi ya kushtukiza, hilo nililitambua na nilijua mshambuliaji wao wanayemtegemea ni Makambo (Heritier), basi nikawaweka watu wa kazi kumdhibiti na walifanikiwa kwa hilo, wamefanya kazi yao na hakuweza kufunga," alisema Matola.

Fainali za michuano hiyo zinatarajiwa kuchezwa ifikapo Juni Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi na ubingwa wa mashindano hayo uko wazi baada ya mshindi wa taji hilo msimu uliopita, Mtibwa Sugar kutolewa mapema.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 34 | 25 | 5 | 4 | 54 | 24 | 80 |
| 2. Simba | 30 | 25 | 3 | 2 | 61 | 12 | 78 |
| 3. Azam | 34 | 19 | 10 | 5 | 50 | 21 | 67 |
| 4. Mtibwa Sugar | 33 | 14 | 7 | 12 | 34 | 25 | 49 |
| 5. Lipuli | 34 | 12 | 12 | 10 | 30 | 31 | 48 |
| 6. KMC | 34 | 10 | 15 | 9 | 35 | 25 | 45 |
| 7. Ndanda | 33 | 11 | 10 | 12 | 22 | 31 | 43 |
| 8.TZ Prisons | 34 | 10 | 12 | 12 | 27 | 28 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Singida Utd | 34 | 10 | 11 | 13 | 25 | 33 | 41 |
| 11. Mbeya City | 33 | 11 | 7 | 15 | 32 | 36 | 40 |
| 12. Kagera Sugar | 34 | 9 | 13 | 12 | 30 | 37 | 40 |
| 13. Stand United | 34 | 11 | 7 | 16 | 31 | 42 | 40 |
| 14. Mbao | 34 | 10 | 10 | 14 | 20 | 33 | 40 |
| 15. Ruvu Shooting | 34 | 9 | 12 | 13 | 31 | 40 | 39 |
| 16. JKT Tanzania | 34 | 9 | 12 | 13 | 21 | 31 | 39 |
| 17. Alliance | 34 | 9 | 11 | 14 | 26 | 38 | 38 |
| 18. Biashara Utd | 33 | 9 | 10 | 14 | 25 | 31 | 37 |
| 19. Mwadu | 34 | 10 | 7 | 17 | 37 | 45 | 37 |
| 20 . African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# SAMATTA ATWAA TUZO MFUNGAJI BORA UBELGIJI

**BRUSSELS,** Ubelgiji

NAHODHA wa timu ya Taifa, Taifa Stars, anayekipiga katika Klabu ya KRC Genk, Mbwana Samatta, ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora mwenye asili ya Afrika 2019 anayecheza soka nchini Ubelgiji (Ebony Shoe Award).

Mbwana Samatta ameweka rekodi ya kuwa mchezaji wa tatu wa Genk kutwaa tuzo hiyo iitwayo Ebony Shoe Award.

**Mchezaji wa kwanza wa KRC Genk kutwaa tuzo hiyo ni Souleymane Oulare raia wa Guinea aliyeshinda mwaka 1999 na wa pili ni Moumouni Dagano raia wa Burkina Faso aliyeshinda tuzo hiyo mwaka 2002.**

Tuzo hiyo inayomaanisha kuwa kwa sasa Samatta ndiye mchezaji bora mwenye asili ya Afrika anayesakata soka Ubelgiji, ubora wake unathibitishwa na mabao 23 aliyofunga hadi sasa kwenye ligi akiwa ndiye kinara.

Baadhi ya wachezaji waliowahi kushinda tuzo hiyo na kucheza ligi kuu ya soka nchini Uingereza ni Youri Tielemens, Michy Batshuayi, Romelu Lukaku, Marouane Fellaini, Vincent Kompany, Mido Emile Mpenza na Daniel Amokachi.



Mbwana Samatta 'Samagoal', akikabidhiwa tuzo ya Mchezaji Bora Mwafrika katika Ligi ya Ubelgiji ijulikanayo kama 'Kiatu cha Ebony', katika sherehe za tuzo za Jupiler Pro League zilizofanyika juzi usiku kwenye Ukumbi wa Birmingham Palace mjini Brussels. Msimu huu katika ligi hiyo, Samatta ameifungia KRC Genk mabao 23. **PICHA: MTANDAO**

# *Zahera ageuka 'sizitaki mbivu hizi'*

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya awali kupania vilivyo ubingwa wa Ligi Kuu Bara huku pia akieleza nia yake ya kutwaa Kombe la FA ili kujihakikishia nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao, Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera sasa amegeuka 'sizitaki mbivu hizi', imefahamika.

Hiyo imekuja baada ya timu yake kutolewa katika mashindano ya Kombe la FA na kuwa kwenye nafasi finyu ya kunyakua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ambapo sasa Zahera, amesema kikosi chake hakikuwa na malengo ya kushinda taji lolote msimu huu kutokana na kukabiliwa na changamoto mbalimbali.

Yanga juzi ilifungwa mabao 2-0 na Lipuli FC na kuyaaga mashindano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake ataiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika hapo mwakani.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao wana pointi 80 na wakiwa wamebakiza mechi nne kumaliza msimu huu, wanawahofia watani zao, Simba wenye pointi 78 kutetea taji hilo kutokana na kuwa na michezo nane wakati Azam FC wanaoshika nafasi ya tatu kwenye msimamo wana alama 67.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alisema timu yake ilianza msimu huu wa mwaka 2018/19, ikiwa katika hali ngumu na hakutarajia kufika hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo ya FA.

Zahera alisema pia hata nafasi ya timu yake kukaa juu katika msimamo wa ligi kwa muda mrefu hakuitarajia na baada ya kuona inawezekana, waliamka na kuanza kupambana na kuwania ubingwa wa ligi pamoja na Kombe la FA.

"Hatukuwa na malengo ya kushinda taji lolote msimu huu, tulijua tungemaliza ligi katika nafasi ya sita au saba, na hapo ndio tuliweka malengo ya kupambana kuhakikisha tunamaliza ndani ya nafasi 10, lakini katikati ya msimu tunaona tunaweza, tulikuwa tumeshachelewa kujiandaa," alisema Zahera.

Kocha huyo aliongeza kuwa kama asingekuwa na changamoto ambazo hakuwa tayari kuzitaja, Yanga ingeweza kufanya vizuri katika mashindano yote waliyoshiriki msimu huu ikiwamo Kombe la Mapinduzi na Kombe la SportPesa Tanzania.

Kuhusu mechi dhidi ya Lipuli, Zahera alisema wachezaji wake walishindwa kufuata mbinu ya kwanza waliyoingia nayo na kusababisha kufanya mabadiliko ya wachezaji wake akiwamo nahodha Ibrahim Ajibu ambaye krosi alizokuwa anapiga hazikuzaa matunda yoyote.

Kikosi cha Yanga kilitarajia kurejea jijini Dar es Salaam jana na kuanza safari ya kuelekea mkoani Mara kuwafuata Biashara United kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma.

Endapo Yanga ambayo Jumapili ilipata viongozi wapya, itashindwa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara, itakosa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa mwakani ikiwa ni msimu wa pili mfululizo.

# Michezo

Jumatano Mei 8, 2019

Nipashe




Samatta atwaa tuzo mfungaji bora Ubelgiji HABARI UK.31



Kwaya ya Usharika wa KKKT, Azania Front, ikiimba katika ibada maalum ya kuaga mwili wa marehemu Mwenyekiti wa IPP, Dk. Reginald Mengi, iliyofanyika katika Ukumbi wa Karimjee, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Siri ya Dk. Mengi Stars Afcon 2019

●●● Waziri Mwakyembe aeleza ni pigo kubwa kwao, aanika walivyoteta naye ili kuhakikisha...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI familia, wafanyakazi na Watanzania kwa ujumla wakiendelea kumlilia na kuomboleza msiba wa Mwenyekiti wa IPP, Dk. Reginald Mengi, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amesema kufariki dunia kwa mwenyekiti huyo ni pigo kwa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inatarajia kuanza maandalizi ya kushiriki kwa mara ya pili Fainali za Afrika (Afcon) 2019, zitakazoanza baadaye mwezi ujao jijini Cairo, Misri.

Akizungumza wakati wa kuaga mwili wa marehemu Dk. Mengi, katika Ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam jana, Waziri Mwakyembe alisema wizara na taifa limepata pigo kwa kuondokewa na Mlezi huyo waTimu ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), huku akitoa siri kuwa mfanyabiashara huyo alitaka kujua maandalizi ya Stars yatakavyokuwa.

**Mwakyembe alisema wadau wa michezo watamkumbuka sana Dk. Mengi kutokana na kushiriki kwake kikamilifu katika kuhakikisha maendeleo ya timu za taifa yanapatikana.**

"Baada ya timu ya vijana ya Serengeti Boys kufanya vibaya katika mashindano ya Afcon, Dk. Mengi alinipigia simu kutaka kujua tunaanza lini maandalizi ya Taifa Stars, kusema kweli tumepata pigo," alisema waziri huyo.

Alisema mbali na kutoa mchango kwa timu hizo za Taifa, pia Dk. Mengi atakumbukwa kwa mchango wake wa kusaidia wanamichezo mbalimbali ikiwamo klabu yake ya Yanga ambayo alikuwa mwanachama. Taifa Stars imefuzu kushiriki Fainali za Afrika ambazo zitafanyika kuanzia Juni 21 hadi Julai 13, mwaka huu huko Misri.

Katika fainali hizo, Stars inayofundishwa na Mnigeria Emmanuel Amunike, imepangwa Kundi C pamoja na nchi ya Algeria, Senegal na majirani zao, Kenya [Harambee Stars].

Katika kuhamasisha mafanikio ya soka, Dk. Mengi alitumia kaulimbiu yake ya 'I Can, I Must, I Will' kwa timu ya Serengeti Boys iliyokuwa ikishiriki Fainali za Afcon 2019 zilizofanyika nchini mwaka huu.

Wakati huo huo, warembo waliowahi kushika taji la Miss Tanzania, Faraja Kotta (2004), Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe na Miss Tanzania namba mbili (2006), Jokate Mwegelo, Nasreen Kareem (2008) na wasanii mbalimbali wa muziki wa kizazi kipya walikuwa ni baadhi ya wananchi waliojitokeza kumuaga marehemu, Dk. Mengi.

Dk. Mengi ambaye alizaliwa mwaka 1942, alifariki dunia huko Falme za Kiarabu usiku wa kuamkia Mei 2, mwaka huu na anatarajiwa kuzikwa kesho Alhamisi kijijini kwao Nkuu Sinde Kata ya Machame Mashariki wilayani Hai, Kilimanjaro.

# Simba kileleni Ligi Kuu leo?

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, leo watakuwa na nafasi ya kukwea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, watakapoikaribisha Coastal Union kutoka Tanga kwenye mechi itakayopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Simba yenye pointi 78, inahitaji ushindi kwenye mechi ya leo, si tu kujiweka nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, lakini pia kuanza kuongoza Ligi Kuu kabla ya kubeba taji hilo.

Timu hiyo ambayo msimu huu imekuwa ikiiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, ilikuwa ni kama imejimilikisha nafasi ya tatu, huku mara chache ikishuka hadi nafasi ya nne kabla ya hivi karibuni kupanda hadi nafasi ya pili.

Itakuwa ni mechi 31 kwa timu hiyo, tatu nyuma ya vinara wa Ligi Kuu kwa sasa Yanga yenye pointi 80, ikiwa imecheza michezo 34. Na iwapo Simba itashinda mechi ya leo itafikisha pointi 81, hivyo kukalia usukani.

Simba itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 zilipokutana kwa mara ya kwanza msimu huu, Aprili 17 kwenye Uwanja wa Mkwakwani.

Itakuwa ni mechi ya 34 kwa Coastal ambayo mpaka sasa imevuna pointi 41, ikikamata nafasi ya 10, lakini kulingana na pointi za washindani wake huko chini, bado haijawa na uhakika wa kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara kama itafanya vibaya kwenye mechi zake tano zilizobaki.

Kocha wa Simba Patrick Aussems amesema kuwa amewaandaa vijana wake kuelekea kwenye mechi hiyo na wanajua umuhimu wa kushinda kila mechi zilizobaki ili kutwaa ubingwa, huku Kocha wa Coastal, straika wa zamani wa timu hiyo, Juma Mgunda akisema kuwa wamekuja Dar es Salaam kuhakikisha wanapambana ili kurudi Tanga na pointi tatu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >